

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Arobaini na Saba - Tarehe 14 Juni, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na swali linaulizwa na Mheshimiwa Chikambo.

Na. 384

**Umuhimu wa Wabunge wa Viti Maalum Kwenye  
Kamati za Fedha na Mipango za Halmashauri**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza:-

Kamati za Fedha na Mipango za Halmashauri ni Kamati muhimu ndani ya Halmashauri kwa Wabunge wote kushiriki vikao vyake bila kujali ni Mbunge wa Jimbo au Viti Maalum kwa sababu Kamati hiyo inashughulikia masuala ya kifedha, ikiwemo bajeti na mipango ya miradi ya maendeleo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kwa sasa upo umuhimu wa kushiriki Wabunge wa Viti Maalum kwenye Kamati hizo?

(b) Kama jambo hilo linatokana na sheria, je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuleta Bungeni mabadiliko ya sheria kandamizi kama hii ambayo haina tija?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye Sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Serikali za Mitaa, Wabunge wa Viti Maalum siyo Wajumbe wa moja kwa moja wa Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri, isipokuwa kama watateuliwa na Meya au Mwenyekiti na kuidhinishwa na Baraza la Madiwani.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo umewekwa kwa mujibu wa Sheria, Sura Namba 287, Mamlaka za Wilaya na Sura Namba 288, Mamlaka za Miji, zilizotungwa na Bunge lako Tukufu hauna ukandamizaji wowote bali ni kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri. Hivyo, kwa sasa mfumo wetu wa kisheria hauna upungufu unaolazimu kufanya marekebisho ya sheria zilizopo, ikizingatiwa kwamba, Halmashauri moja inaweza kuwa na Mbunge kwa Viti Maalum na kuteuliwa zaidi ya mmoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza ikumbukwe kwamba jambo hili

tumekuwa tukilizungumza hapa mara nyingi, hii ni kuonesha kwamba sisi Wabunge wa Viti Maalum tunakerwa na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Naibu Waziri amekuwa akiyarudia hayo hayo kila siku anasema jambo hili limewekwa kwa mujibu wa sheria na mimi nafahamu kwamba sheria sio Msahafu wala Biblia. Napenda kujua ni lini sasa Serikali italeta sheria hiyo Bungeni ili kufanyiwa marekebisho? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi maana muda wetu ni mdogo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapa hii ni kwa mujibu wa sheria, kwa mfano, tufanye *reference* ya Jimbo au Halmashauri ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti wetu Zungu hapa yupo, Halmashauri ya Ilala ina Wabunge wa Jimbo wasiopungua watatu, Jimbo la Ukonga, Jimbo la Segerea na Jimbo la Ilala ambapo kwa mujibu wa sheria inasema wale ni Wajumbe wa moja kwa moja lakini lina Wabunge Walioteuliwa na Viti Maalum zaidi ya saba. Kwa hiyo, hapo unaona ni jinsi gani hali ilivyo, ndiyo maana nikasema sheria inaelekeza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi sheria iko hivyo, lakini kama kutakuwa na *amendment* yoyote ambayo inapendekezwa, basi Wabunge wenyewe ndiyo tutafanya maamuzi katika hilo kuona ni jinsi gani tutafanya. Majibu haya siyo ya Jafo ni ya Serikali na kutokana na sheria ambapo Bunge hili sisi wenyewe ndiyo tumetunga.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali hili lina maneno mengi lakini jibu sahihi leteni *amendment* Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Mheshimiwa Francis Koka.

Na. 385

## **Kupandisha Hadhi Kituo cha Afya Mkoani - Kibaha**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Kituo cha Afya cha Mkoani, Kibaha Mjini kina matatizo mengi ikiwemo ukosefu wa miundombinu ya kutolea huduma lakini kinahudumia wakazi zaidi ya 150,000 wa Mji wa Kibaha:-

Je, Serikali imefikia wapi kuhusu mpango wa kukifanya kituo hicho kuwa Hospitali ya Wilaya ili kipate hadhi ya kutoa huduma ya kuridhisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhitaji wa uwepo wa Hospitali ya Wilaya kwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha. Hata hivyo, Kituo cha Afya cha Mkoani bado kinakabiliwa na upungufu wa baadhi ya miundombinu inayohitajika kuwa Hospitali ya Wilaya. Serikali imeendelea kukiboresha kituo hicho ili kuweza kuwa na hadhi ya hospitali ambapo mnamo tarehe 19/01/2017 kilifanya upasuaji wa mama wajawazito kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2017/2018, Serikali imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya kulaza wagonjwa na shilingi milioni 100 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa gari la wagonjwa ikiwa ni mkakati wa kuongeza miundombinu inayohitajika ili kiwe ni Hospitali ya Wilaya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Koka.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri yanayotia moyo. Pamoja na majibu hayo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, Mji wa Kibaha sasa una wakazi takribani 150 na katika Kituo cha Afya Mkoani kuna msongamano mkubwa na ukizingatia ni Kituo cha Afya pekee katika mji wetu. Serikali ina mpango gani angalau kujenga vituo vingine vya afya katika kata zilizoko pembezoni ili kusogeza huduma hii kwa wananchi na kuondoa msongamano mkubwa katika Kituo hiki cha Afya wakati kinaendelea kuboreshwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pamoja na msongamano huu bado kuna tatizo kubwa la dawa chache zinazopewa Kituo hiki cha Afya, jambo linalosababisha wagonjwa kukosa dawa na kuwa na malalamiko. Je, Waziri anasaidia vipi kituo hiki ili kiweze kupata dawa za kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Koka ni kweli na ni jambo la msingi na napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amefanya juhudi kubwa sana katika kile Kituo cha Mkoani mpaka pale kilipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkakati wa kuongeza vituo vya afya, nimhakikishie Mheshimiwa Koka wakifanya *needs assessment* katika Halmashauri yao na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika mchakato wa bajeti hatutasita kuunga mkono kuhakikisha kwamba pale Kibaha ambapo *population* ni kubwa sana ambayo yeye anaihudumia, tutafanya jitihada za pamoja sisi na Serikali Kuu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kibaha pale kuona ni jinsi gani tutafanya tuongeze idadi ya vituo vya afya ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la dawa na vifaatiba, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Koka kwamba, hivi sasa katika bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha kwa kila Halmashauri tumeongeza bajeti kwa ajili ya dawa na vifaatiba kupitia *Basket Fund*. Kwa hiyo, jukumu kubwa sana tutakaloenda kulifanya ni suala zima la usimamizi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba tuta-*cross check* vizuri kwamba kwa Kibaha nini kimefanyika lakini hata hivyo nilitoa maelezo mahsusni kwa Kibaha Vijijini na Kibaha Mjini tulipokutana Mlandizi, jinsi gani wafanye ili fedha ambazo tumezileta ziweze kutumika kununua dawa na vifaa tiba katika eneo lake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Oliver.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba uniruhusu nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ziara yake aliyofanya Rombo katika Kituo cha Afya cha Karume na kuhimiza sana ujenzi na ukamilishaji wa kituo kile. Mheshimiwa Waziri, kazi aliyofanya pale inaendelea vizuri na jambo lililobaki ni umaliziaji wa jengo la *OPD*. Je, sasa Wizara iko tayari kutusaidia ili jengo lile lipate kukamilika na kituo kile kiweze kupandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya kama ilivyo kusudio lake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulifika na Mheshimiwa Mbunge pale Rombo na tumeweza kubaini ule mchakato na naomba nimhakikishie kwamba mara baada ya kuona mahitaji, Serikali tumeweka katika mipango jinsi gani tuwasadie wananchi wa pale. Kwa hiyo, kulimalizia

eneo lile ili wananchi wapate huduma liko katika mpango wa Serikali, wala Mheshimiwa Mbunge asihofu. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Swali lililoulizwa Na.385 linafanana na Wilaya ya Karagwe, haina Hospitali ya Wilaya, inayo Hospitali Teule ya Nyakanga ambayo inatoa huduma za tiba kwa Wilaya mbili, Karagwe na Kyerwa. Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ili kuboresha huduma za afya? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na Mbunge mwenyewe ni shahidi wakati tunakabidhiwa ile Shule ya Ununio pale Bukoba tulijadili suala zima la Karagwe na kweli tulifika mpaka Karagwe kubaini matatizo yaliyopo pale. Jambo la kwanza tuliloweza kulifanya ni kuhakikisha kwamba katika kile Kituo chao cha Afya cha Karagwe kukiboresha vizuri kwa kuweka miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikwambie kwamba Serikali hivi sasa tunaenda kujenga *theatre* kubwa sana ya upasuaji na kupeleka vifaa vyote pale takribani vya shilingi milioni 700. Hata hivyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo vilevile alifanya harakati za kuomba majengo yaliyokuwa ya *TANROAD* kuhakikisha tunatoa huduma ya afya katika Wilaya ya Karagwe, hii yote ni jukumu la Serikali kuisaidia Wilaya ya Karagwe iweze kupata huduma vizuri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza.

Na. 386

## Uporwaji wa Maeneo ya Umma

**MHE. UPENDO F. PENEZA** aliuliza:-

Kumekuwa na uporwaji wa maeneo ya umma kama vile maeneo ya Shule ya Kalangalala Geita Mjini na maeneo ya Serikali za Mtaa:-

Je, ni lini Serikali itafanya uchunguzi na kurudisha maeneo hayo kwa umma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna wananchi wanne wamevamia eneo la Shule ya Sekondari ya Kalangalala iliyoko Halmashauri ya Mji wa Geita, ambao wamejenga nyumba zao ndani ya mchoro wa Mpango Miji wa eneo la shule. Halmashauri kwa kushirikiana na mkoa imepanga kuwaondoa wananchi hao waliovamia na kujenga kwenye eneo la shule. Aidha, maelekezo yametolewa kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha maeneo yote ya umma yanapimwa na kupatiwa hati miliki ikiwemo shule, vituo vya kutolea huduma za afya na maeneo ya wazi yaliyotengwa kwa matumizi mbalimbali ya umma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu lilikuwa linajielekeza katika Shule ya Msingi ya eneo la Kalangalala ambalo wananchi wanatumu Chama Tawala – CCM kuvamia eneo la



uwanja wa shule hiyo na kujimilikisha uwanja huo. Sasa ninachouliza hapa, limeshashughulikiwa katika maeneo yao, ni lini sasa Serikali itaenda kuumaliza mgogoro huu ili hatimaye Uwanja wa Shule ya Msingi ya Kalangalala uweze kurudi mikononi mwa shule na siyo mkononi mwa chama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lingine ni mkanganyiko mkubwa ambao uko ndani ya Halmshauri nzima ya Geita Mjini ambapo Wenyeviti wetu wa Serikali za Mtaa, wale Wenyeviti waliopita chini ya CCM leo hii viongozi wengine kuingia katika zile ofisi imekuwa ni shida. Hii inatokana na kwamba, wao walivyokuwepo ofisi hizo zilikuwa ni mali ya Serikali, wameondoka ofisi hizo sasa ni mali za chama pamoja na ardhi. Ni lini Serikali itaweza kuushughulikia huu mgogoro ili hatimaye...

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali sasa. Ni lini sasa Serikali itashughulikia huu mgogoro ili yale maeneo ambayo ni ya Serikali yaweze kuondokana na huu mgogoro wa chama na yabaki kama maeneo ya Serikali? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama nilivyosema, kuna timu imeundwa na agizo hili tumetoa sisi Ofisi ya TAMISEMI na timu ya Mkoa na Halmashauri inafanyia kazi suala hili. Tumeelekeza maeneo yote ya taasisi za Serikali yanatakiwa yabaki katika taasisi ya Serikali *regardless* nani amechukua eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba, Ofisi ya Mkoa inafanya juhudi hiyo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wote waliovamia wanaondoka ili maeneo yaliyopangwa kwamba ni ya shule yabakie kuwa maeneo ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la ofisi hizi kwamba nyingine ni za chama, ninachojua ni kwamba vijiji vina ofisi zao za vijiji, lakini maeneo mengine tulikotoka kwa sababu historia inaonesha kwamba vijiji vingi sana viongozi wake walikuwa ni wa CCM na utakuta maeneo mengine yaliyokuwa majengo ya CCM ndiyo yalikuwa yanatumika kama majengo ya Serikali, kuna *scenario* kama hiyo. Kwa hiyo, kama kuna *scenario* kama hiyo kwamba majengo mengine yalikuwa ya CCM na kwa sababu Mwenyekiti wa Kijiji ni wa CCM ametumia majengo haya hatuwezi kusema kwamba yatarudi Serikalini kwa sababu jengo lile *original* yake ilikuwa ni jengo la Chama cha Mapinduzi, lakini kama eneo lile limejengwa kwa ajili ya Ofisi ya Kijiji, hiyo haina mjadala ofisi hiyo itakuwa ni Ofisi ya Kijiji kwa mujibu wa taratibu zote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gekul jandae Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu katika majibu yako kwamba maeneo hayo ya Serikali yapimwe yakiwemo maeneo ya shule. Hili tatizo ambalo limetokea Geita liko pia katika Jimbo langu la Babati Mjini ambako shule za sekondari na za msingi zimevamiwa. Kwa nini Wizara yake ya TAMISEMI isiongee na Wizara ya Ardhi tupewe vifaa vya kupima maeneo ya shule na pawepo na *time frame* kwa sababu vifaa hivyo sasa viko Kanda, kwa nini wasiongee Wizara mbili tupatiwe vifaa tupime maeneo hayo kuepusha uvamizi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, tumekuwa na tatizo hili kubwa sana. Maeneo mengi ukifika kuna changamoto hii kubwa hasa maeneo ya mijini, Mheshimiwa Zungu anafahamu maeneo yao yamevamiwa sana. Ndiyo maana tumetoa maelekezo kupitia Ofisi za

Makatibu Tawala wa Mikoa kuhusu mchakato wa upimaji. Naomba nimhakikishie kwamba zoezi hili hivi sasa katika maeneo mengine linaenda vizuri zaidi. Kwa mfano, hata Mkoa wa Geita, nimepata ripoti yao hivi sasa wanaenda vizuri zaidi katika suala hilo la upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwaambie kwamba tumetoa *go ahead* hii sasa katika Halmashauri zetu zishirikiane na Ofisi zetu za Kanda na Wizara ya Ardhi kuona jinsi gani uwezeshaji kupitia Ofisi ya Kanda unafanyika kwa haraka ili kusaidia zoezi hili. Siwezi kusema vifaa hivyo vitatolewa lini lakini sasa hivi Ofisi za Kanda zinashughulikia suala zima la upimaji wa maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru Naibu Waziri amelijibu vizuri, lakini napenda tu nitoe rai, kama nilivyosema wiki iliyopita tunahitaji maeneo yote yapimwe na taasisi nyingi hazijapima maeneo yake, lakini tumeitaka Mikoa husika waunde vikosi katika maeneo yao kwa sababu unaweza ukakuta Halmashauri moja haina wataalam na vifaa vya kutosha, wakishirikiana na Ofisi za Kanda waunde timu katika Halmashauri zile kwa kuchukua wataalam ndani ya Mkoa waende katika maeneo kama timu au kikosi maalum kwa ajili ya kufanya upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kufanya hivyo, pengine tunaweza tukachukua muda mrefu. Kwa hiyo, niombe pia hata Manyara watumie zile Halmashauri zao pamoja na Ofisi ya Kanda kuweza kutumia vifaa vilivyopo katika kupima Halmashauri moja baada ya nyingine, tutakuwa tumekamilisha zoezi hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Malizia Mheshimiwa Malembeka malizia.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nishukuru kwa majibu

mazuri aliyotoa Naibu Waziri, TAMISEMI, hususan katika kutoa maelekezo kwamba Halmashauri zote zipime maeneo yao. Halmashauri nyingi hazina fedha kwa ajili ya kugharamia upimaji wa ardhi. Je, Waziri haoni kwamba sasa hivi ni wakati muafaka kwa kuwa Serikali inapima maeneo yake huduma hiyo itolewe bure kwa Halmashauri? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Swali fupi na majibu yawe mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu wa upimaji, inawezekana mkapata fedha kutoka *Central Government*, Halmashauri inaweza ikafanya *resource mobilization* yenyewe ikapata fedha, lakini vilevile kuna suala zima la *PPP* ambalo Wizara ya Ardhi ilikuwa inalizungumza, hivi sasa kuna wapima binafsi ambao kwa kushirikiana na Halmashauri wanafanya zoezi hilo la upimaji. Kwa hiyo, suala la *negotiation* likifanyika naamini zoezi hili la upimaji litaenda vizuri lakini wazo la Mheshimiwa Malembeka tumelichukua. Hata hivyo, naomba nizihamasishe Halmashauri kwamba tutumie mfumo wa *PPP* ili mradi kufanya upimaji uende vizuri katika Halmashauri zetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Godwin Mollel.

Na. 387

### **Hitaji la Wodi ya Wagonjwa na Jengo la Upasuaji Hospitali ya Wilaya ya Siha**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. DKT. GODWIN A. MOLLEL)** aliuliza:-

Hospitali mpya ya Wilaya ya Siha ina upungufu mkubwa wa majengo ya wodi ya kulaza wagonjwa, jengo la upasuaji na upungufu mkubwa wa vifaa tiba jambo ambalo linasababisha ifanye kazi chini ya kiwango na kukosa hadhi ya Hospitali ya Wilaya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha hospitali hiyo na kuipatia vifaa tiba ili kuipa hadhi stahiki ya kuwa Hospitali ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Aloyce Mollel, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali iliidhinisha shilingi milioni 250 kwa ajili ya kumalizia jengo la wagonjwa wa nje ambalo linaendelea kutoa huduma za dharura kwa akinamama wajawazito na watoto. Fedha zote zimepelekwa katika Halmashauri na ujenzi utakamilika Julai, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa vifaatiba, Serikali imetoa fedha zote shilingi milioni 247.2 ambazo sehemu ya fedha hizo zinapaswa kutumika kununua vifaatiba. Pia katika mwaka wa fedha 2017/2018 zimetengwa shilingi milioni 228.2 za Mfuko wa Pamoja wa Afya ambapo theluthi yake ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Aidha, Halmashauri inatakiwa kuimarisha makusanyo ya fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii yaani *CHF* pamoja na matumizi sahihi katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza uwezo wa ndani wa kununua vifaa tiba na dawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa wananchi wamekuwa wakihamasishwa sana kujiunga katika Mfuko wa Afya ya Jamii kwa maana ya *CHF* lakini ni ukweli kwamba wanapokwenda kupata huduma za afya katika maeneo mbalimbali wamekuwa hawapati dawa na matokeo yake wanaandikiwa wakachukue dawa kwenye maduka ya

dawa binafsi. Je, Serikali haioni sasa iko haja ya kusitisha kwanza uhamasishaji huu ili iwahakikishie upatikanaji wa dawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa suala la upatikanaji wa dawa na vifaa tiba imekuwa ni changamoto ya muda mrefu kwa maana ya kwamba haitoshelezi katika zahanati zetu, vituo vya afya na Hospitali za Wilaya. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kufikiria kuwa na Mfuko wa Dawa na Vifaatiba kama ilivyo Mifuko mingine ya Barabara, Mazingira, Umeme Vijijini ili kuwahakikishia Watanzania wanapata dawa na vifaa tiba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusitisha CHF kwamba watu wanaenda hawapati dawa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna maeneo mengine kuna *best practice* ya CHF inaendelea hivi sasa. Kwa hiyo, kuna maeneo mengine yenye upungufu lakini maeneo mengine utaratibu unakwenda vizuri. Ndiyo maana kupitia Serikali yetu tumeona kwamba katika *Basket Fund* tuweze kufanya *compliance* nzuri ya matumizi yake na umeona nimetoa taarifa mbalimbali kwamba mwanzo hata hizi fedha za *Basket Funds* ambazo zingesaidia upatikanaji wa dawa za kutosha ulikuwa hautumiki vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tumeweka *commitment by the end of this June* Halmashauri zote zitakazoshindwa kutumia vizuri *Basket Fund* kwa ajili ya madawa na vifaatiba, Ma-DMO tumewaambia wazi kwamba tutaenda kuhakikisha kwamba tunawaweka pembeni, tutawapata watu wengine ambao wanaweza kufanya hiyo kazi. Kwa hiyo, naomba nimshauri kwamba CHF tuendeleo nayo, lakini tutaenda kutatua ule upungufu uliokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuanzisha Mfuko wa Dawa Maalum kama ilivyokuwa Mfuko wa Barabara na

mifuko mingine, hili nasema ni wazo, lakini hivi sasa ukiangalia utaratibu mzuri kwa mfano niwapongeze sana wenzetu wa Muheza. Nilipofika pale *Drug Revolving Fund* inafanya vizuri sana na niliwaambia ma-DMO wengine waweze kujifunza *best practice* ambayo imetokea kule Muheza na hivi sasa ukiangalia sehemu zingine wanaiga hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, tuhamasishane kuiga mambo mengine mazuri lakini lazima twende na utaratibu mzuri wa kutumia mifuko hii vizuri na fedha zinazokuja zitumike vizuri kwa ajili ya manufaa ya wananchi wetu. Jambo hili nasema ni wazo zuri lakini tunaendelea kulifanyia kazi, nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Suala la Hospitali ya Wilaya, Wilaya yangu ya Ileje ilipata nafasi au ilipata fursa ya kujengewa Hospitali ya Wilaya lakini ni miaka miwili haijamaliziwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri kama anaweza kutufanyia tathmini ya kiwango kilichobakia ili waichukue ile hospitali waimalizie. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mama Mbene tulizungumza na ameniambia jambo hili na tumekubaliana kwamba mara baada ya Bunge hili la bajeti tutaenda kule Mkoa wa Songwe na tutafika Ileje kwa ajili ya kuhakikisha tathmini tunaifanyia *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunaenda kuboresha Kituo chake kimoja cha Afya ili kuhakikisha huduma za upasuaji zinapatikana. Kwa hiyo, jambo hili tumelichukua na tutakavyokuwa *site* kule tutajadiliana mambo mengi sana kuwasaidia wananchi wa Ileje.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Matatizo ya vifaatiba ya hospitali ya Siha yanafanana sana na matatizo ya vifaatiba ya Hospitali ya Wilaya Mafya. Hospitali ya Wilaya ya Mafia kwa muda wa miaka minne sasa haina *X-ray machine*. Wananchi wa Mafia kupitia Mbunge wao na wafadhili mbalimbali tumeweza kununua *X-ray machine* mpya na mpaka leo bado tunasubiri ruhusa ya Waziri ili tuweze kuitoa ya zamani na kulfunga mpya. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akalielezeaje suala hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu hilo la siku zote, ndiyo hoja ya Mafia. Mpe majibu arudi tena Bungeni 2020. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Dau siyo kama anaongopa na hili jambo amelizungumza mara kadhaa na mama yangu hapa nakumbuka siku hiyo tumefika mpaka pale hospitali. Waziri wangu alitoa maelekezo *specific* kuhusu Mafia katika jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuzungumza hapa sasa hivi lakini niseme kwamba hili jambo ni la muda mrefu, kama Serikali sasa tunaangalia jinsi gani tutafanya kuangalia maelekezo ambayo Waziri wangu alitoa yamefikia wapi na upungufu uliobakia tuweze kuu-*address* vizuri ili tumalize tatizo hilo na wananchi wa Mafia wapate huduma.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maryam Msabaha ajiandae Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali ndogo la nyongeza. Sambamba na Hospitali hizi za Wilaya lakini kuwekuwa na tatizo sugu la Madaktari. Je, ni lini Serikali itahakikisha Hospitali hizi za Wilaya zinapatwa Madaktari wa kutosha? (*Makofi*)



**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali jipya ujibu kwa kuwa wewe ni mzoefu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la *coalegue* wangu wa Bulombola dada Msabaha. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeliona hili ndiyo maana katika kipindi cha sasa hivi tumeweza ku-*distribute* Madaktari katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, najua kwamba wale Madaktari tuliowapeleka kule bado hawajatosheleza. Ndiyo maana Waziri wa Utumishi hapa alikuwa akizungumza sasa tutaajiri baadhi ya wataalam, naomba nimhakikishie kwamba tutakapoajiri Madaktari katika sekta ya afya tutazidi kuwa-*distribute* katika wilaya zetu ili mradi wananchi wetu waweze kupata huduma.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. MPAKATE D. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jimbo la Tunduru Kusini lina vituo vya afya vitatu Mkasale, Ntina na Mchoteka na vyote havitoi huduma ya upasuaji. Je, Serikali itaisaidiaje zahanati hizi ili ziweze kupata huduma ya upasuaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge anakiri wazi kwamba tulikwenda pamoja Jimboni kwake na ni kweli ni miongoni mwa Jimbo lenye changamoto kubwa sana. Mara baada ya kubaini zile changamoto ndiyo maana kwa pamoja mimi na yeye tumekubaliana sasa tutaenda kufanya huduma za upasuaji mkubwa sana katika moja ya vituo vyake vya afya, lengo letu ni kuwasaidia wananchi wale. Kwa hiyo, jambo hili liko katika *commitment* na Serikali imeshatenga fedha na nadhani si muda mrefu sana ndani ya mwezi huu mmoja kazi itaanza katika kituo chako kimoja cha afya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji.

Na. 388

### **Bajeti Ndogo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

**MHE. MWANTUMU D. HAJI** aliuliza:-

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imekuwa ikitengewa fedha kidogo sana katika bajeti kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo hali inayosababisha Tume hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo:-

Je, Serikal ina mpango gani wa kuitengea bajeti ya kutosha Tume hiyo ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya ukomo wa bajeti kwa mafungu, hutegemea vipaumbele vya Taifa na maoteo ya mapato katika kipindi husika. Katika mwaka wa 2017/2018, ukomo wa bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni Sh.6,166,978,000/= ikilinganishwa na Sh.3,557,589,200/= ya mwaka 2016/2017 ikiwa ni ongezeko la asilimia 42.31. Ongezeko hili la asilimia 42.31 linadhihirisha kwamba Serikali yetu inatambua umuhimu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pamoja na majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuhakikisha kuwa mafungu yote ya kibajeti ikiwemo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora yanaendelea kupata fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tarehe Mosi Juni, 2017, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ujulikanao kama *Revenue Gateway System* ikiwa ni mojawapo ya mikakati ya Serikali ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato yake. Aidha, Serikali itaendelea kutenga na kutoa fedha kukidhi mahitaji ya mafungu mbalimbali kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa na upatikanaji halisi wa mapato.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Dau.

**MHE. MWANTUMU D. HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa vile Serikali imeliona na kuanza kulifanyia kazi jambo hili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutuahidi kuwa bajeti hii iliyopangwa itapelekwa kwa wakati ili hatimaye Tume hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu iko tayari kabisa kupeleka fedha zote zilizopangwa katika mwaka huu 2017/2018 kama ambavyo tumefanya katika mwaka 2016/2017 na mpaka sasa tumeshapeleka asilimia 98 ya bajeti yote ya Tume ya Haki za Binadamu. Kwa hiyo, tuko tayari kabisa kama Serikali na kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba tunafahamu majukumu na tunatambua umuhimu wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Msaada utolewe au haki ya mtu itolewe kwa mujibu wa zile shida zake. Hii Tume jamani ina matatizo makubwa mno, ya ofisi, ya vitendea kazi, lakini ukisema asilimia 40 ambayo haiendi kusaidia hata asilimia mbili ya matatizo yake inakuwa tumefanya nini? Ni lini Serikali itakuwa inapanga pesa kwa mujibu wa matatizo na mahitaji ya taasisi muhimu kama hii? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema upangaji wa bajeti kwa Mafungu yoyote hutegemea maoteo na makisio ya mapato ya Serikali. Huwezi kupanga kitu ambacho kiko nje ya kile ambacho kile Serikali inatakiwa kukipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwenye jibu langu la msingi kwamba katika Mafungu ambayo tunayaangalia kwa jicho la kipekee ni Mafungu ya Tume ya Haki za Binadamu. Kama nilivyosema kwa mwaka huu unaokwisha tayari tumeshapeleka asilimia 98 ya bajeti yao, kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha fedha hizi zinakwenda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issaay, ajiandae Mheshimiwa Ungando.

**MHE. ZAKARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Bunge letu liliridhia uwepo wa Wasaidizi wa Kisheria katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Muswada ambao tumeupitisha hapa Bungeni. Je, lini wadau hawa muhimu sana watatoa huduma yao kupitia Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa vijijini kuhusu hatua mbalimbali za kisheria?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema yeye Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria hapa na Serikali yetu ipo tayari kuhakikisha kwamba sheria hii inatekelezwa kama ilivyopitishwa. Bajeti yao tayari imeshatengwa na wataanza kutekeleza majukumu yao ndani ya mwaka huu wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa. Mheshimiwa Ungando

**MHE. ALLY S. UGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kutokana na mauaji yanayoendelea maeneo ya Kibiti, Halmashauri ya Kibiti inashindwa kukusanya mapato makusanyo yake ndani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuipelekea fedha Halmashauri hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu au Waziri wa Mambo ya Ndani utajibu hilo?

**WABUNGE FULANI:** Wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapa pole ndugu zangu Wanakibiti kwa haya yanayoendelea kutokea. Ni imani yangu Serikali yetu tunashughulikia kwa nguvu zote kuhakikisha shida hii inapotea katika Wilaya yetu ya Kibiti na Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upelekaji wa fedha kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, mafungu yote yametengewa fedha na tutahakikisha yanapatiwa fedha. Nina uhakika kama nilivyosema tunashughulikia kama Serikali tatizo hili la Kibiti na Rufiji na Halmashauri zetu zitaweza kukusanya fedha kama ambavyo imepangwa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Bilakwate.

Na. 389

### **Kushuka kwa Bei ya Zao la Kahawa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuza:-

Zao la kahawa ni miongozi mwa mazao makuu ya biashara lakini bei yake imekuwa ni ya kukatisha tamaa kitu kinachosababisha wengine kung'oa na kuikata kabisa kwa sababu nchini mwetu bei ni ndogo sana ikilinganishwa na majirani zetu wa Uganda. Wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais aliahidi kuondoa tozo zote pamoja na kodi zinazomdidimiza mkulima wa kahawa:-

(a) Je, Serikali imefika wapi katika kuondoa ushuru na kodi zinazomfanya mkulima asione faida ya kuendelea na zao hili?

(b) Kama Serikali haiko tayari kuondoa tozo na kodi, je, iko tayari kuwaruhusu wakulima wauze kule ambako watapata bei nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUNGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifungo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Jimbo la Kyerwa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya uchambuzi wa kina na kubaini baadhi ya tozo, ada na ushuru unaotozwa kwenye mazao ya biashara haukuwa na mahusiano na uendelezaji wa mazao. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeondoa jumla ya tozo 80 na kupunguza viwango tozo nne katika tasnia ya mazao pekee kati ya jumla ya tozo 139 zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakavyokumbuka, katika mwaka 2016/2017, Serikali ilifuta ada ya leseni ya kusindika kahawa na Dola Marekani 250. Aidha, katika mwaka 2017/2018 kwenye tasnia ya kahawa pekee, jumla ya tozo 17 zinafutwa na tozo moja imepunguzwa kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaamini kuwa hatua hiyo inamnufaisha mkulima kwani baadhi ya tozo zilizofutwa zilikuwa zinatozwa moja ka moja kwa mkulima na hivyo kupunguza kipato chake. Aidha, zilikuwepo tozo ambazo zilikuwa zinatozwa kwa wafanyabiashara wa kahawa ambazo pia huathiri kipato cha mkulima wa kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa wafanyabiashara hao hawana namna nyingine ya kuweza kushawishi ongezeko la bei kwenye soko la dunia au kwa mtumiaji kutokana na kuwepo kwa tozo hizo, hivyo

hulazimika kuhamisha mzigo wa gharama kubwa za masoko zinazosabishwa na tozo kwa kumlipa mkulima fedha kidogo katika mazao yake ili kuwa na ushindani katika biashara ya mazao ya nje.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo tayari ipo tayari kuondoa kodi na tozo mbalimbali za mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi zisizokuwa na tija kama ilivyofanya mwaka 2016/2017. Kwa mwaka 2017/2018, Wizara inakusudia kuendelea kuondoa au kupunguza kodi mbalimbali kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili kuwasaidia wakulima, wafugaji na wavuvi. Aidha, itaendelea kuchambua tozo zilizobaki ili kupunguza mzigo wa makato kwa wakulima wakiwemo wa zao la kahawa na hatimaye kuwaongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Serikali hatua hii itatoa matokeo yanayotarajiwa na kuwasaidia wakulima wa zao la kahawa kuongeza kipato chao. Hivyo, Serikali haiwashauri wakulima waanze kuhangaika kutafuta soko la kahawa nje ya nchi kiholela kwani kwa kufanya hivyo watajiingiza katika gharama zisizo na lazima na hivyo kupunguza kipato chao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, niishukuru Serikali kwa hizo tozo 17 ambazo wameondoa lakini bado ziko tozo ambazo zimebaki na ukilinganisha huyu mkulima wa kahawa na mazao mengine wameonewa muda mrefu kwa hizi tozo ambazo zimefikia sehemu ya kuwakatisha tamaa wakulima na wengine wameshaanza hata kung'oa ile mikahawa. Swal la kwanza, je, hizi tozo ambazo zimebaki Serikali ina mpango gani wa kuziondoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa bei ya kahawa inategemea soko la dunia, je, Serikali iko tayari kila mwaka kutoa bei elekezi ili kuondoa unyanyasaji na uonevu ambao wanaupata wakulima? *(Makofi)*

**MWE NYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO MIFUNGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi na tozo ambazo zimebaki, naomba nimfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari hata katika bajeti ya Serikali ambayo tunajadili sasa, kuna kodi zingine ambazo zinategemewa kuondolewa ikiwepo kodi ambayo imekuwa ikiwasumbua wakulima kwa muda mrefu ya *Cess* ambayo inategemewa kupunguzwa kwa asilimia tatu. Tunaamini kwamba hii itawasaidia sana wakulima wa kahawa kuweza kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zile zingine zilizobaki kwa sababu kimsingi zilikuwa 28, tunafikiri kama 20 hivi zitakuwa zimeshaondoka, nafikiri kadri muda unavyozidi kwenda tutaendelea kuzipunguza ili mradi tufahamu kwamba kuna baadhi ya tozo ambazo ni muhimu kwa ajili ya kuendesha zao lenyewe ikiwepo kodi zile za Vyama vya Ushirika, lakini tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na bei dira, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kufanyika kazi utaratibu uliopo sasa ambao kawaida kwa kulingana na bei ya dunia bei dira hutolewa. Vilevile ili tuweze kufanikisha suala la bei dira tunahitaji kuratibu vizuri zaidi minada ya kahawa na ndiyo maana tunataka tuhamishe utaratibu wa stakabadhi ghalani kwenda kwenye kahawa vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumefanikiwa sana kwenye korosho, tunataka vilevile sasa utaratibu ule tuhamishe kwenye kahawa. Juzi juzi nilipokuwa Mkoani Kagera nilipata bahati ya kuzungumza na wahusika wa *KDU* na niliahidi kwamba mfumo wa stakabadhi ghalani kwa kahawa utaanzia Kagera. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.



**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa tumbaku wamekuwa wakilipwa bei ya zao la tumbaku kidogo kwa kisingizio cha gharama kuwa kubwa lakini kwa kuwa zipo tozo 10 ambazo zimetolewa na Serikali, je, ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima zile tozo zilizotolewa ziwanufaishe wakulima ili waweze kupata bei nzuri sambamba na kuwatafutia masoko ya uhakika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo la Serikali la kuondoa tozo zile ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wakulima wanapata bei nzuri ya mazao yao. Kwa hiyo, kwenye tumbaku vilevile katika msimu unaokuja ni lazima bei ibadilike iendane na kasi ambayo Serikali imetumia kuondoa tozo ikiwa ni pamoja na kupunguza cess.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hali ya kawaida hatutegemei bei iendelee kubakia wakati sisi tayari tumefanya kazi kubwa ya kuondoa tozo ambazo zilikuwa zinaingiza gharama za uzalishaji lakini vilevile kuleta gharama zingine katika mnyororo mzima wa tumbaku. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa vile hali ya Kyerwa ni sawa na Jimbo la Same Mashariki ambapo zao la tangawizi limekuwa kubwa sana na kwa muda mrefu sasa mwaka wa tano huu kiwanda hakijawahi kufanya kazi. Je, atatusaidiaje kutuwekea angalau bei elekezi ili hawa wakulima wa tangawizi ambapo Same Mashariki ndiyo inaongoza kulima

tangawizi Tanzania wasilaliwe kwa kupewa bei ndogo sana?  
Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba changamoto ya kiwanda ambacho kilisita kufanya kazi sasa inaelekea kutatuliwa kwani *PPF* wamejitokeza kuwekeza katika ukarabati wa kiwanda kile na watakuwa vilevile wanamiliki *shares*. Kwa hiyo, tunaamini kwamba itasaidia kuweka mtaji ambao utafanya kiwanda kiweze kuendeshwa bila kuwa na tatizo lolote.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mhagama kwa Wizara hiyohiyo.

Na. 390

**Ruvuma Kuendelea kuwa Mkoa wa  
Uzalishaji Mazao ya Chakula**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA** aliuliza:-

Ruvuma ni miongoni mwa Mikoa michache nchini inayotegemewa kwa kuzalisha chakula kwa mahitaji ya nchi nzima lakini hivi karibuni kumekuwa na wimbi la mifugo kuhamishiwa katika mkoa huo:-

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa mkoa huo haupotezi sifa ya uzalishaji bora wa mazao ya chakula?

(b) Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kuwa migogoro ya wakulima na wafugaji haijitokezi kufuatia wimbi kubwa la mifugo kuingia katika mkoa huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa Mkoa wa Ruvuma kuendelea kuwa miongoni mwa mikoa inayotegemewa katika uzalishaji wa mazao ya chakula. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi itaendelea kuhakikisha kuwa wakulima wanapatiwa huduma muhimu za kuwezesha uzalishaji kama vile utafiti wa kuongeza tija, ushauri na upatikanaji wa pembejeo stahiki ili kuongeza uzalishaji wa mazao lengwa kwa mahitaji ya wananchi wa Ruvuma na Taifa la Tanzania.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania raia yeyote wa Tanzania anaweza kumiliki na kutumia ardhi mahali popote nchini, kwa kufuata taratibu za kisheria. Fungu la 32(2) la Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 linaweka utaratibu kwa raia wasio wanakijiji kumiliki wa kutumia ardhi ya vijiji kimila. Kwa mujibu wa sheria hiyo, usimamizi wa ardhi za vijiji uko chini ya Mamlaka za Vijiji ambapo zinapewa ushauri na Mamlaka za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji hao watatoa maombi kwa Mamlaka za Mkoa, Wilaya na Vijiji husika na endapo wakikubaliwa watajiunga na vijiji na watatakiwa kufuata kanuni zilizowekwa na vijiji hivyo. Aidha, vijiji vinatakiwa kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi ambayo itatenga ardhi kwa matumizi mbalimbali kama vile makazi, kilimo, misitu, akiba, uwekezaji, ufugaji na kadhalika kadri ya mahitaji ya wanakijiji. Endapo sheria na taratibu zitazingatiwa na pande zote, hakutakuwa na migogoro. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimuulize swali la nyongeza. Kwa vile ndani ya Kijiji cha Ngadinda katika Kata ya Gumbilo kuna shamba la Serikali la hekta 6,000 na tayari mazungumzo yasiyo rasmi na Wizara kwa kupitia Waziri alionesha nia ya kuligawa lile shamba ili sehemu ya shamba lile wapewe wafugaji na sehemu wapewe wakulima. Kwa vile kaya 111 za wananchi wa Kijiji cha Ngadinda wanalima katika Wilaya ya Namtumbo kwa sababu hawana eneo la kuzalisha chakula, ni nini sasa mwongozo wa Serikali katika kuhakikisha kwamba zoezi hili linafanikiwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na maelekezo ya jana aliyotoa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kwamba tunashughulikia migogoro ya ardhi, ikiwa ni pamoja na kutoa ardhi ambazo hazitumiki kwa sasa kwa wakulima na wafugaji, Wizara imekuwa ikifikiria kujadiliana na Halmashauri ya Madaba kuangalia ni namna gani tunaweza tukagawa Shamba la Mifugo la Ngadinda lenye hekta 6,000 ili wakulima wanaoweza kutumia sasa waweze kupata sehemu ya kulima lakini vilevile sehemu iliyobaki iwe kwa ajili ya wafugaji wengi wao wakiwa wametoka kwenye mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba swala hili ambalo amekuwa akifuatilia kwa muda mrefu tutaendelea kujadiliana kuangalia namna gani tunaweza tukalimaliza moja kwa moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Lubeleje.

Na. 391

**Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo ya Mpwapwa Kuhamishiwa Mjini Dodoma**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli wakati akiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika Serikali ya Awamu ya Nne alikataza Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo ya Mpwapwa (*Veterinary Investigation Centre*) ishamishiwe Dodoma Mjini ili wanafunzi wa Chuo cha Mifugo cha Mpwapwa waendelee kupata mafunzo kwa vitendo katika taasisi hiyo lakini taasisi hiyo tayari inahamishiwa Dodoma Mjini:-

Je, ni sababu gani za msingi zimefanya taasisi hiyo ihamishiwe Dodoma Mjini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Ufuatiliaji na Utambuzi wa Magonjwa ya Mifugo (*Veterinary Investigation Centers*) kikiwemo Kituo cha Mpwapwa vilibadilishwa muundo rasmi na Serikali mwaka 2012 kufuatia kuanzishwa kwa Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (*Tanzania Veterinary Laboratory Agency - TVLA*) kwa Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala za Serikali, Sura Na. 245 ya mwaka 1997 iliyofanyiiwa marekebisho mwaka 2009. Mabadiliko haya yalizaa taasisi mbili ambazo ni Kituo cha Ufuatiliaji wa Magonjwa ya Mifugo (*Zonal Veterinary Centre - ZVC*) na *TVLA*. Shughuli za ufuatiliaji wa magonjwa zilibaki *ZVC* na shughuli za utambuzi wa magonjwa zilibaki *TVLA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivi viliamishiwa Mjini Dodoma ili kusogeza huduma hizo karibu na wadau husika

wa sekta ya mifugo wa Mikoa ya Singida na Dodoma ambayo ilikuwa inahudumiwa na Kituo cha V/C kilichokuwa Mpwapwa. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa mwaka 1992, Serikali ilipunguza wafanyakazi wakiwemo wahudumu wote wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa. Kwa hiyo, taasisi ikakosa wahudumu hata wa kukamua na kuchunga mifugo. Kwa kuwa, taasisi aliajiri vibarua 90 ambao hawajalipwa mishahara yao mpaka sasa miaka miwili, wanateseka na familia zao, je, Serikali itapeleka lini fedha ili taasisi hii iweze kuwalipa hawa vibarua 90? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa hapa nchini mifugo mingi inakufa kutokana na ugonjwa wa homa ya kupe (*east coast fever au tick-borne disease*) na kwa kuwa tiba kubwa ya ugonjwa huu ni kuogesha mifugo kwenye majosho. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inachimba majosho ya kutosha Wilayani Mpwapwa pamoja na Wilaya zingine hapa nchini? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu, kuna swali jipya hapo wewe jibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nitambue Mheshimiwa Lubeleje siyo kwamba ni mdau tu wa mifugo lakini vilevile ni Afisa Mifugo Mstaafu kwa hiyo amebobea sana katika hilo eneo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maswali yake mawili, kuhusu kulipwa kwa wafanyakazi ambao anawataja, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu

suala hili alilileta vilevile kwa uzito wakati wa mjadala wa bajeti yetu, tayari tulishatolea maelekezo liweze kufanyiwa kazi katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili kuhusiana na ugonjwa wa *east coast fever* na miundombinu ya kuogesa mifugo, nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa shughuli za uogeshaji wa mifugo zinaendeshwa na Halmashauri. Kwa hiyo, nimshauri kwa sababu naye ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Mpwapwa waweke mikakati ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na majosho ya kutosha katika Wilaya hiyo vilevile Wizara pale itakapoweza inaweza kuangalia namna ya kuwasaidia. Pa siku hizi Serikali inajaribu kuhimiza wafugaji wenyewe waweze kujihamasisha na kutumia mifugo waliyonayo waweze kujipatia huduma za mifugo ikiwepo maji pamoja na majosho.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje, kaa tafadhali.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje tafadhali kaa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka kumbukumbu sawa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje tafadhali kaa. Kanuni zetu haziruhusu haya mambo, *please* kaa.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Afisa Mifugo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje, kaa chini, Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye Mnada wa Pugu kumetokea shida kubwa sana ambayo ningepomba Mheshimiwa Waziri anaisaidie majibu kwamba wale watu ambao wanafanya biashara ya kuuza ng'ombe pale wamepangiwa muda ikifika saa nane mnada unafungwa. Kule Pugu ni mjini hakuna sehemu ya kuweka ng'ombe kwa maana ya kupata majani na maji. Matokeo yake kuna ugomvi mkubwa kati ya watu wenye mifugo yao na wananchi ambao wanazunguka maeneo yale hasa mboga mboga zao kwa akinamama wajane wale. Kwa hiyo, naomba nipate kauli ya Mheshimiwa Waziri kwamba anatoa maelekezo gani juu ya muda wa kuuza ng'ombe kwenye Mnada wa Pugu hivi sasa? Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, swali la msingi ni kuhusu Chuo cha Utafiti, wewe unakuja na minada, kaa chini. *(Kicheko)*

Tunaendelea Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa.

Na. 392

### **Idadi Ndogo ya Wanawake Kumiliki Ardhi**

**MHE. SALMA M. MWASSA** aliuliza:-

Idadi ya wanawake wanaomiliki ardhi ni ndogo sana ikilinganishwa na wanaume:-



Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wanawake wengi zaidi kumiliki ardhi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu wanawake na wanaume wana haki sawa ya kupata na kutumia ardhi. Misingi ya haki hii imewekwa katika Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inatoa haki ya kikatiba ya kumiliki mali kwa kila mtu pasipo kujali jinsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, kifungu cha 4.2.4(i) cha Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, kifungu cha 3(2) cha Sheria ya Ardhi (Sura 113) na Sheria ya Ardhi ya Vijiji (Sura 114) vinaelekeza kuwa haki ya kila mwanamke kupata, kumiliki, kutumia na kufanya miamala inayohusiana na ardhi itakuwa sawa na haki ya mwanaume kwa kiwango na masharti yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa matamko ya kikatiba na kisheria yanayolinda haki ya wanawake kumiliki ardhi, bado kuna changamoto hususan katika maeneo ya vijiji ambako wanawake wengi wananyimwa haki ya kumiliki ardhi kutokana na mila, desturi na kaida (*norms*) za baadhi ya makabila zinazowabagua wanawake kwa kugawa ardhi kwa viongozi wa familia ambao kwa kawaida ni wanaume na kuwanyima wanawake haki ya kurithi mali ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kuondoa tamaduni, mila na desturi za kibaguzi katika kumiliki ardhi kwa kutumia sheria hazijafanikiwa kutokana na kushindwa katika utekelezaji kutokana na mfumo dume na uelewa

mdogo wa umma kuhusu sera na sheria zilizopo. Katika kukabiliiana na changamoto hii, Wizara yangu imefanya juhudi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya maboresho katika Sera ya Taifa ya Ardhi ambayo kwa kiasi kikubwa imeweza kuwashirikisha wanawake ili wafahamu haki yao ya kupata ardhi bila kikwazo vinavyotokana na mila, desturi, kaida na tamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa elimu kwa wananchi ili waendeleo kufahamu namna Sera na Sheria za Ardhi zinavyoelekeza kuhusiana na suala zima la umiliki wa ardhi baina ya wanaume na wanawake. Hivyo, wanawake kote nchini wanahimizwa kujitokeza kuomba milki za ardhi kulingana na mahitaji yao kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwassa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nishukuru kidogo kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini siyo kwamba wanawake hawana elimu ya haki yao ya msingi ya kumiliki ardhi, lakini tatizo kubwa pamoja na matamko ya kikatiba na kisheria, haki yao hii ya msingi wanawake ya kumiliki ardhi inanyang'anywa na mila, desturi na taratibu za mifumo dume katika makabila yao au makabila ya Tanzania yaliyo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Serikali ni kwa nini sasa tusilite sheria hapa Bungeni au kuweka sera maalum inayosema kwamba kwa uwiano maalum wanawake wamiliki kiasi gani na wanaume wamiliki kiasi gani ili kuleta usawa wa kisheria wa kumiliki ardhi kama ilivyo kwenye...

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa Mwassa, muda wetu umekwisha.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Kama ilivyo kwenye Viti Maalum hapa Bungeni, kuna sera kama hizo za kuweka uwiano. Je, Serikali inasema nini

kuhusu kuleta sera maalum au hiyo kanuni hapa Bungeni ili tuweze kupata hiyo haki yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ya urasimishaji na upimaji, ni kwa nini sasa isiwekwe uwiano maalum kwamba kama ni viwanja labda 1,000 basi 200 *specific* vimilikishwe kwa wanawake? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali lake la kwanza, kulingana na matamko yanavyosema kwamba kwa nini kusiwe na sera maalum ambayo inawezesha wanawake hawa kuweza kumiliki ardhi. Ukiangalia kwenye Sera ya Ardhi kwenye yale matamko yake, kifungu namba 4.2.6(i), inataja wazi kwamba pale ambapo mila na desturi zinakwenda kinyume na Katiba ya nchi, Katiba ya nchi ndiyo inachukua nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kwenye matamko tayari imeshataja kwamba umiliki uko sawa kwa wanaume na wanawake lakini pale ambapo unakuta kuna mila na desturi mbovu zinazomkandamiza mwanamke basi ile sheria ya nchi kwa maana ya Katiba inachukua nafasi yake kwa hiyo bado uwiano uko palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la kusema kwa nini tunapopima viwanja kusiwe na uwiano. Inakuwa siyo rahisi kuweka uwiano wa namna hiyo kwa sababu inategemea na uombaji, ni nani kaomba, lakini pia inategemea katika yale maeneo ni akina nani kuomba kupewa umiliki wa vile viwanja. Kwa hiyo, ukisema unatenga kwa wanawake wakati huohuo inategemeana na makubaliano ya ndani ya familia, kama wanaomba kama familia watachukua kama familia, kama akiomba *individual* kama mwanamke bado anayo nafasi ya kupewa lakini inaweza kuwa sio rahisi sana kwamba useme utenge maeneo maalum kwa ajili ya wanawake lakini tutaendelea kutoa

elimu ili wajue kwamba wanayo haki sawa ya kumiliki ardhi kama wanaume.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ikupa, ajiandae Mheshimiwa Flatei.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa baadhi ya mila na desturi zetu zimekuwa kikwazo kikubwa cha wanawake kumilikisha ardhi hasa kwenye ngazi ya familia linapokuja suala la mirathi. Je, Serikali haioni sasa kwamba ni muhimu kukaa na hawa viongozi wetu wa jadi na kuwaelimisha kwa sababu wao ndiyo viongozi wakuu ambao wanaweza wakalegeza hizi mila na desturi? Mimi swali langu ni hilo, kwamba kwa nini sasa Serikali isikae na hawa viongozi wa jadi ambao ndiyo viongozi wakuu ambao wanasimamia hizi mila na desturi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo lake alilolitoa ni jema na ndiyo maana wakati tunapitia upya Sera ya Ardhi ambayo ilikuwa iko kwenye mchakato karibu itatoka, makundi yote yamehusishwa na kutaka kujua pale ambapo kuna maeneo ambayo pengine mwananchi wa kawaida na hasa mwanamke pengine hatendewi haki wananchi wametoa mawazo yao namna bora ya kuweza kugawa ile ardhi kwa kutegemeana na sheria ya nchi ilivyo. Kwa hiyo, kwenye sera hii itakayokuja kutoka, makundi yamehusishwa na pale ambapo palikuwa na changamoto imezungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado fursa ipo kama pengine inaonekana kuna umuhimu wa kuwa na mazungumzo tofauti na hapo. Hata ukienda katika ugawaji wa ardhi katika maeneo, pale ambapo unakuta mwanamke amedhulumiwa bado kuna ile fursa ya kuweza kukaa na watu wa kimila na kuweza kuliona kwa utaratibu mzuri wa kupitia vikao na siyo kukiuka mila ambazo zipo, lakini zile ambazo hazikiniani na Katiba ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei .

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, inaonekana Mfumo Dume ndiyo unaleta tatizo, lakini amezungumzia Sera ya Ardhi ni lini analeta Bungeni ili wanawake wapate haki yao? Anitajie lini analeta Bungeni. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, lini? Mwambie tu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisitamke *specific* kwamba ni lini lakini imeshafikia kwenye hatua za mwisho, ile *draft* ya mwisho tayari imeshakamilika maana yake tunasubiri itoke *final version* ambayo tutaita hapa. Kwa hiyo, ni lini, nadhani ndani ya kipindi kifupi tutaita.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Vulu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na juhudi za Serikali na asasi mbalimbali...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vulu, subiri kidogo. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongeze jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu Sera haziji Bungeni, sheria ndiyo zinakuja Bungeni. Waheshimiwa Wabunge mwanzoni kabisa wakati wa bajeti ya mwaka jana tuliwapa *questionnaire* na tukawaomba kila mmoja kama mdau atoe maoni yake. Hayo maoni yenu wale wanaokumbuka mliyatoa na wananchi wengine ndiyo tunatengeneza sera kwa utaratibu wa Serikali lakini hatutaahidi hapa kwamba itakuja lini kwa sababu haitakuja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vulu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na juhudi za Serikali na asasi mbalimbali za kuhakikisha wanawake wanapata maeneo na lengo la kupata maeneo ya ardhi ni kujenga ama kulima, Serikali haioni kwamba wale wanawake wa vijijini waliokuwa na uwezo mdogo wamepata ardhi, wakajenga nyumba lakini wameweka kodi ya majengo au ya ardhi ambayo wanaweza wakashindwa kulipa. Je, kuna mkakati gani wa kuweza kuwasaidia ili wapunguze au wasilipe kabisa kwa wale ambao wako vijijini kwa ajili ya kuweza kujitendeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipita unaweza ukaona hata hizo nyumba zenyewe haziko imara, ni nyumba hafifu sana kutokana na kwamba hawana pesa za kutosha. Naomba mkakati wa Serikali kuwahurumia wanawake walioko vijijini au wale ambao hawana uwezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimkumbushe tu Mheshimiwa kama amesikiliza vizuri wakati Waziri wa Fedha na Mipango anawasilisha bajeti yake, aliongea kwa kina zaidi kuona ni majengo gani na ya aina ipi yanayotozwa kodi za majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hilo analozungumza la vijijini sidhani kama kuna kodi ya majengo katika vijiji ambavyo anavisemea kwa maana ya vijiji. Kuna maeneo yaliyoainishwa katika utaratibu ule ambao Waziri wa Fedha na Mipango aliutoa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Mpakate.

Na. 393

## Madini ya Vito – Wilayani Tunduru

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Wilaya ya Tunduru ni mojawapo ya Wilaya zenye utajiri wa madini ya vito na leseni za kununulia madini zipatazo 21 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya kununua madini hayo:-

Je, ni kwa nini Serikali haioni haja ya kuweka Ofisi ya TMAA ili kufanya tathmini ya thamani ya madini yanayonunuliwa na wanunuzi hao badala ya kufanyia Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wilaya ya Tunduru imebarikiwa kuwa na madini ya vito ya aina mbalimbali kama vile *sapphire*, *alexandrite*, *spinel* pamoja na *emerald*. Wachimbaji wadogo huuza madini yao kwa wafanyabiashara wadogo (*brokers*) lakini pia kwa wafanyabiashara wakubwa wanaoitwa *dealers*. Kwa sasa Tunduru kuna wafanyabiashara wadogo wapatao 15 na wakubwa 22 lakini kutokana na uzalishaji kupungua maduka matano ya wafanyabiashara wakubwa yamefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthamini wa madini ya vito hufanywa kupitia Kitengo cha Uthamini wa Madini ya Almasi na Vito (*TANSORT*). TMAA ni Wakala wa Ukaguzi wa Madini na wana majukumu ya kufanya ukaguzi wa uzalishaji, mazingira na biashara ya madini hapa nchini. Ofisi za TMAA zipo katika kanda zote ikiwemo Songea inayosimamia Ofisi ya Madini ya Tunduru. Jukumu la TMAA ni kuhakikisha kwamba mapato stahiki ya Serikali yatokanayo na madini yanapatikana hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Swali la kwanza, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru haijawahi kupata *service levy* kutoka kwenye makampuni haya aliyoyataja kwa maana ya *dealers* na *brokers* kutokana na mauzo yao ya madini ambayo wanayatoa kutoka Tunduru. Je, ni lini *TANSORT* na *TMAA* watapeleka taarifa za manunuzi na usafirishaji wa madini kutoka Tunduru kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili iweze kupata *service levy*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Halmashauri hii ya Wilaya ya Tunduru ina leseni takribani 800 za wachimbaji wadogo wa *copper* katika Kijiji cha Mbasa, je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo waliopo pale ili waweze kufanya kazi zao vizuri? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mpakate kwa sababu katika juhudi zake na Wabunge wengine wa Songea, pamoja na Wabunge wanaotoka katika maeneo ya madini wamehangaika sana kushughulikia madai na maslahi ya wachimbaji wadogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza, niseme tu kwamba tangu mwezi uliopita wachimbaji wote wa madini sasa wametakiwa kuwasilisha taarifa zao kupitia ofisi zetu za Kanda. Kwa hiyo, kuanzia mwezi uliopita Ofisi za Kanda pamoja na za Mikoa zinawasilisha sasa taarifa za uzalishaji wa madini katika maeneo yale kwenye Halmashauri. Nitoe rai sasa kila Mkurugenzi kuhakikisha kwamba anadai ile *service levy* ya *0.3 percent* ya kila mchimbaji wa madini popote anapochimba, hii ni kwa wachimbaji wakubwa pamoja na wadogo, kwa hiyo nawashukuru sana Wabunge kwa hili.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madini ya shaba, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mpakate lakini sio leseni 800, leseni tulizotoa Tunduru pamoja na Songea ni 1,620, ni nyingi sana. Niseme ni hatua gani Serikali inachukua, cha kwanza, inatoa elimu kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, cha pili tunawafundisha wachimbaji ili waweze kuwa na uchimbaji salama unaozingatia pia utunzaji wa mazingira na la tatu tunawapa ruzuku. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpakate, nitoe nafasi hii wachimbaji wako sasa wanaweza kuja kwenye ofisi zetu ili waendeleo kupata msaada zaidi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumetumia dakika kumi za kuchangia bajeti na muda wetu umeshapita na kama mnavyofahamu maswali ni saa moja tu.

Tangazo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo. Kikao kitafanyika katika Ukumbi wa Zahanati ya Bunge mpya.

Waheshimiwa Wabunge, mnaarifiwa kuwa Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Chama cha Kuhudumia Wenye Ulemavu wa Usikivu Tanzania, wameandaa zoezi la uchunguzi wa afya ya sikio kwa Waheshimiwa Wabunge. Zoezi hili linafanyika kwa muda wa siku tatu tokea tarehe 14 hadi tarehe 16 na linafanyika kwenye Kituo cha Afya cha Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kutumia fursa hii kuweza kufanya uchunguzi na kupata ufafanuzi zaidi kuhusu afya ya sikio na ni muhimu sana mwende kwa sababu wengi hamtusikii Kiti hapa. *(Kicheko)*

Tangazo la wageni, wageni 70 wa Mheshimiwa Edwin Sannda ambao ni wanafunzi 67 na Walimu watatu kutoka Shule ya Sekondari Mtobubu iliyopo Wilaya ya Kondoa, Mkoani Dodoma. Karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Hassan Kaunje ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango kutoka Mkoani Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Pia tuna wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambao wamekuja kutembelea Bunge. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### **MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuweka, Kutoza na Kubadili baadhi ya Kodi, Tozo, Ada na Ushuru na Kufanya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Zinazohusu Ukusanyaji na Usimamizi wa Mapato ya Umma *(A Bill for an Act to Impose and Alter Certain Taxes, Duties, Levies and Fees and to Amend Certain Written Laws Relating to Collection and Management of the Public Revenues)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

### **AZIMIO LA BUNGE**

**Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua anazochukua kukabiliana na Upotevu wa Mapato ya Serikali katika Sekta ya Madini**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita msoma Azimio, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu, Mheshimiwa Mkuchika. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Bunge kumpongeza Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hata anazochukua kukabiliana na upotevu wa mapato ya Serikali katika sekta ya madini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya utangulizi. Kwa nyakati tofauti, Waheshimiwa Wabunge, wananchi na asasi mbalimbali za kiraia kutoka katika maeneo mbalimbali nchini wamekuwa wakilalamika na kuonesha kutoridhishwa kwao na mchango wa sekta ya madini katika maendeleo ya Taifa na usimamizi wa Serikali katika sekta hiyo. Aidha, yapo malalamiko kuwa Taifa letu halinufaiki ipasavyo na sekta hii kwa sababu mikataba iliyopo haitoi fursa kwa Serikali kupata gawio la kutosha, kupata kodi na mapato mengine mbalimbali yanayotokana na shughuli za uchimbaji wa madini zinazofanywa na makampuni yaliyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli ilipoingia madarakani, hatua mbalimbali zimechukuliwa kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali na kuziba mianya ya upotevu wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Madini, hivi karibuni Mheshimiwa Rais aliunda Kamati mbili zilizofanya uchunguzi kuhusu usafirishaji wa makinikia ambapo Kamati ya Profesa Abdulkarim Hamisi Mruma ilichunguza kiwango na aina ya madini yaliyomo kwenye makinikia yanayosafirishwa nje ya nchi na Kamati ya Profesa Nehemiah Eliakim Osoro ilifanya tathmini ya hasara ama faida inayopatikana kwa kipindi chote tangu usafirishaji wa makinikia ulipoanza mwaka 1998 pamoja na kushauri hatua zinazoweza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 24 Mei, Mheshimiwa Rais alipokea Taarifa ya Kamati ya Profesa Abdulkarim Hamis Mruma na mapendekezo yake ya kuchukua hatua za kuwawajibisha wale wote waliohusika kwa namna moja au

nyingine na dosari zilizobainika. Aidha, tarehe 12 Juni, 2017, Mheshimiwa Rais alipokea Taarifa ya Kamati ya Profesa Nehemiah Eliakim Osoro na kuzielekeza taasisi zote zinazohusika kila mmoja kwa nafasi yake kuyafanyia kazi mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua uzalendo aliouonesha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli, juhudi na uthubutu wake katika kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kwamba Watanzania na Taifa kwa ujumla wananufaika ipasavyo na rasilimali za madini ambazo zinaweza kutoa mchango katika uanzishaji wa viwanda, ustawi wa maendeleo ya jamii, huduma za jamii, miundombinu na hali bora ya maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilikuwa ndiyo ndoto ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye kwa miaka mingi alikuwa anatamani Tanzania inufaike na rasilimali za madini zilizopo nchini. Hivyo, naomba kutumia fursa hii kuliomba Bunge hili Tukufu ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi kuridhia Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nawasilisha Azimio la Bunge lenyewe la kumpongeza Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua anazochukua katika kukabiliana na upotevu wa mapato ya Serikali katika Sekta ya Madini nchini. Hii inatolewa chini ya Kanuni ya 54 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. *(Makofi)*

KWA KUWA kwa nyakati tofauti, Waheshimiwa Wabunge, wananchi na asasi mbalimbali za kiraia kutoka katika maeneo tofauti nchini wamekuwa wakilalamika na kuonesha kutoridhishwa kwao na mchango wa sekta ya madini katika kuliletea Taifa maendeleo;

NA KWA KUWA kumekuwepo na malalamiko kuwa Taifa halinufaiki ipasavyo na sekta ya madini kutokana na mikataba ya madini iliyopo kushindwa kutoa fursa kwa Serikali kupata gawio la kutosha, kwa Serikali kupata kodi na mapato mengine mbalimbali yanayotokana na shughuli za uchimbaji wa madini zinazofanywa na makampuni mbalimbali hapa nchini;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonesha juhudi, uthubutu na uzalendo wa hali ya juu kwa kufungua njia itakayoweza Taifa na wananchi wote kwa ujumla kunufaika ipasavyo na rasilimali za nchi; *(Makofi)*

NA KWA KUWA Wabunge na Watanzania wote ni mashahidi wa matokeo ya uchunguzi wa Kamati ya Profesa Abdulkarim Hamisi Mruma na Kamati ya Profesa Nehemiah Eliachim Osoro zilizoundwa na Mheshimiwa Rais na kutoa taarifa kwake tarehe 24 Mei, 2017 na tarehe 12 Juni, 2017 ambapo Mheshimiwa Rais alikubali mapendekezo ya Kamati zote mbili kisha akachukua hatua za kuwawajibisha wote waliohusika kwa namna moja au nyingine na dosari zilizobainishwa na Kamati ya Profesa Mruma na kwa upande wa Kamati ya Profesa Osoro akazielekeza taasisi za Serikali zinazohusika kuchukua hatua;

KWA HIYO BASI, Bunge hili katika Mkutano wake wa Saba, Kikao cha Arobaini na Saba, leo tarehe 14 Juni, 2017 linaazimia kwa kauli moja kama ifuatavyo:-

(1) Kumpongeza Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi, uthubutu, uzalendo wa hali ya juu wa kufungua njia itakayoweza Taifa na wananchi kwa ujumla kufaidika ipasavyo na rasilimali za nchi. *(Makofi)*

(2) Kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba Bunge hili la Kumi na Moja linaloongozwa na Mbunge wa Kongwa, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, liko pamoja naye na liko

tayari kutoa ushirikiano wa dhati kwa kadri itakavyohitajika katika kuhakikisha kwamba juhudi, uthubutu na uzalendo aliouonyesha haupotei bure bali unakuwa chachu ya kuhakikisha kuwa sekta ya madini inachangia katika kuleta maendeleo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

(3) Kushauri kwamba hatua kali zichukuliwe kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa wote ambao kwa namna moja au nyingine watathibitika kuwa wamehusika katika kulingizia Taifa hasara na kuwakosesha Watanzania fursa ya kufaidika na rasilimali za madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono na Bunge zima.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaa.

**MWENYEKITI:** Ahsateni. Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wetu sasa tunaingia kwenye mjadala wa Azimio hili na tayari nina majina ya wahusika wa vyama vyote. Nitaanza na Mheshimiwa Omar King, dakika ni tatu tatu. *(Makofi)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii. Kwa kuwa Azimio limejikita katika kumpongeza Mheshimiwa Rais kutokana na tukio ambalo limetokea na sote tunampongeza kama ilivyofanya hotuba ya Mwenyekiti hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM miaka yote tokea mwaka 1992 ni chama kipevu sana tokea huko nyuma kwa hiyo kilijiwekea miongozo ya kwamba kujikosoa leo kuliko

jana na CCM imepanga lazima rasilimali za nchi ziwafaidishe wananchi. Katika kufikia lengo hilo ndiyo maana tukaona kwamba Marais wetu ambao wamepita wote walikuwa wana ripoti zao, Mheshimiwa Mkapa alikuwa ana ripoti, Mheshimiwa Mwinyi alikuwa ana ripoti, Mheshimiwa Dokta Kikwete alikuwa ana ripoti kuhusiana na suala hili la kufaidika na rasilimali za nchi. Hata hivyo, isitoshe tunafanya hivyo kwa lengo la kwamba ni lazima kuweka uwiano mzuri kati ya maslahi ya Taifa kwa wananchi wote pamoja na kuwavutia wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pongezi zangu kwamba Rais Magufuli amejipambanua kutokana na wengine wote ingawaje kwamba wametokezea watu sasa wanajipaka damu za simba kama wao ndiyo walioua simba lakini simba tayari ameshauliwa sasa wanajitokeza. Hoja hii hata kama kuzungumzwa ilikuwa ikizungumzwa mpaka kwenye vibaraza vya kahawa kwamba vipi watu watafaidika na mchanga au na madini ambayo yapo katika nchi kwa hiyo siyo kwamba ni suala la fulani na fulani. Mimi naeleza hili kwamba Rais Dokta John Pombe Magufuli ni kiumbe na roho yake hawa wengine wote wanaojipapakapa ni midoli tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika Azimio hili tuiombe Serikali kwa upande wake iweze kupitia mikataba na kubaini mianya yote na kuiziba ili rasilimali za Taifa zisaidie Taifa. Pia kwa upande wa Bunge kama ilivyopendekezwa kwamba Serikali italeti marekebicho ya sheria, kwa hiyo, yatakapoletwa marekebicho ya sheria tuweze kuziba mianya yote, sisi ni Watanzania tuzilinde rasilimali zetu. Pamoja na hayo Waziri naye atengeneze taratibu kwa sababu madini haya yanatoka sehemu tofauti tofauti, kwa hiyo, hizo taratibu atakazoiweka ziwe sambamba na maeneo ambayo madini yetu haya yanatoka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsahte. Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 25 Aprili, 2017 nilisimama mbele ya Bunge

lako hili Tukufu na nikasema kwamba nchi hii imepata Rais mzalendo namba moja. Niliposimama nililiomba Bunge lako Tukufu kufuta neno uzalendo katika Kamusi ya Kiswahili iwapo siku moja Wabunge walio wengi watasema kwamba mambo yanayofanywa na Dokta Pombe Magufuli siyo uzalendo katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokifanya Dokta John Pombe Magufuli ni utekelezaji wa Kanuni ya 10 ya Uongozi (*The Law of Connection*) ambayo inasema kwamba, *leaders touch the heart before they ask for the hand*. Mambo haya yaliyofanywa hivi punde ni ya kizalendo na yamemgusa kila Mtanzania katika moyo wake, wale walio katika Vyama vya Upinzani lakini pia hata wale ambao tupo katika Chama Tawala hapa nchini na nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ni uwepo wa mikataba mibovu na nakumbuka wakati nasoma historia nilimsoma Carl Peters mwaka 1884 ambaye aliingia Afrika na kuwasainisha Mababu zetu mikataba ya hovyoka kabisa. Leo hii tunajionea uwepo wa mikataba mibovu kabisa hapa nchi ambayo Rais wetu Dokta John Pombe Magufuli amedhamiria sasa kwa kupitia Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015-2025, ukisoma vyema ukurasa wa 28 na 29 wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, inazungumzia kuhusu usimamiaji wa madini yetu na kuhakikisha kwamba madini haya yanawanufaisha Watanzania walio wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio letu hili ambalo limetolewa siku ya leo lakini pia niombe tu Serikali kufuata maelekezo yaliyowahi kutolewa na Keith Jefferis ambaye aliwahi kuwa *Deputy Governor* kule Botswana ambaye aliwahi kusema kwamba, *the paradox of plenty* inatokana na kwamba nchi nyingi zenye utajiri wa madini zimekuwa na umaskini wa hali ya juu. Sasa tuombe yale maelekezo yaliyotolewa na Keith Jefferis tuweze kuyafuata katika nchi yetu hii ili sasa madini haya yaweze kuwakomboa Watanzania walio wengi.



Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi aliyowahi kuyazungumza Keith Jefferis ni uwepo wa *open and transparent* katika *mineral licensing* pamoja na *taxation regime*. Tuombe uwazi uwepo katika mikataba hii ambayo tayari Rais amekubali kuileta kwenye Bunge hili, uwazi huu utaweza kuisadia nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa sisi Watanzania hususani Jimbo langu la Rufiji wanaamini kabisa kwamba mambo haya yakitekelezwa vyema barabara zetu za kutoa Nyamwage - Utete zitajengwa kwa kiwango cha lami, mambo haya yakitekelezwa vyema basi hata leo hii tusingekuwa na deni la Taifa. Naamini kabisa mambo anayofanya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi ya kuchangia Azimio hili japo kwa uchache kwa hizi dakika chache ambazo umetugawia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napatwa na mshituko mkubwa kuona ni kwa nini tunaanza kupongezana mwanzo wa safari, tumezoea kupongezana pale kazi inapokamilika. Kuundwa kwa Tume hakujaanza leo, hakujaanza jana, nikiwa niko mwanafunzi sekondari miaka ya 1997-1998 tulikuwa tunaona Mheshimiwa Benjamin Mkapu aliunda Tume zikafanya kazi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliunda Tume zikafanya kazi, hawa wote tungeanza kuwapongeza pale tu walipounda Tume mwanzoni kabla ya kazi kukamilika tungekuwa tuko wapi? Lazima tuache kazi ifanyike, madini bado yanaibiwa kwa kiasi kikubwa migodini leo tukianza kupongeza kuzuia makinikia peke yake tunakuwa tunakosea. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maisha kuna vitu viwili vya kuchangua ama uchague kuwa mtendaji au uchague kuwa mshangiliaji. Bunge tunaamua kuwa washangiliaji, hili ni jambo la kusikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliamua kubeza hoja nzito zinazohusu kuyalinda madini yetu wakati muafaka, akina Peter Serukamba hawa walipiga kelele hapa, Hamisi Kigwangalla huyu alikamatwa na kuteswa huko kwa sababu ya madini, John Mnyika, Tundu Lissu, Zitto Kabwe walizungumza mambo haya na tuliamua kuwabeza. Leo kwa sababu imepigwa ngoma na tunayempenda tumeamua kuishangilia, tunaishingilia kwa sauti nzito nzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitendee haki Bunge hili, tunapoiingia hapa Bungeni tuvae viatu vya Kibunge tuenee ili tuishauri Serikali na tusijigeuze kuwa washangiliaji tu wa Serikali. Inasikitisha sana, tukilichukulia jambo hili rahisi rahisi kama vile limekwisha na kilichofanyika ndiyo kinatoshwa tunapoteza rasilimali za nchi hii. Kama Bunge tukae na tuone kwamba kama Rais ana nia nzuri kiasi hiki na sisi Bunge tumsaidie kwa ku-*pressurize* sheria zote za mikataba tuzifanyie *amendments* hapa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapande ya dhahabu bado yanaendelea kuondoka na kwa sababu tayari hizi *indicator* za kuzuia zimeanza, tukichukua muda mrefu kabla hatujayazuia haya, watu wataongeza *speed* ya kuziiba kwa sababu wanajua mwisho wao unakaribia. Tuongeze nguvu ya kuzuia rasilimali zetu ziache kuibiwa, kupongezana ni jambo dogo sana, tunaweza kupongezana wakati wowote na wala siyo lazima tukapongezana kwenye Bunge, tunaweza kupongezana kwenye mabaraza ya kahawa, tunaweza kupongezana... *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupata hii nafasi na nalipongeza Bunge kwa kuja na hili Azimio ambalo ni muhimu sana katika kumpongeza Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenye macho haambiwi tazama na mwenye masikio lazima asikie. Rais amechukua hatua nyingi, Rais amethubutu kuzuia makinikia yasiende nje, Rais amezuia kusafirisha madini yote nje, hizo ni hatua za dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu hii ni tajiri sana, tuna madini mengi sana labda nizungumzie kwenye Jimbo langu la Vwawa na Mkoa wa Songwe na Mbeya kuna madini mengi. Kwa mfano, kuna *niobium* pale kwenye Gereza la Songwe ni madini yanayoweza kutumika kutengeneza injini za ndege, ni madini pekee yamegunduliwa yapo Tanzania. Kuna gesi na kila aina ya madini, tuna makaa ya mawe kule Magamba ambayo hayapo yoyote katika Afrika ni makaa bora, tuna makaa ya mawe kule Kiwira, tuna madini ya dhahabu kule Chunya...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Rudi kwenye hoja.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Kuna ugunduzi wa kila aina ya madini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga hebu subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge, sidhani kama ni sahihi wakati tunachangia mijadala muhimu kama hii, upande mmoja uponde upande mwingine bila sababu. Sisi ni watu ambao tuna hoja muhimu mbele yetu, sasa Mbunge wa huku akichangia huku mnaanza kuponda lakini huku wanavumilia sababu wanatumia kanuni za kistaarabu za kusikiliza mijadala ya Kibunge. Sasa naomba, tumtendee haki kila mchangiaji humu ndani.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** *(Aliongea nje ya kipaza sauti)*

**MWENYEKITI:** Gekul kaa kimya.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo natoa *warning* ya mwisho, Mheshimiwa Hasunga endelea na Makatibu muda wake mpeni. *(Makofi)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hawa wenzetu hawasomi vizuri ...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Kwa sababu Botswana mwaka 2006 ilichukua hatua kama hizo na haikushtakiwa. Utajiri ni wa kwetu, madini ni ya kwetu lazima hatua zichukuliwe. Marais waliotangulia walithubutu kuchukua hatua lakini wale wasaidizi wao hawakuwaunga mkono na ndiyo maana sisi tunasema Marais walifanya kazi nzuri lakini watendaji wasaidizi hawakutekeleza majukumu yao, lazima hawa hatua zichukuliwe. Marais walifanya kazi nzuri na Rais huyu wa Awamu ya Tano hatua anazozichukua lazima ziungwe mkono na kila mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru nimeona baadhi ya Wapinzani wanasema ile Miswada mibovu mibovu ambayo ina matatizo iletwe, ni kweli ndiyo tunachosema zile sheria zote mbovu mbovu, mikataba ya kila namna ambayo ina matatizo iletwe hapa Bungeni, tuiptie upya kwa uwazi ili iweze kuleta maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili ni suala la msingi sana ili nchi yetu iweze kunufaika na rasilimali za madini ambazo ni nyingi sana katika nchi hii. Nchi haistahili kuwa maskini kwa utajiri uliopo ambao tumepewa na Mwenyezi Mungu. Tuna almasi, dhahabu, *nikel*, *uranium* na kila aina ya madini, kwa nini tuwe maskini? Lazima tukae chini kama watu tuliokwenda shule tuone ni nini cha kufanya ili nchi yetu iweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais na naomba Wabunge wote tumuunge mkono, tupambane ili nchi hii iweze kuleta maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane kuunga mkono Azimio hili la kumpongeza Rais John Pombe Magufuli. Watanzania tulimwomba Mungu atulettee Rais ambaye ni jasiri, Rais ambaye ana uthubutu, Rais ambaye atakuwa mlinzi wa rasilimali za nchi yetu na Mungu akasikia kilio chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya watu ambao wanasimamia kauli zao ni Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Mheshimiwa John Pombe Magufuli kabla hata hajawa Rais wa nchi hii, alitoa kauli kwamba atakapokuwa Rais atahakikisha mchanga wa dhahabu hautasafirishwa tena kwenda nchi za nje. Mheshimiwa Magufuli kabla hajawa Rais alisema, ole wao Watanzania watalimia meno endapo atakuwa Rais wa nchi hii. Leo tunashuhudia Watanzania aliwalenga kulimia meno ni mafisadi wanaoiba rasilimali za nchi hii na sasa wanaanza kulimia meno. Namwomba Rais wetu hata wale wanaoshabikia na kuunga mkono mafisadi na wenyewe awaweke katika kulimia meno kwa sababu na wao wanashabikia kuibiwa rasilimali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi zote duniani huwezi ukampata mtu wa aina ya Magufuli ambaye amezaliwa kila wakati, ambaye anazaliwa kila mahali na ndiyo maana hata nchi zingine wanaanza kumlilia kwamba huenda na sisi tungekuwa na mtu kama huyu mtu ambaye ana uchungu na watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu wakati anapokea Ripoti ya Makinikia alitaka kulia, nilimwona ameshika shavu

la kushoto, anasema kama na yeye ana damu Rais wetu analia na rasilimali za Watanzania. Leo kuna watu hawataki tumpongeze Rais wetu wakati amejitoa mhanga, kuna watu wanajitoa mhanga kulipua ndege, kuna watu wanajitoa mhanga kulipua hata Mabunge leo Rais anajitoa mhanga kufa kwa ajili ya rasilimali za Watanzania kwa nini tusimuunge mkono mtu kama huyu? Ndiyo maana ukisoma Isaya 54:17 unasema, kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa... (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Ameen.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Na ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu hauta... (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Wajibu wa Kikatiba wa Bunge hili ni kuisimamia na kuishauri Serikali, wajibu wa Bunge siyo kuishangilia au kuimba mapambio kwa Serikali. (Makofi)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizomea)*

**MWENYEKITI:** Order, Order Waheshimiwa

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Kazi ya Upinzani siyo kupinga kila kitu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizomea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa upande huu.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo wastaarabu hao, ndiyo wataarabu hao.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo ustaarabu huo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Subirini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna hoja muhimu kwenye Bunge letu leo.

**MBUNGE FULANI:** Waambie hao.

**MWENYEKITI:** Nimetoa *warning* ya kwanza na nikitoa *warning* natoa kwa Bunge zima.

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**MWENYEKITI:** Sasa nyie mnakataa nini, nimesimama hapa kwa sababu ya nini, mnataka mkafuturu saa hizi. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, natoa agizo tena, mchangiaji yeyote atakayechangia, aachiwe achange kwa namna kanuni zetu zinavyoelekeza. Asizomewe wala asisemwe. Hii natoa *warning*, nitamtoa mtu yeyote, mmenielewa.

**MBUNGE FULANI:** Waambie hao.

**MWENYEKITI:** Msitake kuharibu kazi ya Bunge na msitake kuharibu Azimio. Inawezekana wengine upande huu mmetumwa kuharibu Azimio.

**MBUNGE FULANI:** Kveli.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, natoa onyo tena huku. *(Makofi/Kicheko)*

Makatibu mpeni Mheshimiwa Lissu muda wake.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema wajibu wa Kikatiba wa Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali siyo kuisifia na kuiambia mapambio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Azimio siyo Azimio la Bunge ni Azimio la wana CCM kumpongeza Mwenyekiti wao wa CCM. Kama sisi siyo wanafiki, kama Wabunge wa Bunge hili siyo wanafiki, basi kwa vile mnataka tumsifu Magufuli kwa kuunda Kamati, tuanze na Rais Benjamin Mkapa aliyenda Kamati ya Jenerali Mboma, aliyenda Kamati ya Dkt. Kipokola, aliyenda Kamati ya Dkt. Bukuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi siyo wanafiki, twende kwa Kikwete aliyenda Kamati ya Lau Masha, akaunda Kamati ya Mark Bomani, kama sisi sio wanafiki lakini kwa sababu ni wanafiki hatuko tayari hata kusema kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu kaa. Mheshimiwa Lissu nakuomba, sidhani kama ni jambo muhimu kuchangia na kutupia maneno Wabunge na Kanuni zetu zinakataza. Unatumia lugha ya kuudhi lakini vilevile unatumia lugha ya kuwatuhumu Wabunge wenzio ambayo siyo sahihi kwa mujibu wa Kanuni zetu. Changia tu mjadala wako, huna haja ya kuwaambia watu wanafiki, huna haja ya kuwatukana watu, sababu Kanuni zetu haziruhusu. Jielekeze kwenye Kanuni na wewe ni Mwanasheria mzuri tu, sheria hizi zimetungwa na Bunge letu na wewe ukiwemo.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza, huyo tunayeambiwa amethubutu, mikataba yote ya madini anayoita ya wizi bado ipo, hakuna uliobadilishwa hata mmoja. Hivi tunavyozungumza, sheria zote ambazo zimetungwa miaka yote hii ambazo zimetuleta



hapa tulipo, hakuna iliyoguswa hata moja. Hivi tunavyozungumza asilimia 100 ya madini ya dhahabu yanayochimbwa Geita yanasafirishwa kutokea Geita. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mlinga kaa chini.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza asilimia 100 ya dhahabu inayochimbwa North Mara Tarime inasafirishwa nje kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kewanja Tarime. Asilimia 95 ya dhahabu ya Bulyanhulu inasafirishwa nje kutokea kiwanja cha Bulyanhulu. Asilimia 95 ya dhahabu ya Buzwagi inasafirishwa kutoka Buzwagi...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Alichofanya Rais ni kuzuia mapanki wakati minofu inakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *for the record* naomba niseme, hizo Kamati mbili za Profesa Mruma na Profesa Osoro ni *Professorial rubbish*, ni uongo, uongo uongo. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Mpelekeni Mirembe huyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu kaa chini.

**MBUNGE FULANI:** Kachanganyikiwa, tumpeleke Mirembe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, muda wako umekwisha na lugha unazotumia Bungeni sio sahihi. Kwa hiyo, naomba neno hilo *rubbish* ulifute, *please*.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Changia hoja zako, Kiti kitakuruhusu uchangie hoja, huwezi ukazungumza vitu kama hivyo lugha ambazo si za kistaarabu ndani ya Bunge. Kwa hiyo nakuomba ufute hilo neno lako.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Taarifa mbili zilizotolewa na Profesa Mruma na Profesa Osoro hazina utaalim wowote, haziwezi zikasimama mahali popote. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Oooooooooo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Lusinde. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa dakika tatu za kuunga mkono Azimio la Bunge kwa ajili ya kumpongeza Rais kwa hatua madhubuti alizochukua kuhakikisha kwamba nchi yetu inanufaika kikamilifu na uchimbaji wa madini hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli viongozi wote waliotangulia, naomba unyamaze usiniite, nitakutakana halafu nitaonekana sina maana. Eeh kwa sababu wewe unaniita jina la nini mimi mume wako niache nichangie. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Lugha ya maudhi hiyo.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli viongozi wote waliotangulia waliunda Tume na ni kweli wakati ule sheria zetu zilikuwa zina wa-*favour* sana wawekezaji kwa wakati ule wa 1977, 1979, tulihitaji wawekezaji waje wawekeze kwenye sekta ya madini ambapo hawakuwepo wawekezaji wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume zile zilizoundwa zilifanya kazi zake lakini Tume ya Mheshimiwa Magufuli kwa nini tunaipongeza, imefanya kazi na yeye mwenyewe ameenda mbele zaidi. Ameweka wazi ripoti za hizi Tume tena hadharani na kila mtu amezisikia tofauti na Tume zilizoundwa hapo kabla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua hii kubwa kwa sababu haiwezekani Taifa lisimpongeze kiongozi wake anapochukua hatua zinazoonekana kwa macho. Hapa nilisema na leo tumegawana, ukishindwa kupongeza, utapongeza wale wanaotuibia na imekuja hiyo wazi kabisa kwenye Bunge hili, umeona ripoti za Maprofesa, wataalam zinaitwa za upuuzi kwa sababu kuna watu wanaunga mkono upande mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi ambao tuko kwenye Bunge hili ambao tunaona kazi nzuri iliyofanywa na Rais, nataka niwaambie tu, siyo msemaji wake lakini nimeona kuna *clip* Mzee Lowassa naye kampongeza Rais. Sasa sijui hawa ambao wanakataa kumpongeza Rais wanaitoa wapi, kwa sababu hata Sumaye amempongeza Rais na ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA. Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema Bunge zima lina wajibu wa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua kubwa alizozichukua. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kurekebisha sheria, hivi kwenye Bunge la Bajeti hili, umeletwa Muswada wa kurekebisha sheria ya madini? Labda uelewa wangu mdogo, kwa sababu haiwezekani ulete Muswada sasa hivi turekebishe hizo sheria wakati tuko kwenye Bunge la Bajeti. Hapa tunachukua hatua ya kumpongeza Mheshimiwa Rais halafu tuitake Serikali ilete haraka Miswada ya kurekebisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niungane na Wabunge wote wazalendo wa nchi hii ya Tanzania ambao wanampongeza Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, kumekuwa na maneno mengi katika jambo hili. Tukitizama hoja ambayo ipo hapa ndani ya Bunge letu Tukufu, hoja yenyewe kimsingi inatutaka sisi Wabunge kwa pamoja tuungane na Watanzania wenzetu ambao kwa mara ya kwanza wameshuhudia uzalendo, ujasiri na hekima na busara iliyotumiwa na Rais wetu katika kutekeleza llani ya Uchaguzi na mwenendo mzima wa utendaji kazi wa Serikali katika kulinda rasilimali za Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika historia ya nchi yetu ya Tanzania, nashukuru leo Mheshimiwa Tundu Lissu amezungumza vizuri sana, ameona kuna umuhimu tunapompongeza Rais Dkt. John Pombe Magufuli tuwapongeze na Marais waliotangulia pia. Ingawa jana Tundu Lissu huyo huyo aliwadhalilisha pia Marais waliotangulia katika hoja hii hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachojifunza hapa ni kwamba hata dhamira ya mioyo ya wenzetu kumbe wanakubaliana na kazi nzuri aliyoifanya Rais...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Pamoja na watangulizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa nini? Marais waliotangulia walianzisha hoja hii kwa namna moja ama nyingine kwa kuunda Kamati zile zinazojulikana, lakini kazi iliyokuja kuendelezwa ambayo pia tunaipongeze vizuri leo, ni kitendo cha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wetu, kuziweka kwanza ripoti hizo zote mbili hadharani

na zikasikika na Watanzania wote. Pili, ni kuanza kuchukua hatua kwa ripoti ile ya kwanza. Tatu, ni kutoa maagizo makubwa kwenye ripoti hii. Kwa hiyo, Watanzania wote...  
(*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante dakika tatu zako zimekwisha. Sasa namwita Mwenyekiti aje ku-*wind up* hoja yake. (*Makofi*)

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa tena nafasi. Mimi leo nimefarijika sana katika Bunge hili. Watu wote waliochangia upande wa CCM na upande mwingine hakuna aliyesema Rais kakosea. Hakuna aliyesema Rais kakosea, mwingine anasema hapana tunashangilia mapema mpira, tsubiri mwishoni. Mimi ninavyofahamu mpira unashesha dakika 90, filimbi ikipigwa tu mwenye timu yake anashangilia hangoji dakika ya mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwa kifupi sana, ndugu yangu pale Mheshimiwa King ameunga mkono hoja tunashukuru, Mheshimiwa Mchengerwa ameunga mkono hoja tunashukuru, ndugu yangu Mheshimiwa Mtolea pale ndiyo yule kasema kwa nini tunapongezana bado safari ni ndefu (*encouragement*), watu wote wa Tanzania wanajua kwamba Rais anafanya kazi ngumu ili aendelee kuifanya ile kazi nzuri anahitaji kutiwa moyo, ndiyo hiki tunachokifanya hapa. Hata hivyo, nampongeza ndugu yangu Mheshimiwa Mtolea, wala hajasema Rais kakosea kuunda wala hajasema, ndiyo nilichompenda hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia anasema tuongeze nguvu za kuzuia dhahabu. Kwa upande mwingine ukilinganisha lugha yake hiyo ni kama vile yupo pamoja na Rais, hivi wenzangu mnaonaje? (*Makofi/Vigelelele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu Mheshimiwa Hasunga ameunga mkono hoja, lakini hili suala la mikataba mimi

nilisikiliza juzi Rais wakati anapooonea, alisema yale mambo ya kisheria, pale ambapo mikataba haikukaa sawa, pale ambapo sheria haikukaa vizuri, Serikali itatuletea hapa Bungeni ili tuiptie na kurekebisha. Sasa naomba usitie unga kupika ugali kabla maji hayajachemka. Ukitia mapema utapata uji badala ya ugali. Tsubiri muda ukifika hiyo kazi tutaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Kangi Lugola ameunga mkono, ndugu yangu Mheshimiwa Tundu Lissu pale alikuwa anacheka maana yeye pamoja na lugha yote ya ukali, hakuna Mheshimiwa Tundu Lissu aliposema napinga Rais kuunda Tume, mmemsikia anasema hivyo? Tuko naye pamoja katika hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Bunge moja hapa aliwahi kuja Spika wa Bunge la Kenya anaitwa Ole Kaparo, akasema kwamba, katika nchi zingine vipo vyama vinaitwa Chama Pinga. Chama Pinga maana yake yeye hata ukimwambia mbili jumlisha mbili jawabu nne atakwambia hapana tano. Sasa sifikiri kama ndugu yangu Mheshimiwa Tundu Lissu amefika huko kwenye hatua ya kusema mbili jumlisha mbili saba. Kwa hiyo, nasema nimemsikiliza sana ndugu yangu Mheshimiwa Lissu yeye ni mzalendo na jana kwa mfano hata wenzetu upande wa Upinzani walisema, tulikuwa tukipiga kelele hamkutusikia, hamkutusikia, sasa tumekusikieni leo, si msem basi *Alhamdulillah* mmetusikia. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile la kuwasifu Marais waliotangulia nadhani Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni kasema, sisi ni Bunge la mwaka 2015-2020 tunashughulika na mambo yaliyomo ndani ya kipindi chetu. Wale Marais waliotangulia walianza Magufuli anaendeleza pale walipoachia wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kama nilivyosema sitaki kupoteza muda, hili Azimio limepokelewa vizuri, pande zote mbili wamelipamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(Makofi)

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono kwa wingi na pande zote naona.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa wapi.

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji kuhusu Azimio la Bunge kumpongeza Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua alizochukua kukabiliana na upotevu wa mapato ya Serikali katika sekta ya madini nchini.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda kwa kura nyingi sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii kupongeza Azimio hili zuri na wale waliosema siyo kimoyo moyo mmesema ndiyo.

**WABUNGE FULANI:** Hapana, hapana.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, niwapongeze Wabunge na tumpongeze Mheshimiwa Rais, tuungane naye kupambana na vita hii kubwa sana ambayo sasa hivi ameivalia njuga na kuhakikisha rasilimali za nchi yetu zinabakia. Rais amesema vizuri juzi, amewaambia wahusika wote waje wakubali walipe pesa biashara iendelee, hakuna lingine zaidi ya hilo. Tunaendelea.

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajenda ambayo ipo kwenye *Order Paper* yetu ni ajenda ya mjadala wa hotuba ya bajeti ambayo imesomwa na Waziri wa Fedha na Mipango. Kwenye hotuba hii ya bajeti kumekuwa na suala zima la mjadala kuhusiana na mapato yanayopatikana kupitia kwenye vyanzo mbalimbali ikiwemo rasilimali za Taifa lakini hususani suala zima hili la rasilimali ya madini ambayo ipo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaendelea na michango hii, tumeendelea kuchangia tukitafakari pia kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli na hasa baada ya kuunda Kamati hizi mbili ambazo zimetupa picha kuhusiana na rasilimali hii ya madini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mjadala unaohusiana na hoja hii, yamejitokeza mambo ambayo naomba kupatiwa Mwongozo kutoka kwenye Kiti chako. Ibara ya 66 na vifungu vingine vidogo katika Ibara hiyo, vinazungumzia kinga dhidi ya madaraka ya Rais wetu lakini katika mjadala huu, kumejitokeza baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakiunganisha mjadala huu na kuwaingiza Marais Wastaafu na kutaka Marais Wastaafu wachukuliwe kama vile wana hatia lakini kwa kupitia kazi nzuri iliyofanywa na Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli.



Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako hivi katika kushughulika na jambo ambalo liko Kikanuni ambalo ni *specific* tunaloendelea nalo na haya yanayojitokeza sasa yanayowahusu Marais wetu wastaafu. Je, Bunge hili liko sahihi katika kufanya jambo hilo kama nilivyolisema na ninavyoliomba mwongozo. Naomba sana mwongozo wako ili jambo hili mahsusi la suala la bajeti na kazi nzuri iliyofanywa na Rais, liweze kutenganishwa na haya mengine ambayo yameendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Vipi na wewe una mwongozo?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana hii hoja kinachoitwa mwongozo na Mheshimiwa *Chief Whip* wa Serikali ni lengo la kuzuia mjadala. Masuala yaliyozungumzwa ya Marais wastaafu ni sahihi kabisa kwa sababu kama nilivyosema jana Mheshimiwa Jakaya Kikwete ndiye aliyesaini leseni ya Bulyanhulu, ya Nzega, Geita akiwa Waziri Maji, Nishati na Madini, hakuwa na kinga *then* hana kinga leo. Anayo kinga kwa mambo aliyoyafanya kama Rais, kwa hiyo hii hoja ya kutaka wawekewe ulinzi wasiokuwa nao usikubaliane nayo, hawa watu wajadiliwe kwa madhambi waliyolitendea Taifa hili. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimesikia nimeombwa miongozo miwili, hata mkiwa Mahakamani, pande za utetezi na pande za mashtaka wanapotoa hoja zao ni Jaji ndiye anayetoa *ruling* ya mwisho, kama mtu haipendi inakuwa ni bahati mbaya lakini Jaji ndio anatoa *ruling* yake ya mwisho. Sasa nikijibu miongozo yote miwili *ruling* yangu ni hii inayofuata:-

Waheshimiwa Wabunge, kuanzia tarehe 13 Juni, 2017 baadhi ya Wabunge katika mjadala, nikisema mimi wengine

mnakaa kimya, Mheshimiwa Grace nakuomba nisikilizeni ninachokisema muache ku-- *interrupt* mazunguzo yangu kwa pande zote mbili, ndio utaratibu wa Kibunge. **(Jina la Mheshimiwa Grace ambalo Mwenyekiti amelitaja siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)**

Kuanzia jana tarehe 13 Juni, baadhi ya Wabunge katika mjadala hapa Bungeni wamekuwa wakiwataja Marais wastaafu na kuwahusisha na masuala mbalimbali yanayoendelea katika sekta ya madini nchini na kudai kwamba Marais hao nao wachukuliwe hatua.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo nimesema Waheshimiwa Wabunge asiyependa kunisikiliza aende nje, Waheshimiwa Wabunge mnadharau mamlaka ya Kiti, kuna mtu anadharau Mamlaka ya Kiti anyooshe mkono wake. Hamdharau eehh? Kaeni kimya sasa, hamdharau ehee kaeni kimya sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 inatoa kinga kwa Rais aliyeko madarakani na hata Rais mstaafu Ibara ya 46(3) inaelekeza kwamba itakuwa ni marufuku kumshtaki au kufungua Mahakamani shauri lolote la jinai au la kumdai mtu aliyekuwa anashika madaraka ya Rais baada ya kuacha madaraka hayo kutokana na jambo lolote alilolifanya wakati alipokuwa bado anashika madaraka ya Rais kwa mujibu wa Katiba. Isipokuwa tu kama aliacha Urais baada ya Bunge kupitisha Azimio kwa mujibu wa Ibara ya 46(a).

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 64 inatoa makatazo kwa masuala mbalimbali ambayo hayaruhusiwi wakati wa mjadala Bungeni, Kanuni hiyo pamoja na mambo mengine inazuia kujadili mwenendo na utendaji kazi wa Rais aliyeko madarakani na kwa tafsiri pana Kanuni hiyo inazuia pia kuzungumza mwenendo wa Marais wastaafu ikiwa Rais mstaafu huyo alitumikia nchi kwa miaka yote inayotakiwa

Kikatiba na kuondoka madarakani bila kuondolewa na Bunge au kwa nanma yoyote ile. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa mantiki hiyo tujielekeze katika mjadala uliopo Bungeni kwa sasa bila kutumia nafasi hiyo kuwashambulia viongozi wetu waliotumia nguvu na uwezo wao kutumikia nchi kwa mara nyingi. Waheshimiwa Wabunge hiyo ndio *ruling* yangu. Ndio *ruling* ya leo, ahsanteni kwa makofi, hii ndiyo *ruling* yangu na *ruling* hii ni tahadhari kwa yeyote. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mmeona mapendekezo ya ripoti, mmeona mapendekezo ya azimio, yeyote atakayehusika si lazima atajwe humu ndani watashughulikiwa na vyombo vinavyohusika. Kwa maana hiyo...

Naona kuna mtu anataka kufuturu mapema huku. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

na

**Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ruth Mollel, ajiandae Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia japokuwa sikuwa najua nachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wasilisho la Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango nina mambo matatu ya kuchangia. Jambo la kwanza linahusu *development budget* ambayo kwa miaka yote tumekuwa tunapata *development budget* kidogo na tunakuwa na maoteo makubwa na ni kwa nini Mheshimiwa Mpango hatuwezi ku-*budget* maoteo *realistic* ambao haiwezi kuwa na tofauti kubwa, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu *property tax*. Nilipokuwa nachangia majuzi kwenye bajeti ya Wizara nililizungumzia hili la *property tax* na bado nalizungumzia kwa sababu kuchukua *property tax* ya *Local Government* tunazua *Local Government* na dhana ya *D by D* inadhoofishwa kwa sababu maendeleo yote yako katika *Local Government*, ndiko kuliko na shughuli za jamii, elimu, maji, barabara na afya. Ikiwa *property tax* inachukuliwa basi hizi huduma za jamii zitakuwa hazipatikani kwa wakati na kukaa kusubiri *return* kutoka Serikalini inachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka jana Mheshimiwa Kamala alizungumza akasema kwamba *D by D* siyo lazima mtu akusanye mapato, lakini dhana ya *D by D* ni lazima upeleke *resources* za pesa ni lazima upeleke *resources* za watu kuiwezesha *Local Government* iweze kufanya kazi yake vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo *property tax* ambayo imezungumzwa pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu zile nyumba ambazo hazijathaminiwa, ghorofa Sh.50,000/= nyumba zingine ambazo ni siyo za ghorofa ni Sh.10,000/=. Kwa kweli, kwenda kutoza Sh.10,000/= kwa nyumba za tope na majani ni sawasawa na kuwaongezea wananchi wetu umaskini. Kwa sababu wengine kwanza wako kwenye *TASAF*, sasa unampelekea pesa za *TASAF*, halafu unamtoza Sh.10,000/=. hiyo ataitoa wapi kama yeye hela yenyewe anaisuburi ya *TASAF*? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, labda wenzetu wa CCM wanatoka kwenye vijiji vina maendeleo sana lakini mimi nikiangalia kule kwangu Arusha kwa mfano, utakwenda kwenye vile vijumba vya majani unakuta huyu Mama watoto ni vumbi, ni nguo zilizochanika hizo shilingi 10,000 watazitoa wapi? Naona tutarudia kama wakati wa kikoloni ule wanapokuja watu wa kodi wazee wanaingia porini, hicho ndicho kitakachotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Menyekiti, napendekeza Mheshimiwa Mpango hiyo Sh.10,000/= ya kutoza nyumba za matope na nyumba za majani tafadhali sana iondolewe tuwapunguzie wananchi wetu umaskini. Napendekeza pia katika zile tozo za nyumba ya Sh.50,000/= kwa za ghorofa na zingine ambazo wanaishi wazee wastaafu au wazee wenye zaidi ya miaka 60 na kuendelea wasitozwe hiyo kodi ya Sh.50,000/= kwa ajili ya kurahisisha maisha yao, kama wanavyofanya watumishi wastaafu wa Serikali ambao hawalipi *property tax* katika nyumba wanazoishi. Kwa hiyo, wazee hawa wa miaka 60 na wenyewe kama ni nyumba ni ya ghorofa ni Sh.50,000/= haijathaminiwa kama anaishi humu ndani asitozwe hiyo kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi hii ya mafuta kwa kweli nasikitishwa kwa sababu tumetoa mzigo kutoka kwa *upper class na middle class* tumepeleka kwa watu wa chini. Kama kweli Serikali ya Awamu ya Tano ina dhamira ya kupunguza umaskini basi hiyo Sh.40/= ya mafuta itolewe kwenye mafuta ya taa. Kwa sababu hao tunaokwenda kuwadai Sh.40/= kwenye mafuta ya taa ni watu ambao kwa kweli maisha yao ni duni sana. Haiwezekani Shangazi yangu yuko kule yuko kwenye kile kijumba anatomia mafuta ya taa halafu tunamtoza Sh.40/= wakati huo mzigo ungetakiwa kubebwa na *upper class na middle class*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kama kweli tuna dhamira ya kweli ya kuwajali wanyonge hiyo Sh.40/= itolewe kwenye mafuta ya taa, wananchi wetu kule mikoani na vijijini waweze kutumia mafuta ya taa. Natofautiana na Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza

akasema sijui utaleta gesi, hiyo gesi itakuja lini? Ni kama alivyozungumza Mbunge mwenzangu mmoja atakuwa kama yule *First Lady* wa Ufaransa, watu wanataka mkate yeye anasema wapeni keki. Kwa hiyo, ninayo hayo mapendekezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Menyekiti, tukiangalia pia hata katika suala la mafuta japo wengine wanasema kwamba *ooh!* bei haiwezi kupanda lakini haiwezi ikaenda bure kuna mahali watu watalipa zaidi au kwa kusafirisha mizigo au kwa usafiri wa kawaida na wataendelea kulipa, nasisitiza ile Sh.40/= ya mafuta ya taa iweze kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba Mheshimiwa Mpango achukue mawazo yangu kama kweli Serikali ya Awamu ya Tano ina dhamira ya kuwaondolea wananchi umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa niliposimama asubuhi hii, nilitaja jina la Grace Kiwelu kama moja ya mtu ambaye amefanya kosa, kwa kweli hakuwa Grace Kiwelu nakuomba radhi kwa kutaja jina lako na naomba *Hansard* ifute jina la Grace Kiwelu kwenye maneno yangu yote niliyoyasema leo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Lugola, ajiandae Mheshimiwa Mlata.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii ya Serikali. Kwanza kabisa nimpongeze Dkt. Mpango na watu wake kwa kuleta bajeti ya kihistoria katika Bunge lako Tukufu, bajeti ambayo tunaamini kwa kiwango kikubwa itakwenda kutoa majibu ya mapambano dhidi ya umaskini ambao umekithiri miongoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda hotuba yangu ya leo itajikita katika kuwaelimisha wenzangu ambao

pengine wanadhani wao ndiyo wanajua sana mambo kuliko wengine ili tuweze kuelewana na Watanzania waweze kutuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kabisa na hotuba aliyotoa rafiki yangu Mheshimiwa David Silinde ninayemheshimu sana katika ukurasa wa 158 wakati anahitimisha alisema, nimalizie kwa kuwakumbusha Watanzania kuwa Serikali hii ya CCM inayoongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mheshimiwa John Pombe Magufuli imekuwepo madarakani miaka mingi toka Taifa letu lipate uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa sana kama kweli hii kauli ndiyo ya bajeti mbadala. Mheshimiwa Magufuli tunayemzungumzia leo ni tofauti kabisa na Mheshimiwa Magufuli aliyekuwepo jana. Mheshimiwa Magufuli wa jana alikuwa ni Waziri tu katika Serikali ya Awamu ya Nne lakini Mheshimiwa Magufuli wa leo tunamzungumzia Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamzungumzia Magufuli ni mtu wa namna gani. Ukienda Ibara ya 33 (2) inasema Magufuli ni Rais ambaye ni Mkuu wa nchi, ni Kiongozi wa Serikali, ni Amiri Jeshi Mkuu. Hiki pekee yake kinaonesha utofauti wake na alivyokuwa Magufuli wa jana, inakuwaje leo watu wawe na mashaka juu ya maamuzi na utendaji wa Rais John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Menyekiti, Mheshimiwa Magufuli wa leo kwa mujibu wa Katiba hii ana madaraka ya kutangaza hali ya hatari katika nchi Ibara ya 32. Magufuli wa leo ni tofauti na Magufuli wa jana, Magufuli wa leo Ibara 44 ya Katiba ana madaraka ya kutangaza vita dhidi ya nchi nyingine ambayo inaweza kuvamia mipaka yetu. Magufuli wa leo ni tofauti na Magufuli wa jana, Magufuli wa leo ana uwezo wa kutoa misamaha, Magufuli wa leo ndiye ambaye ni mlinzi mkuu wa rasilimali za nchi yetu. Inakuwaje ndugu zetu kama mnasoma Katiba hii leo mumlinganisha Magufuli wa jana

na Magufuli wa leo? Huyu ni Magufuli tofauti na ndiyo maana ameanza na kushughulika na rasilimali za Watanzania na Watanzania sasa tunapaswa kumuunga mkono Rais wetu ambaye amejitoa muhanga ili Watanzania tuondokane na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa rafiki yangu Tundu Lissu ninayemheshimu sana wakati tunampongeza Rais hapa, mimi nilidhani yeye kama Rais wa *TLS*, angetuambia kwamba sasa ameshajipanga kupitia *TLS* skuleta mapendekezo mazuri hapa ambayo tutakwenda sasa kutazama mikataba na lile agizo la Rais ambapo amemwambia Spika kwamba inawezekana akatuongezea muda ili Sheria hizi ambazo zina wizi ndani yake tuje hapa tuzibadilisha. Badala yake Mheshimiwa Lissu anasema kwamba hakuna chochote na yeye sasa hajajiandaa. Anaonesha vitabu hapa vya Kamati zilizopita, nilitazamia pia aoneshe na *book* lililosheheni la Wanasheria kwamba tayari sasa wana kitu kizuri watakachotuletea hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu Mheshimiwa Lissu anapenda sana kukimbilia *MIGA (Multilateral Investment Guarantee Agency)*. Mimi ninayo hiyo *Convention* hii hapa, ambayo Mheshimiwa Lissu kila wakati anaisema tu lakini hana mimi ninayo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii *convention* ukiangalia *article* ya 12(3) ambacho kinazungumzia *Eligible Investments* kinasema hivi:

*“Uwekezaji wowote utakuwa eligible pale ambapo utakuwa na yafuatayo:- Namba 3 unasema compliance of the investment with host Countries laws and regulations.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu uwekezaji wa wezi hawa hauko *eligible*, kwa hiyo *MIGA* hii haitawatetea hata siku moja, wanatakiwa...



## TAARIFA

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Kangi Lugola siyo cha kweli na hakifahamu. Mikataba ya Madini kati ya Serikali hii ya CCM na Wawekezaji hawa mnaowaita leo wezi, marafiki zenu wa miaka yote, imeingiwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini, kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania, kwa mujibu wa Sheria zetu za Kodi. Unazungumza jambo usilolifahamu, ndicho ilichosema Kamati ya Bomani, ndicho ilichosema Kamati ya Masha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante ameshakuelewa, Mheshimiwa Kangi Lugola taarifa unaipokea.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lissu ambaye namheshimu sana na ambaye ni msomi, atalifanya Bunge hili lishindwe kuamini kauli zake. Mheshimiwa Tundu Lissu huyu kila wakati yeye ndiye alikuwa anazungumzia hii *MIGA* na *MIGA* hii ndiyo nimelelea ili nimwelimishe, katika kumwelimisha nimemsomea kipengele cha tatu ambacho kinasema wazi kwamba wale Wawekezaji lazima wafuate sheria za nchi, kama hawafuati sheria za nchi, matokeo yake *MIGA* haiwezi ikawaunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** *Order, Oder in the House!* Mheshimiwa Lissu ulishapata nafasi yako kaa chini, kaa kimya. Mheshimiwa Lugola endelea.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Walimu huwa wanafundishwa na Walimu wengine, mimi leo ni Mwalimu wa Tundu Lissu akae kimya ili niweze kumfundisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Rais wa nchi yangu katika hilo, kwa kuwa hawa watu, ripoti imesema bayana ikiwa na Wanasheria na Wachumi kwamba hawa watu vitu vitatu; moja ni wezi, mbili wametoa taarifa za uwongo na tatu ni wahujumu uchumi. Mheshimiwa Rais

wangu John Pombe Magufuli bado anasubiri nini kuchukua hatua juu ya wezi hawa na nashangaa Mawaziri wanaomsaidia Mheshimiwa Rais yeye tayari amekwishawapa majukumu haya, leo ningetarajia Mheshimiwa Mwigulu kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani angekuwa anashughulika na kule Buzwagi kule Bulyanhulu. Nilitarajia Mheshimiwa Mwinyi ambaye yuko kwenye Majeshi, angekuwa anashughulika na maderaya yanayoenda kwenye migodi kwa sababu migodi hawa watu ni wezi, wanasubiri nini mpaka Rais ndiye aende tena Bulyanhulu kule. Tunesubiri sasa wakati huu akina Majembe *Auction Mart* wameshakwenda ku-*cease* ile migodi kwa sababu hawa ni wezi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao bado wanahangaika na hawa wawezeshaji tu, vinginevyo mimi nitakuwa mtu wa mwisho kuamini *report* hii, kama hawa watu ni wezi, bado tunasubiri nini, kama kweli hawa watu ni wahujumu uchumi, tumekwisha kuwa na Mahakama ya Mafisadi, matokeo yake popo wanakojoa mle, hakuna washtakiwa, mafisadi tumewapata leo, bado hawapelekwi. Nitashangaa sana! Kama wananchi hawana maji, wananchi wa Mwibara wanasota, leo tumepata matrillioni bado tena tunataka ku-*negotiate* tuna-*negotiate* na wezi, mwizi tuna-*negotiate* naye kwa sababu gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hapa, sasa hivi tunapeleka mzigo wa Sh.40/= kwenye mafuta kwa ajili ya wananchi wapate maji ilihali matrillioni ya pesa tumekwishayapata kwa wawekezaji hawa, lakini bado tunasema tunataka ku-*negotiate*, tunataka ku- *negotiate*, ku-*negotiate* huku watakuwa nao Bahari *Beach* au Kilimanjaro Hoteli kwenye viyoyozi, wanakunywa *juice* na wakati hawa ni wezi! Namwomba Mheshimiwa Rais aende mbele zaidi ili achukue hatua kwa ajili ya watu hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hii tozo ya Sh. 40/= kwenye mafuta, ndugu zangu tusitake kuwadanganya na kuwapotosha Watanzania. Kwanza tumefuta *road license*, *road license* tumeifuta haipo tena,

tulichofanya ni kuhakikisha tunaongeza Sh.40/= kwenye lita ya mafuta ili Watanzania wote waingie gharama ili Serikali yetu iweze kutupatia maji, kwa hiyo mtu anaposema kwamba Sh.40/= haimsaidii mtu ambaye hana gari, hatuzungumzii gari pale, tunazungumzia kukusanya pesa kwenye mafuta ili zile fedha tuzipeleke kwa Watanzania wote ambao wanahitaji maji. Kila mtanzania lazima achange na hata nauli hizi wanazosema zitapanda Serikali yetu inavyo vyombo vya kudhibiti nauli, *SUMATRA* wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba Mheshimiwa Rais huyu *SUMATRA* ambaye hasimamii nauli hizi zinazopanda kiholela, *SUMATRA* ndiye mtu wa kwanza kutumbua huyu. Sisi tunaongeza pesa kwenye mafuta, hatumaanishi kwenda kupandisha nauli kwa wananchi bila kupitia *SUMATRA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie hili la mwisho, kuna suala ambalo limetusumbua kwa muda mrefu, hili suala la ukusanyaji wa mapato. Kila wakati Mheshimiwa Mpango, mapato haya tunaambiwa wanakusanya vizuri wamefika kwenye trilioni lakini mapato haya hatuyaoni, sasa kama hatuyaoni na leo tunaenda kwenye trilioni 32 na zaidi, tunataka atakapokuja kuhitimisha hapa, atuondolee wasiwasi na sisi tusiwe tunaendelea kila wakati, tunapitisha bajeti za makaratasi, tunapokwenda kwenye utekelezaji pesa haziendi, pesa hazionekani halafu wanakuja na lugha nyingine vilipanda, vilishuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa mtu wa mwisho sasa, bajeti ya mwaka jana ilikuwa ni ya kwanza ya Mheshimiwa Rais, alikuwa anajipanga, sasa imekuja bajeti ya pili, bajeti ya pili namhakikisha Mheshimiwa Mpango kama hatapeleka pesa kwenye Halmashauri zetu za Wilaya, kama hatuta-*finance* miradi, nitakuwa mtu wa kwanza bajeti yake inayokuja kuikataa kwa sababu nitaamini ni wale wale waliokuwa wanatusumbua kwenye Serikali ya Awamu ya Nne kwa hiyo fedha hizi zikakusanywe, fedha hizi zipelekwe kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri hajaziondolea uwezo wa kuendesha Halmashauri zao, haya makusanyo ambayo wanayafanya sisi kama Wabunge hatuwezi kuwa sehemu ya kuua Halmashauri, kwa hiyo anayesema Halmashauri tunakwenda kuziua si sahihi. Halmashauri zitaendelea kuwepo, Halmashauri wataendelea kutekeleza miradi, hata hizi kodi ambazo tunasema kwamba wanaenda kutozwa watu kwenye nyumba za tope, huu ni uwongo wanataka kuwadanganya wananchi, hakuna mwananchi ambaye nyumba yake ya tope inaenda kutozwa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba ambazo zinaenda kutozwa kodi tumeanza na mjini na hizi nyumba za mjini kwenye Halmashauri baadaye ndiyo tutaenda kule vijijini kuangalia zile nyumba ambazo zina viwango, siyo kila nyumba ya mwananchi ambaye amejenga nyumba ya tope na yenyewe inaenda kutozwa, huu ni uwongo ambao wanataka wenzetu kutuchonganisha na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ni Bunge la kihistoria, hili ni Bunge ambalo Rais wetu tunayemfahamu kwa mara ya kwanza wakati anapiga pushapu, Watanzania wengi hawakumwelewa hizo *push-up* alizopiga alikuwa anamaanisha yeye ana nguvu, yeye ana afya njema, yeye ana uwezo, ndiyo maana anasema tumwombee Watanzania. Mheshimiwa Rais tuko nyuma yako tutaendelea kukuombea na ndiyo maana nawaomba Wabunge kupitia Bunge hili tusimame tumwombee. Eee Baba yetu uliye Mbinguni tunakuomba Rais huyu ambaye ulituletea umuwekee mkono wako, umwepushe na ajali, umwepushe na mikono ya watu ambao wanamnyemelea, wengine wako humu... *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlata ajiandae, Mheshimiwa Gama.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia mjadala huu ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na timu yako yote, kwa kweli sisi hatuna mashaka na wewe na kadri miaka inavyozidi kwenda naamini mambo yataendelea kuwa mazuri. *So, endelea hivyo na Mungu aendeleo kukubariki. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa nataka nichangie ila kwa huzuni sana, nina uchungu sana, kwa sababu alitokea mtoto mmoja akasoma, akalelewa mikononi mwa wazazi wa Chama cha Mapinduzi, akasoma kwa kodi ya Watanzania na wananchi wa Singinda hususani wananchi wa Ikungi Mashariki, Mheshimiwa Tundu Lissu mdogo wangu. Wananchi wa Singida wakamwamini wananchi wa Ikungi Mashariki, wakampa nafasi nenda baba katutetee, ukatuombe shida zetu huku, wananchi wa Ikungi hivi ninavyoongea wanawake wana taabu, walimwamini kijana wao aje alie ndani ya Bunge ili waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimtegemea kijana wao akawakomboa na shida zao. Naomba niongee kwa ajili ya wananchi wa Ikungi, Ikungi maji salama ni asilimia 25 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii leo niwasemie akinamama, naomba maji yaende Ikungi hawana mtetezi humu ndani, kwa sababu mtoto wao kahamia kwa Wazungu. Kwa hiyo, naomba sana maji yaende Ikungi. Hakuna barabara kule, umeme ambao umepelekwa kule ni vijiji 44 tu kati ya... *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata kaa chini. Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba lugha za kuudhi ndani ya Bunge kusema Mbunge amehamia kwa Wazungu siyo lugha nzuri, tutumie lugha za

kistaarabu ili amani iwepo Bungeni, ndiyo ombi langu na tunamwomba msemaji afute au athibitisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata Bunge hili tunakwenda na Kanuni, as *much as* watu wana- *enjoy* lakini mimi nasimamia Kanuni hapa ambazo tumezipitisha wenyewe. Huna haja ku-*profile* mtu yeyote humu ndani, mjadala ambao uko hapa ni mjadala wa bajeti, zungumza mambo ya bajeti, mambo ambayo yameruhusiwa na Kanuni zetu. Kwa hiyo, nakuomba jielekeze kwenye bajeti ya mambo ambayo unayaona wewe yanakuhusu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hatutaki kuvuruga mjadala wala Bunge hapa, kila mtu ajenge hoja inayomhusu kwenye Jimbo lake.

**WABUNGE FULANI:** Mbunge wa Mkoa.

**MWENYEKITI:** Kama ni Mkoa sawa, kama ni Mkoa sawa, lakini hamna haja ya kupigana vijembe humu ndani. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Uliyesema aaah! nimekusikia nitakutoa nje. Mimi nasimamia Kanuni hapa, sisimamii chochote kingine, kwa hiyo endelea na hoja zako kama unazungumzia Mkoa, Kitaifa zungumza huna haja ku-*profile* watu. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi kwa kweli naomba nijielekeze kuwatetea wanawake wa Mkoa wa Singida hususani wa Jimbo la Ikungi Mashariki. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Kuna Ikungi Mashariki nchi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu sijakuita kaa kimya.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Makyungu iko Singida Mashariki. Hospitali ya Makyungu mpaka sasa hivi huduma za maji pale ni hafifu, naomba sana Wizara kwa sababu Hospitali ile imekuwa ikitoa huduma nzuri sana na kuna ongezeko la watu, naomba Wizara iiangalie kwa jicho la pekee kupeleka maji pale Makyungu ili yaweze kuhudumia wananchi wanaoishi maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza haya bado nitashukuru sana kwenye Jimbo la Singida Magharibi pale Sepuka, kuna mradi wa maji mkubwa ambao umepelekwa pale, kwa hiyo naishukuru sana Wizara kwa sababu wamepeleka milioni 101, naamini zitasaidia maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasema haya kwa sababu nafahamu kazi kubwa ambayo anaifanya Rais wetu, anapaswa kuungwa mkono na watu wanaowatetea wanyonge. Kama kweli wewe ni mtetezi wa wanyonge utapaswa umuunge mkono Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nasema haya kwa sababu mpaka sasa hivi tunavyoongea akinamama wa Singida hususani Singida Mashariki wanashindwa kwenda kujifungulia kwenye Vituo vya Afya kwa sababu huduma kule hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Rais wetu ameamua kulinda rasilimali za Taifa letu ili ziende zikaokoe hata wale akinamama wanaofia njiani kwa sababu ya kushindwa kwenda kwenye vituo vya afya, mtu anasimama anasema amekosea, inauma sana! Nampongeza Rais wangu na tutaendelea kumuomba na nataka kusema hivi, nawapongeza wale wanaompongeza, hata neno la Mungu linasema ni heri uwe baridi au moto kuliko kuwa vuguvugu, kwa sababu ukiwa vuguvugu kinywa cha Bwana kitakutapika, unaelewa maana ninayoisema hii. Ni lazima tumuunge mkono Rais wetu katika juhudi hizi anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Singida, bomba la mafuta linaloenda Tanga, linapita katika

Wilaya tatu katika Mkoa wetu wa Singida, wananchi wa Singida wanakwenda kunufaika na juhudi kubwa ambazo zimefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi, mwizi ni mwizi tu, iwe umeweka mkataba mbovu, usiwe mbovu, mwizi ni mwizi na akikamatwa achukuliwe hatua. Nilimsikiliza Rais wetu, ameonesha huruma kubwa sana amesema jamani njooni tuzungumze ili mtulipe pale mlipoona mmetuibia tatizo liko wapi? Naomba tumpongeze Rais wetu ili hawa watu ambao naamini kesho na kesho kutwa tutawaona wanaenda kutaka suluhu kwa ajili ya kutulipa, kwa hiyo nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pale Londoni na pale Sambaru huko Mashariki ya Singida, kuna matatizo makubwa ya wachimbaji wadogo, nategemea tusimame kuweza kuwatetea wachimbaji wadogo pale, tukimuunga mkono Rais wetu, hata wachimbaji wetu wadogo pale watanufaika na mradi uliopo pale. Mwekezaji aliyepo pale tangu 2006 mpaka sasa hajalipa *compensation*, mpaka sasa wananchi wanahangaika, naomba sana tumuunge mkono Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kengele ya kwanza, kabla sijamalizia nataka nimalizie kwa kusema hivi, Mheshimiwa Magufuli songo mbele, ukiona watu wanakupinga, ujue kuna jambo limejificha nyuma yao, ama wanaona aibu na upinzani wa kupinga kila kitu utajipinga hata wewe mwenyewe, kuna mambo ambayo utayasema leo kwa sababu ya kupinga, utapinga kesho. Mheshimiwa Rais wetu naomba usonge mbele, wanaokupinga ni kwa sababu wanaona nchi hii inakwenda kupaa, nchi hii inakwenda kunufaika na kwa sababu wanapinga na ni wachache wala hawatuwezi humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kusema hivi, ngoja nikae sawa.....



*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alimba -Kanyanga twende  
Magufuli wetu, Kanyaga twende, usiogopeeee)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
*(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gama na Mheshimiwa  
Bashe atafuata.

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niungane na wenzangu kuipongeza sana bajeti ya Serikali ya mwaka huu, ni bajeti ambayo tumeona wote, ni bajeti ya karne, bajeti ambayo haijawahi kutokea, ni bajeti ambayo imegusa kila mahali, bajeti ambayo imegusa wakulima, bajeti ambayo imegusa wafanyabiashara, bajeti ambayo imegusa wafanyabiashara wadogowadogo na akinamama lishe, bajeti ambayo imegusa viwanda, bajeti ambayo imegusa wafanyakazi, bajeti ambayo ina vipaumbele vinavyoonesha mwelekeo wa Taifa letu. Vipaumbele kama ujenzi wa reli, vipaumbele kama uanzishaji wa makaa ya mawe, vipaumbele vya ndege, vipaumbele vingi ambavyo vinaonesha mwelekeo mzuri kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza uzuri wa bajeti hii hatuna jinsi lazima tumsifu Rais wetu. Nataka niwakumbushe tu ndugu zangu, mwaka 2015 wakati tunajiandaa na uchaguzi Mkuu, watu wote tulikwenda kwenye Makanisa yetu, tulikwenda Misikitini, tukaomba tupate Rais mzuri ambaye atasaidia nchi hii. Hakuna aliyemtazamia Mheshimiwa Magufuli. Mheshimiwa Magufuli alilibuka alikoibuka na tumefika mahali tumeona. Tunaweza tukasema Mheshimiwa Magufuli ni chaguo la Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anavyosema mwenyewe na kama tulivyosema hapa, tumuombee. Tufike mahali tumpe moyo. Anavyovifanya havijawahi kufanyika nchi hii, tulitaka Rais wa namna gani? Kwa hiyo, nachukua

nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na mipango yote ya maendeleo ambayo ameipanga kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kitu kimoja, Mkoa wa Ruvuma ni moja kati ya mikoa inayozalisha kwa wingi sana mazao ya chakula. Wakati fulani ulikuwa kwenye *the big four*, ile *the big four* imepungua sana sasa hivi. Nafikiri niombe Serikali tuone namna gani tunaweza kuifanya *the big four* iwe kweli *the big four* ili tuweze kuzalisha chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwa Serikali, kama kuna uwezekano hebu tukusanye nguvu zetu zote badala ya kusambaza kwenye mikoa tofauti ili kujiletea uhakika wa chakula, twende tuwekeze kwenye mikoa ile yenye hali nzuri ya hewa ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Ruvuma. Tuangalie namna ya kupeleka mbolea ya uhakika ili watu walime bila wasiwasi, tuangalie namna ya kupeleka ununuzi wa mazao ili watu wauze kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo hatuna sababu ya kuhangaika na njaa katika nchi hii. Tukitumia mikoa miwili, mitatu au mikoa hiyo minne, tukaamua nguvu zetu zote za uzalishaji tuzipeleke kwenye mikoa ile, nina uhakika kabisa nchi hii itaondokana kabisa na tatizo la njaa, badala ya kuhangaika, mbolea tunapunguza, tunatafuta njia tunapeleka kwenye mikoa ambayo mvua haina uhakika, tusifanye hivyo. Kwenye mikoa ambayo mvua haina uhakika tupeleke mazao ambayo yanavumilia ukame, mbolea, matunzo na shughuli zote za kilimo cha mazao ya chakula tukipele kule kwenye maeneo ambayo yanaweza kutuzalishia mazao kwa wingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo pendekezo langu hilo la kwanza tuangalie mikoa ile ambayo ina uzalishaji mzuri, tuipeleke uzalishaji ili kuhakikisha ghala ya chakula linapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tumezungumza kwenye bajeti hii juu ya suala zima la kupunguza asilimia tano za

mazao ya mkulima mpaka asilimia tatu au mbili, lakini tumeweka vilevile kwamba usafirishaji wa mazao kutoka Wilaya moja kwenda Halmashauri nyingine yanayozidi tani moja tuweze kuya-charge. Nashauri kwamba kwa vile tumeshatoa punguzo na tayari wakulima wanakwenda kulipa asilimia tatu au mbili kwenye eneo ambalo wamezalishia basi hii tozo ya tani zaidi ya moja tuifute, tuifute ili mazao yasafiri bure, asilimia watakazolipa za CESS kwenye eneo ambalo wamezalisha iwe imetosheleza kulipa gharama zote za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwangu Songea ni wakulima. Tuko Songea Mjini lakini hatuwezi kulima mjini kwa mujibu wa Sheria za Mjini, kwa hiyo wakulima wa Songea Mjini wanakwenda kulima maeneo ya Halmashauri za karibu. Wanakwenda kulima Madaba, Namtumbo na Peramiho. Akishalima anatakiwa kutoa mazao yake kuyasafirisha kurudisha mjini. Sasa ukimtaka huyu alipe mara mbili atalipa CESS asilimia tatu, wakati huo huo atalipa na tani zaidi ya moja anayoisafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiri ili tuweze kumfanya mkulima huyu apate faida kutokana na kilimo chake, basi tum-charge mara moja na kwamba aweze kusafirisha mazao kwenda Halmashauri yoyote. Napendekeza pendekezo hili lifanywe kwa mazao yote ndani ya nchi. Mtu akiwa na mahindi anataka kuyaondoa Songea kwenda kuyauza Shinyanga, aruhusiwe kupita na mahindi hayo mpaka Shinyanga, anatoka Tabora anakwenda Kigoma aruhusiwe kwenda mpaka Kigoma bila kulipa gharama yoyote zaidi ya ile asilimia ya CESS ambayo tumeiweka. Itawasaidia sana wakulima wetu kuwapa moyo katika shughuli za uzalishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka nizungumze katika bajeti hii, Mkoa wa Ruvuma ni Mkoa ambao bahati mbaya sana sio mkoa wenye viwanda. Ukienda pale Songea Mjini hakuna kiwanda chochote ukiacha kiwanda kilichoko Mbinga cha Kahawa na Kiwanda

kilichoko Tunduru cha Korosho, lakini Songea Mjini hakuna kiwanda chochote. Kwa hiyo maana yake mzunguko wa fedha ni mdogo sana kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara mwezi Januari mwaka jana kule Songea na alipofanya ziara alitembelea kiwanda cha Ngomati, kiwanda cha tumbaku. Kile kiwanda kimekufa katika mazingira ya ajabu sana, hebu tuangalie; Waziri Mkuu alisema angalieni mazingira haya ili muone namna gani tunaweza kukifufua kile kiwanda. Kwa sababu kuna tatizo kubwa la tumbaku kwa sasa kama kiwanda kile hakiwezekani kuzalishwa kwa ajili ya kuzalisha tumbaku, basi tufanye utaratibu wowote wa kupata kiwanda ambacho kitakuwa mbadala wake, maana mashine zipo, mitambo ipo, kiwanda kipo lakini kimekufa katika mazingira ya ajabu kidogo na hivyo mzunguko wa pesa ni mdogo sana kwa sababu hakuna ajira Songea Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna utaratibu ambao tumekubaliana na Serikali wa kutafuta eneo la EPZA ambalo bado halijakamilika. Naomba katika bajeti hii tukamilishe eneo la EPZA kwa ajili ya kutafuta wawekezaji ili waje kuwekeza viwanda Songea Mjini. Hii itasaidia sana kuweza kuinua uchumi na kusaidia ajira kwa wananchi wa Songea na Mkoa mzima wa Ruvuma kwa ujumla. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweke kipaumbele kwanza suala hili la kufufua kiwanda cha Ngomati lakini la pili ni hili la kufungua EPZA, ukanda wa viwanda ambao bahati nzuri Serikali imeshaamua, imetafuta eneo lipo pale, watu hawajalipa tumalize tatizo la kulipwa ili watu waje kuwekeza pale Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kabisa viwanda vitasaidia sana hali ya uchumi ya wananchi wa Songea. Sisi tuko pembezoni sana, hatuna viwanda, hatuna shughuli zote zaidi ya kilimo, hakuna shughuli zozote za kiuzalishaji. Kwa hiyo, tukifanya hivi tutasaidia wananchi wa Songea ili wapate ajira waweze kupata uzalishaji huo utakaosaidia maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna tatizo kubwa sana la suala la makaa ya mawe Ngaka kule Mbinga. Tuna makaa ya mawe lakini usafirishaji wa makaa yale ya mawe ni mgumu sana, unafikia mahali unaharibu barabara zetu unaharibu mazingira. Tunaomba tuone uwezekano wa kupata reli, reli ile ambayo ingejengwa kati ya Mbamba bay na Mtwara naomba iharakishwe kwenye mpango ili iingie kwenye mpango wa maendeleo ili iweze kutengenezwa reli. Reli ile itasaidia sana... (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Sakaya ajiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti hii. Kwanza nianze kwa maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanapoenda kuchagua viongozi na wanapoenda kupiga kura ya kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanamchagua mtu ambaye wanamkabidhi dhamana juu ya usalama wao, uhai wao, usimamizi wa rasilimali zao. Huyu anakuwa *custodian* wa *resources* zao ambazo wamekuwa nazo walizopewa na Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameunda Tume mbili na ametusomea *findings* za Tume zake, lakini huko nyuma Marais nao waliunda Tume mbalimbali. Nataka nitumie Bunge hili kuwaambia Waheshimiwa Wabunge wenzangu, vita ya kupambania rasilimali ya nchi hii siyo vita ya John Pombe Magufuli, vita hii ni vita ya Watanzania wote. Naamini kwamba *there is no wrong doing in doing right thing*, hakuna kufanya makosa katika kufanya jambo jema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana baada ya kuchangia

kaka yangu Mheshimiwa Tundu Lissu mimi nilimfuata kwa heshima kabisa ili anipatie maandiko yake. Mpaka saa tisa usiku jana nimekuwa nasoma baadhi ya maandiko yake. Ukisoma ripoti ya Bomani, ukisoma *writing* alizoandika kaka yangu Mheshimiwa Tundu Lissu na mkononi hapa ninayo kesi ambayo yeye aliisimamia ya mwaka 2006, *this country* imebiwa raslimali zake kwa muda mrefu. Nataka niombe Bunge hili, *let's not be hostage of the history*. Bunge hili limefanya makosa, viongozi wetu huko nyuma wamefanya makosa, leo tumepata mtu anayetu-*lead* kwenda kupambania haki zetu *let us join hands with him*. Tumnyooshee mkono akishindwa kutufikisha mwisho wa vita hii, *not now!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Nzega, katika kesi hii kaka yangu Mheshimiwa Tundu Lissu anawafahamu akina Mzee Jumbe Kumega, anamfahamu Mama Fatuma Mhina wa Isungangwanda amewa-*cite*, *these are victims*. Leo kama Mbunge wa Jimbo la Nzega Mjini ndugu yangu Mheshimiwa Kigwangalla alipigwa mabomu kwa ajili ya *Resolute*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeibiwa na kama alivyosema Mheshimiwa Heche jana na mimi nataka niseme leo, *Resolute* ameondoka na fedha za Halmashauri ya Nzega *ten billion shillings* za *service levy*. Jambo la kusikitisha Serikali imeipa kampuni tanzu ya *resolute* leseni ya kupewa maeneo ndani ya Jimbo la Nzega, *Wallah wabillah watallah*, kama hamtafuta leseni ya Mwabangu *Miners*, mimi nitaongoza wananchi *I will not care the outcome!* (Makofi)

Mheshimiwa Menyekiti, pili, namwomba Mheshimiwa Mpango, yeye ni Waziri wa Fedha, *Resolute* wana mgogoro na *TRA* juu ya kodi! Kuna *ten billion* yetu kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Kalemuni anajua. Nataka kwenye *wind up* waniambie *ten billion* ya Halmashauri ya Nzega inapatikanaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amesema nasi lazima tumuunge mkono na katika hili la *Resolute* nitamuunga

mkono kwa jitihada zangu zote. Asiponijibu Mheshimiwa Kalemani, kile chuo walichofungua cha madini naenda kuwaambia wananchi wagawane yale mabati, *that is all we can get* wananchi wa Nzega. Tumeachiwa mahandaki yenye urefu wa zaidi ya mita 1,000, tunaambiwa yatajaa maji baada ya miaka 200 *we will not allow this*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme Rais amekuwa mstaarabu sana, angetangaza kufunga hii migodi, leo kuna *Diamond Williamson*, walichokifanya *Diamond Williamson* pembeni kuna uchimbaji unaendelea wa kampuni nyingine ya Hilal, yule Hilal kapewa kazi ya ulinzi wa migodi ya *Diamond*, wanachukua almasi kutoka kwenye mgodi wa Mwadui wanaenda ku-*process* kwenye mgodi wa Hilal zinaondoka kwa njia za panya, *this has been the game for years, this business has to stop!* Lazima tumuunge mkono Rais katika hili, tuje tumnyooshee mkono akishindwa kutufikisha mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye hoja ya kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango, sina mgogoro mkubwa na yeye *this time*, namuunga mkono nina mambo machache ya kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri kwenye hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango; kwenye *page* namba 50 ametaja sheria anazokuja kutuletea kwa ajili ya kuzifanyia mabadiliko. Sheria ya kwanza ni Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148. Hapa tunaona dhamira ya Serikali ya ku-*link industrialization* na *fiscal measures* za nchi. Serikali inafuta *VAT on capital goods* ni jambo zuri, namwomba Mheshimiwa Waziri a-*extend* hii iwe ni *capital goods with processing chemicals*, kwa sababu *chemicals* ambazo tutakuwa tuna-*import* kwa ajili ya ku-*process* kwenye viwanda bado zitakuwa na *import duty tax*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tunapofuta kodi ya ongezeko la thamani kwenye *capital equipment* tufute na kodi zinazoendana na *chemical goods* ambazo zitatumika katika viwanda vifuatavyo: Viwanda vinavyohusika na

mazao ya kilimo hasa ya nguo, kwa maana ya viwanda vya *cotton* vinavyo-*process* nguo ili tu-*link* na mpango wa Serikali wa *cotton to clothes (C to C)* ambao umeandikwa na Serikali. Hilo ni jambo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tufute kodi ya *import duty* kwenye *chemicals* zinazotumika ku-*process leather industry*. Nchi yetu ni ya pili kwa mifugo, itakuwa *it is not helping* kama hatutaweza ku-*take* hii *advantage*, kwa sababu asilimia 65 ya watu wetu wako kwenye sekta ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya pili ambayo nataka nishauri ni kodi ya mapato. Tumepunguza kutoka asilimia 30 kwenda asilimia 10 ya *corporate tax*, lakini maeneo gani? Ni *assemblies* ya matrekta na magari. Namwomba Mheshimiwa Waziri, tu-*extend* hii *docket*, tutatoa hii *fiscal incentive* ya asilimia 10 ya *corporate tax* kwenye viwanda vyote ambavyo vitawekeza kwenye korosho, vitawekeza kenye mazao ya kilimo kwa maana ya kwamba *cotton*, korosho, kahawa kwa sababu leo korosho yetu yote inakuwa *exported raw* kwenda India. Hii haitusaidii, maana yake ajira zinakwenda nje. Kwa hiyo, naomba *docket* hii iongezwe zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kwenye *VAT*, leo mkulima wa alizeti akizalisha alizeti, akisindika tu anakutana na *VAT*. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, ili tuweze ku-*gain advantage* ya kukua kwa viwanda, iweze kuchukua watu wengi, mazao ya kilimo yanayosindikwa ndani tufute kodi ya *VAT* katika mazao haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 20, wenzangu wameongelea sana suala la *CESS*. Mheshimiwa Waziri nataka niwaombe kuna kodi inaitwa *services levy* ya asilimia 0.03 ya *gross income*. Kodi hii inakwenda kinyume na *principle of taxations*, kwa sababu tunachaji kodi kwenye mtaji, sheria hii ilifanyiwa mabadiliko mwaka 2012 Sura ya 6, tukasema kila Mtanzania mwenye leseni pato lake la mwaka (*Gross income*) linachajiwa asilimia



0.03, kwanza ina-*attract double taxation* kwa sababu *service levy* hii inachajiwa kule juu lakini kwa mzalishaji, vilevile na muuzaji wa Nzega anachajiwa. Tufanye nini? Tuweke *dermacation*, tutengeneze *levels*, kwamba *service levy* ichajiwe 0.01 kwa wafanyabiashara wadogo wenye leseni, *corporate* wabaki wachajiwe 0.03. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sheria hii tumei-*impose* asilimia 10 kwenye *crude oil*. Najua kuna *a lot of politics* kwenye suala la mafuta ghafi, lakini ukisoma ripoti ya *BOT* ya mwezi Aprili *re-exportation* imeshuka. Nchi za jirani wenzetu wamefuta! Matokeo yake sisi tunakuwa soko la mafuta kutoka Kenya na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, udhaifu wa taasisi zetu za kusimamia shughuli wanazowapa usiathiri uzalishaji, kwa sababu sasa hivi ni kwamba kuna udhaifu inawekwa kodi ili ku-*discourage* kama walivyofanya kwenye sukari za viwanda. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba dakika moja kama muda wangu umekwisha. Naomba niongelee kodi ya *railway development*...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, muone baadaye Waziri tunakwenda kikanuni.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sakaya, jiandae Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hakuna Mtanzania yeyote mwenye akili timamu, mpenda maendeleo ya Taifa lake, anayependa Taifa hili, anayeweza kupuuza juhudi zinazofanywa kwa ajili ya kusaidia kuokoa rasilimali za Tanzania, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Bunge hili wapo Wabunge ambao wana miaka 30, wengine 25, wengine tuna miaka 10. Kilio chetu, miaka yote ndani ya Bunge hili ni juu ya sekta ya madini kugeuzwa kuwa shamba la bibi miaka yote. Kwa miaka yote sekta hii imekuwa hainufaishi Taifa, tumekuwa tunaomba mikataba ije ndani ya Bunge hili miaka yote. Tumekuwa tunapewa majibu na Serikali ilizopita kwamba mikataba ya sekta ya madini ni siri kali. Tulikuwa tunauliza hii siri anafichwa nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia sekta hii na namna ambavyo Watanzania hata wale wanaozunguka maeneo ya madini wanavyonyanyasika, wanavyoumia hawana maji, barabara zinabomolewa hawatengenezewi ni suala la uchungu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, yale ambayo tuliyokuwa tunayaomba miaka yote hayafanyiwi kazi, nikiona leo anatokeza mtu, Rais anaweza kuyafanyia kazi angalau kwa hatua za mwisho, mimi binafsi napongeza, napongeza juhudi yoyote kuhakikisha kwamba rasilimali ya Watanzania inanufaisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba maamuzi yote, mapendekezo yote likiwepo la kuleta mikataba Bungeni ije haraka Wabunge tuiptie sisi ni wawakilishi. Unapoingia kwenye nyumba yako hata kwa maisha ya kawaida, ukikutana na changamoto huwezi kutatua zote kwa wakati mmoja unakwenda *step by step*. Kwa hiyo, tumeanza na hili hapa, ije mikataba yote tatizo kubwa ni kwenye mikataba ndiko tunapopigwa madini, mchanga wa makinikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia hatua kuna

mikataba ya madini imekwenda kuingiwa Ulaya, Karamagi hapa alipeleka mkataba Uingereza kwenda kusaini, una mbuzi wako baada ya kuita mnunuzi ndani ya nchi yako unambeba unampeleka kwenda kumuuzia nje ya nchi ulifanyika ufisadi. Kila aliyeweka kidole chake kiwe ni kidole kidogo, kikubwa chochote lazima ashughulikiwe vizuri ihakikishwe kwamba adhabu inatolewa ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hotuba ya Waziri kuendelea kushuka kwa shilingi ya Tanzania. Katika hotuba ya Waziri tumeona kwamba shilingi ya Tanzania inaendelea kushuka na tumekuwa tunazungumza hapa Bungeni hatuoni mikakati kama Taifa, hakuna mikakati ya kuweza kudhibiti kuporomoka kwa shilingi ya Tanzania na kuporomoka kwa shilingi yetu kunasababisha mambo mengi yanakwenda vibaya, kunasababisha kupanda kwa vyakula na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashangaa ni Tanzania pekee ambapo dola ya Marekani inauzwa kama njugu mitaani, ni Tanzania pekee ambapo *Bureau de Change*, vioski vya kubadilisha fedha vipo kila kona kama vioski vya soda. Tanzania pekee unaweza kuona kwamba bidhaa zinanunuliwa kwa fedha ya nje, nendeni nchi nyingine hata hapa Kenya huwezi kutumia shilingi ya Tanzania kununua kitu Kenya huwezi! Tumejisahau kama Taifa na kwa kweli hapa nasema, Gavana wa Benki Kuu ameshindwa kabisa kusimamia kuporomoka kwa shilingi ya Tanzania, kabisa nasema kila siku, ni kwa nini tunashindwa kusimamia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tunataka mikakati sio kila siku bajeti tunasema kwamba shilingi inaporomoka, tuilinde shilingi yetu tusikubali fedha za nje ije *i- overhaul shilingi* ya Tanzania. Tunaomba sana shilingi yetu iendeleo kupanda ipande kwa sababu inazidi kushuka matokeo yake kama Taifa kiuchumi inaathiri uchumi pia inaathiri maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya uchumi, nimesoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri cha hali ya uchumi

wa Taifa, ukiangalia mazao mengi ambapo yalikuwa yanaingizia pato kubwa kwa Taifa hii, *page* 49, mazao mengi yamepungua sana kusafirishwa nje, tukianza na kahawa, kuna *cocoa* kuna mazao mengi kuna katani, kuna pamba. Kutokusafirisha mazao mengi ina maana uchumi wetu unazidi kwenda chini, kwa nini tunashindwa kusafirisha mazao kwa sababu tumepunguza mapato, mazao yapo kidogo ndani ya nchi yetu kwa sababu hatujaweza kuwekeza vizuri kwenye kilimo hiyo ni ishara tosha, kupungua kusafirisha mazao nje hatuwekezi vizuri na kama hatusafirishi sisi tunakuwa ni masoko kuonyesha kwamba tunauza vitu vya wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kama Taifa tuweze kuinua sekta ya kilimo hakuna namna nyingine. Tuiue sekta ya kilimo tuhakikishe kwamba mazao yote ambayo ukisikia leo Mkoa wa Kilimajaro umeendelea ilikuwa ni kahawa, leo Kagera Bukoba ni kahawa, ndizi, ukisikia Mbeya wameendelea ilikuwa ni *cocoa*, tumeyasahau yale mazao tumeyaacha. Leo mkulima wa kahawa anang'oa kahawa kwa sababu pembejeo ni ghali hawezi kununua, Serikali haiangalii, kwa hiyo hatuwezi kuinua kilimo kama tunashindwa kuhakikisha kwamba pembejeo zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amesema amebadilisha mifumo kwa ajili ya kutoa pembejeo, tulikuwa tunatumia mfumo wa *voucher* ukawa ni hasara kubwa wakulima hawanufaiki. Tukaja na mfumo mwingine Serikali ikasema itaunda vikundi *then* itoe dhamana benki vikundi vikakope benki, mfumo ule haukutekelezwa, matokeo yake mwaka uliopita mpaka ndani ya Wilaya yangu Kaliua watu hawakupata pembejeo kwa sababu Serikali haikupeleka pembejeo na waliopewa kusambaza pembejeo hawakupeleka kwa wakati. Kwa hiyo, lazima kama Taifa tuwe na mfumo ambao ni endelevu na ni wa uhakika kuhakisha kwamba wakulima wetu wanapata pembejeo kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta nyingine ni sekta ya mifugo, Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kuwa na mifugo mingi,

lakini kwa bahati mbaya sana mifugo yetu hatujaweza kuitumia vizuri kuongeza kipato cha Taifa. Leo wafugaji wamekuwa wanatangatanga hapa na pale, mifugo imeaachwa inazagaa karibu nchi nzima, hakuna maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya wafugaji, hakuna malisho, hakuna viwanda, hakuna kuchakata mazao yao, hatujaweza kutumia sekta ya mifugo vizuri. Nilitegemea bajeti kama ya leo Waziri angekuwa anatuambia mifugo yenyewe inaingiza zaidi ya robo *percent* kwa sababu tunayo mifugo mingi inakufa tu, wakati wa ukame inateketea yote kwa sababu hatujaweza kujizatiti vizuri kwenye mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunazo ranchi za Taifa, ranchi zile Serikali haiwekezi chochote, ranchi zimekuwa ni mapori majengo yale yanaharibika, tunaiomba Serikali kama wameshindwa kuwekeza kwenye ranchi za Taifa wayagawe yale maeneo wawape wafugaji, waweze kufungua ranchi zao kule wafuge kisasa Serikali inufaike. Kuacha yale maeneo yanateketea wakati wafugaji wanasambaa nchi nzima, siyo sahihi na wala hatuangalii uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Serikali kubana matumizi au udhibiti wa upotevu wa fedha za Serikali. Serikali imesema huku nyuma kwamba itahakikisha samani zote za Serikali za ofisini, samani zote za ofisi za Serikali kuanzia Serikali Kuu mpaka *Local Government* wanunua samani kutoka ndani ya nchi. Pia tumeambiwa huko nyuma kwamba watanunua magari ya bei ya kawaida sio mashangingi lakini leo yote hayo hayafanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atuelekeze ni kwa nini Tanzania hii tuna mbao nzuri, tuna vijana wenye uwezo, tuna viwanda vidogo vidogo wanazalisha samani, Serikali inanunua samani za Kichina ambazo ni *low quality* ni *expensive* na hazina ubora, wakati huo tuna viwanda vidogo vidogo ndani ya nchi yetu wanashindwa kununua. Tunao Magereza, tunao JKT, tunao vijana wote wana *capacity* nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri aje atuambie ni lini Serikali itaacha utaratibu wa kuagiza fanicha/samani kutoka nje ya nchi za Kichina na kuhakikisha kwamba zote zinanunuliwa ndani ya nchi yetu, ili tuweze kutoa ajira kwa vijana lakini pia tuweze kulinda viwanda vya ndani vidogovidogo na hivyo kuweza kuinua uchumi wetu ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya utalii, tunayo rasilimali nyingi sana tuna vivutio vizuri ndani ya nchi yetu, tatizo kubwa hatuwekezi vya kutosha. Ukiangalia hapa *Ruaha National Park* ni *National Park* kubwa kuliko nyingine zote Afrika, lakini *National Park* ile barabara ya kutoka Iringa tu kwenda Ruaha Serikali zaidi ya miaka 15 mmeshindwa. Matokeo yake watalii hawaendi kule. Hebu tuhakikishe tunawekeza kwenye utalii tunavyo vivutio vizuri, leo sio watu wa kushindwa na Kenya, inatushinda kwa ajili ya kipato cha utalii kwa sababu hatuwekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuvuna pasipo kupanda, lazima tupande tuweze kuvuna. Kwa hiyo, naiomba Serikali tuwekeze vizuri kwenye sekta ya utalii, tuweze kuvuna vizuri kwenye utalii. Nina imani kabisa kwamba kwa vivutio vyetu vilivyo vizuri kuliko nchi zote za Afrika tunaweza tukaingiza kipato kikubwa na hivyo kuongeza uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi, sijaona hotuba ya Mheshimiwa Waziri namna gani ya kuweza kudhibiti au kupambana na mabadiliko ya tabianchi ndani ya nchi yetu. *Climate change* ni suala la Kitaifa, nchi zote duniani wamejiwekea mikakati kwenye nchi zao kwa njia namna gani ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi, leo ndani yetu tunaona jinsi gani tutapata madhara makubwa kwa mabadiliko ya tabianchi, tumeona tetemeko kule Kagera limeua watu, mafuriko kila siku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Conchesta, wajiandae Mheshimiwa Juliana Shonza na Mheshimiwa Augustino Masele.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi kidogo nami niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mawazo yangu napenda nichukue nafasi hii kwanza kuunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani, pia napenda tu kuwashukuru Viongozi wetu wa kambi, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Riziki S. Mngwali pamoja na James Francis Mbatia kwa kazi nzuri wanayoifanya na niwaambie kwamba kufanya kazi ya upinzani katika nchi zetu za Kiafrika inataka moyo. Kwa hiyo, tuendelee tu kupambana na matokeo ya kazi yetu yanaendelea kuonekana na kuleta mabadiliko katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza maji katika bajeti hii, nikiamini kabisa kwamba tumekaa hapa takribani miezi miwili, tukifanya mipango na kutafsiri mipango hii katika pesa ndiyo maana ya bajeti, tunapanga halafu tuna tafsiri mipango katika pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunahitaji kuona mafungu tunayoyagawa yanaleta matokeo mazuri, kwa vikundi vya wananchi na mwananchi mmoja mmoja na tunapima matokeo haya tunaona bajeti yetu tuliyoipanga imeleta matokeo yapi, imeweza kuleta maendeleo ya nchi na watu wake imeweza kupeleka mbele maendeleo ya mtu mmoja mmoja katika makundi yao na baadaye tunarudi mwaka kesho tunakuja kushangilia na kupiga makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiria kwamba hii bajeti

inapaswa kujibu matatizo ya maji, kwa sababu tulikaa hapa na hasa wanawake, tulipanga mkakati mzuri na tukafanya *lobbying*, Wanaume wakatusaidia tukasema Serikali iongeze tozo ya Sh.50/= kwenye mafuta iende kwenye maji ili tuweze kuwatua wanawake ndoo, lakini cha kushangaza Serikali imekataa maombi yetu. Kwa lugha nyingine Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi isitudanganye haipo tayari kuwatua wanawake ndoo, badala yake mmetuletea sasa hoja nyingine ya Sh.40/= ambazo wanasema zitaongezwa kwenye mafuta baada ya kufuta *road license*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejiuliza Mheshimiwa katika kitabu cha bajeti cha Waziri mbona hajatuonesha hii Sh.40/= kama inakwenda kwenye maji? Hii Serikali inaelewa vizuri mafuta yanayoingia nchini kwa sababu wanaagiza mafuta kwa *bulk procurement*, kama wanafanya hivyo wanajua ni lita ngapi, kwa hiyo mngeweza kukokotoa kutueleza ni fedha kiasi gani zitapatikana, hakuna jambo kama hilo katika vitabu vyao. Sasa tunakaa hapa tunaanza kupigwa wananchi kiini macho kwamba unajua hiyo Sh.40/= itakwenda kwenye maji, wapi na wapi watuoneshe mahali ambapo mmeandikwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atuonyeshe ni shilingi ngapi ambazo zitatokana na mafuta hayo. Wanajua kwa nini wameshindwa kufanya *calculation* ni kwa sababu walikuwa hawakuipanga kwenye bajeti hata kidogo ni wazo limeletwaletwa tu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani kwamba hii Sh.40/= haziwezi kupandisha maisha ya watu. Nilikuwa nafanya *simple calculation*, kwa basi ambalo linatoka Dodoma kwenda Mwanza, mtu tu ambaye anaweza kutumia lita 200 analipa *road license* zaidi milioni mbili, kwa hiyo na wao watufanyie mahesabu tuone haya mafuta ambayo wanaagiza kwa *bulk procurement* yanaleta pesa kiasi gani ambazo wanasema zitakwenda kwenye mafuta, *otherwise* wanachofanya wanajaribu kutetea hii hoja, wakijua wanafanya siasa, sawa tunafanya siasa hapa, lakini



wasifanye siasa za kwenda kudanganya au kuwaweka sawa au kuwaweka vibaya wananchi wa chini na hasa akinamama wanaotumia vibatari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa kwenye Halmashauri, siwezi kuchangia bila kugusa Halmashauri. Bajeti ijibu matatizo ya wananchi, tukienda kwenye Halmashauri tunatazama pesa za barabara ambazo zinatolewa na Serikali Kuu katika Mfuko wa Barabara, ukienda kwenye kitabu cha ujenzi ukurasa wa 172 kinaonesha kwamba wao mwaka huu watakusanya bilioni 832.4. TAMISEMI wanapewa pesa bilioni 249.7, pesa hizo siyo kwamba zinakwenda zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona bajeti ya mwaka huu Serikali imeweza kutoa fedha za maendeleo asilimia 38, kwa hiyo tunaona ni namna gani Serikali ilivyoshindwa kabisa hata kufika asilimia 50. Kama pesa hizi zinakuwa ndogo na mara nyingi tumekuwa tukiwaambia kwamba waongeze pesa katika Halmashauri ili Halmashauri ziweze kutengeneza barabara na barabara hizi zikipitika ni njia ya kusaidia wananchi kuweza kusafirisha mazao yao lakini pia kusaidia wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemwona Mheshimiwa Waziri Umy hapa anahangaika kutafuta *ambulance*, hizo *ambulance* zinakwenda kupita barabara gani, kama Halmashauri barabara zake hazitengenezwi? Kuna mtu ameuliza hapa kwamba inawezekana Serikali Kuu wana mpango wa kutoa huduma wenyewe badala ya Halmashauri ndiyo maana wanachukua vyanzo vyote. Wanachukua vyanzo vyote vya Halmashauri Je, ninyi wana mpango ngani mbadala wa kutoa huduma kwa Halmashauri hizi. Nina wasiwasi mkubwa haya mambo yote tunayoyapanga yatakwenda kushindwa kutoa majibu sahihi na kusaidia wananchi ili waweze kuinua maisha yao kuleta maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama barabara hazitengenezwi za Halmashauri, Serikali Kuu watakwenda

kuona mashimo yaliyomo kwenye mitaa? Wanaweza wao wenyewe kukaa Dar es Salaam pale au kukaa Dodoma hapa wakajua mimi kwetu kule Kamachumu Makongola Kijijini kwangu nilikozaliwa kwamba kuna barabara mbaya, hamna barabara ni mbaya za Halmashauri hazitengenezeki, hakuna mahali pa kupitisha mazao, wananchi wanahangaika lakini bado Serikali inatoa pesa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kutamka kuhusu *percentage* ya pesa ambazo zinakwenda Halmashauri kwenye Mfuko wa Barabara, Serikali inakaa kimya Mawaziri wanakaa kimya, ni kwa nini hawaleti sheria, wasilete Sheria za Madini tu na hizi wazilete tuzibadili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo niongelee kuhusu madini na mikataba, watu wengi wanasema mchawi mpe sifa yake, mimi namshukuru sana Mheshimiwa Bashe amesema mtu akifanya kitu kizuri asifiwe wakati mwingine kwa kitu kizuri, kama wanavyosema tumuunge mkono Rais wetu, mimi nafikiri wazo siyo baya, pia hata Mheshimiwa Lissu amefanya kazi kubwa sana kuhusu mambo haya ya mikataba, amesimamia kesi mbalimbali. Kwa hiyo siamini kama kuna mtu ambaye anaweza kushindwa kutambua kazi ya Mheshimiwa Lissu ambayo ameifanya tangu mwaka 2004 mpaka leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema walete sheria na wakubali tumewaambia kwamba hakuna sababu ya kupigiana makofi, kufanya kosa kitu kibaya ni kulirudia, kama CCM walitufikisha hapa kwa miaka 50, basi wawaombe radhi Watanzania na wakubali tusahihishane humu ndani. Waende walete sheria maana yake hata Ndugu Ludovick Uttoh, aliyekuwa CAG amewaambia kwamba nchi iliingia kwenye mikataba ya kipumbavu, siyo maneno yangu yako kwenye magazeti, alisema tulipitisha sheria ambazo zinaruhusu madini na kila kitu kiende. Kwa hiyo, waende walete sheria, hata tukiongea maneno ya namna gani hapa, kama hakuna sheria wale jamaa wataendelea kubeba mabonge ya dhahabu kwa asilimia 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani Waziri ambaye anaweza kwenda kwenye uwanja wa ndege hapa? Nenda kwenye machimbo, kwenye uwanja wa ndege hakuna anayekanyaga pale hata Waziri wa Fedha hakanyagi, hata wewe Mwenyekiti wa Bunge leo hukanyagi mle, ni sheria tuliziunda zinatupeleka. Waletе sheria hapa tubadili ili tuweze kwenda na jambo hili vizuri kwa sababu ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba ni kwamba tuhakikishe bajeti hii inajibu matatizo ya Watanzania, inaangalia kilimo kwa mfano, hebu tuangalie kilimo kwa undani, wameanzisha mashamba darasa hayafanyi kazi, mimi ninapoishi nyumbani kwangu kijijini natazana hivi na shamba darasa hamna kitu, kwa sababu hakuna *Extention Officers* hawatuoneshi katika bajeti kwamba wanaenda kuajiri *Extention Officers* hawatuambii wanakwenda kufanya mikakati ipi kwa ajili ya kilimo ili wananchi waweze kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wangekubali *issue* yetu ile ya Sh.50/= wangeweza kutuambia tutapata pesa kiasi gani, tutajenga malambo, tutajenga mabwawa, tutafanya umwagiliaji *and then* wananchi watalima, tutapata chakula lakini hata lishe, hatuwezi kuongea ya lishe wakati watu hawashibi, watu hawana chakula na utegemee watu wafanye kazi wakati watu wana njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shonza, ajiandae Mheshimiwa Augustino Masele.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Mpango. Vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Mpango kwa hotuba nzuri

ambayo ameiwasilisha hususani kwa kuweza kugusia vipengele muhimu, kuainisha vipengele ambavyo ni vya kipaumbele kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimevutiwa sana na kipengele cha kuainisha kwamba moja ya vipengele vya msingi ni Mchuchuma pamoja na Liganga. Hii itakuwa ni mkombozi lakini nimwombe sana Mheshimiwa Mpango aweze kuangalia anavyoenda kushughulikia hivi vipengele vya msingi aangalie sana kwa yale maeneo ambayo yanazalisha makaa ya mawe (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia kwa Mkoa wangu wa Songwe, katika Wilaya ya Ileje kuna makaa ya mawe, vilevile ukienda kwenye Wilaya ya Mbozi Magamba kuna makaa ya mawe. Nichukue nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Mpango aviunganishe pamoja haya maeneo katika mpango huu mkubwa wa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuweza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwa Taifa letu. Sote ni mashahidi tumeshuhudia namna ambavyo Rais anapambana kuhakikisha kwamba anasimamia rasilimali za Mtanzania likiwepo suala la madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashangaa sana watu ambao wanaibuka katika Bunge hili kuponda jitihada kubwa ambazo Mheshimiwa Rais anazifanya. Jana nimemsikiliza kwa umakini sana Mheshimiwa Msigwa, ameuliza kwamba eti Mheshimiwa Pombe Magufuli alikuwa wapi miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kama ambavyo Watanzania huko nje sasa hivi wameungana na Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba wanamtia moyo katika vita hii kubwa ambayo ameianzisha, nilijua kabisa kwamba hata humu ndani Bungeni tutaungana wote kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunamtia moyo Mheshimiwa Rais, lakini wenzetu wanauliza kwamba alikuwa wapi. Sasa kwa sababu yeye ameamua kufukua makaburi na mimi naomba nimsaidie kufukua makaburi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya huko nyuma, ukifuatilia historia ya nchi hii, wakati Mwalimu Nyerere akiwa Rais, Mzee wangu Ndugu Mtei alikuwa ni Waziri wa Fedha na hilo wenzangu wanalijua vizuri sana na tutakumbuka kwamba ni Ndugu Mtei huyu ambaye alimshawishi Mwalimu Nyerere kwamba akubaliane na masharti magumu ambayo walitupa mabeberu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sharti mojawapo ikiwa ni kwamba kuweza kushusha thamani ya fedha yetu, lakini Mheshimiwa Nyerere alikataa na alipokataa tunaona kabisa Mzee wangu Mtei alijiuzulu na akahama nchi akaenda kufanya kazi *World Bank* kwa wale wale mabeberu ambao alikuwa anawatetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo siyo jambo jipya kushuhudia hawa wenzetu wakiendelea kutetea mabeberu ndani ya Bunge hili, kwa sababu hata Muasisi wao ni kitu ambacho alishakianzisha tangia huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi wanavyouliza kwamba Mheshimiwa Magufuli alikuwa wapi? Wakati Mwinyi akiwa Rais Mheshimiwa Lowassa pamoja na Mheshimiwa Sumaye walikuwa ni Mawaziri, kweli siyo kweli? Sasa na kipindi hicho Magufuli hakuwa Waziri. Sasa unapouliza Mheshimiwa Magufuli alikuwa wapi, naomba waanze kuwauliza ambao wanao huko Mheshimiwa Lowassa pamoja na Mheshimiwa Sumaye walikuwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, Mheshimiwa Mkapa akiwa Rais wa nchi hii Sumaye alipanda cheo akawa Waziri Mkuu kwa maana ndiye Kiongozi wa shughuli zote za Serikali ikiwemo suala la mikataba ya madini. Sasa leo hii wanauliza kwamba eti Magufuli alikuwa wapi, kaka yangu Msigwa amenisikitisha sana. Hata kwenye Serikali ya Jakaya Mtendaji Mkuu wa Serikali Mkuu wa Serikali alikuwa ni Mheshimiwa Lowassa na mikataba yote ambayo ilikuwa ikisainiwa katika Bunge hili yeye alikuwa anahusika na sote tunafahamu alishirikiana na Karamagi kwenda nje wakaenda wakasaini mkataba ambao leo hii umeliingiza

Taifa letu katika matatizo makubwa. Sasa mtu anapohoji kwamba eti Magufuli alikuwa wapi, naomba kabisa kwamba aanze kumuuliza Mheshimiwa Lowassa pamoja na Mheshimiwa Sumaye walikuwa wapi? Kwa sababu wao kipindi hicho ndio walikuwa Watendaji Wakuu wa shughuli zote za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja, inapokuja vita kama hii ni vizuri kama Taifa tukaungana wote kwa pamoja kumsema na kumshauri Rais wetu. Kaka yangu Mheshimiwa Lissu unapoanza kutaja watu kwamba Mheshimiwa Jakaya alihusika kusaini, unasahau kabisa kwamba Jakaya akiwa Waziri wa Maji Sumaye alikuwa Waziri Mkuu. Sasa nashangaa jana umemtaja Jakaya lakini Sumaye vipi ulimsahau? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inaonesha kabisa kwamba hawa watu ni watu ambao wanafanya vitu kwa *double standard*, ni watu ambao hawajielewi na sasa hivi Magufuli amewashika pabaya, walizoea kufanya siasa za matukio, siasa za matukio sasa hivi hamna. Walizoea mtoke humu Bungeni wakafanye maandamano, sasa hivi wananchi wanakipenda sana Chama cha Mapinduzi na ndio maana wanavyoona Rais anafanya kazi nzuri wanageuka wanasema Rais hatekelezi Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie masuala ya madini yapo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ukisoma ukurasa wa 28 imezungumzia kwamba Serikali hii itaenda kusimamia kuhakikisha kwamba suala la madini linawanufaisha Watanzania wote wakiwepo Watanzania ambao ni maskini. Sasa mtu anapokuja kusema kwamba haipo kwenye ilani anajitahidi baada kuona kwamba Serikali yetu inafanya kazi nzuri sasa hivi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anafanya kazi nzuri, anageuka kuanza kumtenga Rais pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo rahisi kumtenga Rais wetu na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kazi anayoifanya

anafanya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kumtenga Rais na Ilani ya Chama cha Mapinduzi haiwezekani ni kama kumtenga Lowasa na ufisadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nizungumzie jambo moja. Kuna suala ambalo limejadiliwa katika bajeti yetu kuhusiana na *road license*, wasijaribu kupotosha umma, Serikali imefuta na kuondoa kabisa tozo ya *road license*. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo limepunguza mzigo mkubwa sana, mzigo ambao ulikuwa ni lazima mwananchi aweze kwenda kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi hiyo tozo ambayo imeongezeka, tumshauri Waziri Mpango ahakikishe kwamba hiyo tozo Sh.40/= moja kwa moja anaipeleka katika kutatua changamoto za Mtanzania. Kwa sababu Mtanzania wa sasa anachoangalia je, hiyo Sh.40/= inaenda kufanya kazi gani? Shida hapa siyo tozo kuongezeka, shida ni kwamba hiyo tozo inayoongezeka inakwenda kufanya kazi gani? Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Mpango hiyo Sh.40 ambayo imeongezeka basi iende moja kwa moja kutatua matatizo ya Watanzania ikiwepo matatizo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango katika Mkoa wangu wa Songwe akinamama wanapata shida kubwa sana ya maji na ni jambo ambalo nimekuwa nikilisema katika Bunge hili. Kwa hiyo, naomba sana namna pekee ya kuweza kuwapunguzia Watanzania machungu ni kuhakikisha kwamba tunatatua kero za Watanzania. Tunaomba sana hiyo pesa iende moja kwa moja kutatua kero za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kesema hayo, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masele jiandae Mheshimiwa Joel Makanyaga.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na

kukushukuru wewe Mwenyekiti wetu kwa kunipatia nafasi siku ya leo nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya mwaka 2017/2018 kama ilivyowasilishwa na Waziri wetu Dkt. Philip Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu la Tanzania limekuwa ni Taifa la mfano katika dunia hii. Taifa letu limejitoa muhanga katika kuwakomboa Waafrika wenzetu katika nyanja za kiuchumi na kisiasa. Sisi kama Taifa tumetumia utajiri wetu kuhakikisha kwamba wenzetu wanajikomboa. Sasa wakati umefika na wakati wenyewe unamweka mbele Rais wetu Dkt. John Magufuli kuvipigana upya vita vya uchumi, ndiyo maana ameamua sasa kuhakikisha kwamba madini na rasilimali zetu zote zinanufaisha Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema neno moja kwamba Mwenyezi Mungu ametujalia sana na ametupenda akatupatia rasilimali nyingi na hasa nijikite katika suala zima la vyanzo vya nishati ya umeme. Nishati ya umeme ndiyo msingi wa mambo mengi iwe kilimo, iwe ujenzi, iwe kila kitu ukiwa na umeme wa uhakika utajenga viwanda na ukiwa na umeme wa uhakika utafanikiwa katika mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo Mungu katupa gesi, Mungu katupa maji, tunao upepo, tunalo jua la kutosha. Hivyo, niombe Serikali ihakikishe tu kwamba kwa kweli suala zima la uzalishaji wa umeme kutokana na vyanzo vyote hivyo ikiwemo makaa ya mawe yatumike katika kuhakikisha kwamba umeme unapatikana kwa wakati na kwa wingi unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali yangu kwa kuhakikisha kwamba tunaanza mara moja ujenzi wa Reli ya Kati kwa *standard gauge*. Kuwepo kwa usafiri wa reli ya kati ambao uko katika *standard gauge* ni ukombozi wa aina yake katika Taifa letu la nchi jirani za Afrika Mashariki na Afrika ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu hiki cha bajeti



cha Mheshimiwa Mpango nizungumzie habari ya Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam imekuwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ile changamoto ya kodi ya ongezeko la thamani kwa usafiri wa bidhaa zinazokwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Waziri amesema inakuwa sasa inachajjiwa asilimia sifuri ya VAT, yapo malalamiko pia kwa upande wa mawakala wa meli zinazoleta mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam nao wanalo lalamiko linalofanana na hili kwamba VAT inatozwa kwa mawakala hawa na hawa mawakala wanapochajjiwa wanaweka hiyo chaji kwenye wamiliki wa zile meli, kwa maana hiyo gharama za uendeshaji katika Bandari ya Dar es Salaam zinaonekana kwamba ziko juu zaidi na wenye meli wanakuwa wana-*opt* kwenda kwenye bandari zingine za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba na hao mawakala wa meli katika Bandari ya Dar es Salaam na wenyewe wachajjiwe kiwango cha asilimia sifuri ili kuhakikisha kwamba hizo meli zisije zikawa zinaelekezwa upande mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozunguzia habari ya ujenzi wa viwanda ni pamoja na viwanda vya mbolea ambavyo tumehaidiwa kwamba kwa sababu tumepata gesi hapa Tanzania na kwa maana hiyo Mtwara na Lindi tungeweza kupatiwa viwanda vya mbolea. Kwa bahati mbaya sana sioni hapa kwamba hizi jitihada za kuweza kujenga hivi viwanda vya mbolea ambavyo vingeweza kukuza kilimo chetu katika Taifa hili vimewekwa katika sehemu gani. Nimwombe Mheshimiwa Waziri aliangalie jambo hili kwa jicho la pekee kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa hili na Watanzania walio wengi wameajiriwa katika sekta hii muhimu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kuiomba Serikali katika Wizara ya Nishati na Madini, katika Jimbo la Mbogwe tunao wawekezaji ambao wamekuwa wanafanya utafiti kwa muda mrefu katika eneo la Nyakafuru, naomba

mara moja kwa kweli na hawa watu wamulikwe ili kuhakikisha kwamba madini yaliyopo katika Wilaya yetu yanawanufaisha wananchi wa Wilaya ya Mbogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia na kwa mara nyingine naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joel Makanyaga na Mheshimiwa Leah Komanya ajjandae.

**MHE. JOEL J. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja katika mjadala huu wa bajeti ya Serikali mwaka 2017/2018. Nianze kabisa kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu wake pamoja na timu yao nzima kwa uandaaji wa bajeti nzuri kabisa waliyoiandaa hapa na walivyoiwasilisha kwa umahiri kabisa hapa ndani. Nianze kwa kuiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuudhihirishia umma kwamba bajeti hii imedhihirisha nia thabiti ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuipeleka Tanzania kwenye uchumi wa kati kupitia viwanda kwa maana ya Tanzania ya viwanda. Bajeti hii inatilia mkazo ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge*. Reli hii itakapojengwa kwa kiwango cha *standard gauge* itasaidia mambo kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa itasaidia kutupatia pesa za ziada kwa maana ya kusafirisha mizigo ya nchi jirani. Pili, itatusaidia kupunguza gharama ya uzalishaji ya viwanda vyetu tulivyonavyo na viwanda tunavyovitegemea katika kuingiza nchi yetu katika uchumi wa kati. Mwisho, itatusaidia sana kutuondoa na tatizo kubwa la utumiaji mkubwa wa pesa katika kufanya matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara zetu kwa sababu ya kupitisha mizigo mizito ambayo inapitishwa sasa kutokana na ukosefu wa reli madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii vilevile imejikita kumwangukia Mtanzania wa chini kabisa kwa maana ya ile asilimia kubwa kati ya asilimia 65 hadi 70 ya Watanzania ambao ni wakulima. Tunaiona bajeti hii imeamua kumwondolea mzigo wa kodi kero mbalimbali mwananchi, imepunguza kodi za mazao ya chakula na kupunguza kodi za mazao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bajeti hii imeonesha wazi kabisa kumjali Mtanzania wa kawaida na wa chini kwa kuhakikisha kwamba anapata umeme kule aliko kijijini kupitia mpango wa *REA* awamu ya tatu. Katika hili, kupitia uchangiaji wa bajeti hii niombe kabisa wahusika wahakikishe kwamba ukamilishaji wa *REA* awamu ya tatu unafanyika ili wananchi waweze kufaidika na mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bajeti hii inajikita katika kuwasaidia Watanzania kuingia kwenye viwanda. Kwa mfano, inajikita kuanzisha mashamba ya miwa ili kuanzisha viwanda vingine vya sukari vitakavyowasaidia wananchi kupata uchumi kwa maana ya kulima miwa. Katika hili niombe kabisa juzi nilipata fursa ya kuongea na Waziri wa Ardhi kwamba katika Jimbo langu la Chilonwa, Kata ya Dabalo Serikali imeweza kuongea na wananchi pamoja na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amepatikana mwekezaji ambaye yuko tayari kuanzisha kiwanda pale, mazungumzo yalishafanyika na wananchi walishalima miwa, miwa imefika kiwango cha kuvunwa sasa lakini mwekezaji huyo bado kuna tatizo dogo la kupatiwa hati ya kiwanda ili aweze kujenga kiwanda na zoezi la wananchi kuanza kujipatia fedha kwa ajili ya biashara ya miwa ianze kuwafaidisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni nzuri sana kwetu na tunaposema bajeti ni nzuri tunakuwa na vigezo. Kitu kizuri au kibaya unapokilinganisha na kingine lakini kama ndio kwanza unakipata hakiwezi kuwa kizuri au kibaya ni kwamba umeanza. Tunaposema bajeti hii ni nzuri

tunailinganisha na bajeti za miaka kadhaa iliyopita, tunaona na tunashuhudia wenyewe jinsi bajeti ilivyosimama katika kumsaidia Mtanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wenzetu ambao wanajaribu kuibeza hii bajeti, waone kwamba bajeti hii tunakwenda mbele hatua moja baada ya nyingine, ni sawasawa na mtu katika maisha yako ya kawaida. Leo unapokuwa mtu wa kawaida huna hata baiskeli unatamani sana uwe na baiskeli, huwezi kutamani uwe na ndege hata siku moja, lakini ukipata baiskeli kesho utatamani uwe na pikipiki, huwezi kutamani kuwa na gari wakati huna pikipiki, ukipata pikipiki kesho utatamani uwe na gari. Kila jambo linakwenda kwa hatua, hapa tulipofikia ni hatua muhimu sana na tuna uhakika tuko kwenye njia sahihi ya kutufikisha kwenye Tanzania ya uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii sasa kwa umakini kabisa, niombe Serikali itusaidie wananchi wetu vijijini waweze kusaidiwa katika matatizo ya maji waliyonayo. Tumesema kutakuwa na michango ya Sh.40/= katika kila lita kwa maana ya *replacement ya road license*, lakini tunajua kabisa kwamba pesa hiyo inapokusanywa kutoka kwenye chanzo chochote cha Serikali inakwenda kutumika katika sekta mbalimbali ambazo zinakwenda kuwasaidia Watanzania. Vilevile katika suala la ahadi za viongozi, niombe sana Serikali izingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wanajisikia kama viongozi wanatoa ahadi na ahadi zile zinatekelezeka. Kwa kweli naishukuru Serikali hii sikivu, juzi nilikuwa na swali kuhusu ujenzi, nikamchukua Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano tukaenda naye kwenye daraja ambalo Mama Samia alitoa ahadi wakati wa kampeni na nashukuru kwamba Serikali imetenga fungu kwa ajili ya kuanza kulishughulikia safari hii. Vilevile niseme, isiishie hapo tu, kuna daraja linalounganisha Kijiji cha Msanga na Kijiji cha Kawawa, vilevile ni kati ya ahadi zilizoahidiwa na Serikali wakati ule, naomba zote zitiliwe maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo mfupi, naomba kuunga mkono hoja tena. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Leah Komanya, ajiandae Seif Gulamali.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti Kuu. Kwanza naomba kuunga mkono hoja hii ya bajeti ya Serikali kwa kuwa inakwenda kujibu matatizo ya wananchi wetu. Niipongeze Serikali kwa namna inavyoanza kutekeleza miradi ya vielelezo ambayo itakwenda kuharakisha maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*. Reli hii kwa Mikoa ya Magharibi inakwenda kuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi kwa kushusha gharama ya usafirishaji na gharama ya maisha. Reli hii inakwenda kusaidia kushusha bei ya saruji kwa kupunguza gharama ya usafirishaji, kwa sababu Mikoa ya Magharibi haina kiwanda cha saruji na saruji hii imekuwa ikisafirishwa kwa mfuko Sh.5,000/= kwa hiyo na kuongeza bei ya saruji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, bei ya saruji baadhi ya Wilaya ni Sh.16,000/= wakati wilaya nyingine ni Sh.12,000/= hadi Sh.13,000/=. Inakwenda kushusha bei ya gharama ya kusafirisha ng'ombe kutoka Mikoa ya Magharibi na kuleta mikoa mingine. Inakwenda kupunguza gharama ya usafirishaji wa marobota ya pamba kutoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa na kupeleka bandarini Dar es Salaam kwa ajili ya kusafirisha nje. Reli hii inakwenda kusaidia kupokea mizigo kutoka nchi ya Rwanda ambayo itapita reli ya kati na kuongeza kodi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niipongeze Serikali kwa kuleta marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ili kupunguza ushuru wa mazao unaotozwa na Halmashauri za Wilaya kutoka kiwango cha asilimia tano hadi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa msimu mfululizo katika Awamu hii ya Tano, bei ya pamba mwaka jana ilitoka Sh.600/= mpaka Sh.1,000/=, mwaka huu bei ya pamba kwa kilo ni Sh.1,200/=, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuwajali wakulima wa pamba. Kwa kupunguza ushuru huu pia kwa bei ya mwaka huu tunakwenda kuongeza Sh.24/= kwa kila kilo, lakini bado upo wigo mwingine, Serikali inaweza ikaangalia ni wapi pia iweze kupunguza tozo ili iweze kumwongezea mkulima bei ya pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Uendelezaji Zao la Pamba. Mkulima amekuwa akichangia Sh.15/= na mnunuzi amekuwa akichangia Sh.15/=, sawa na Sh.30/= kwa ajili ya uendelezaji wa zao la pamba. Fedha hizi kwangu mimi naziona ni nyingi, kwa mfano 2015/2016 tani 149,000 zilikusanywa, mfuko huu uliwekewa Sh.4,483,350,000/=. Naishauri Serikali ifuatilie matumizi ya fedha hizi ili iweze kulinganisha, je, matumizi ya hizi bilioni nne yanamsaidia mkulima wa pamba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hakuna tija mnunuzi apunguziwe Sh.10/= na mkulima apunguziwe Sh.10/=, wachangie shilingi tano tano, naamini itakwenda kusaidia katika kuendeleza zao la pamba katika mambo ya utafiti. Ukizingatia Serikali imekuja na mbegu mpya ambayo inaongeza uzalishaji, kwa hiyo kilo za pamba zinakwenda kuongezeka na fedha zinakwenda kuwa nyingi sana, kwa hiyo Sh.10/= pekee inatosha kuendeleza zao la pamba katika shughuli za utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pia kuna tatizo katika ucheleweshaji wa usambazaji wa mbegu na dawa na wakati mwingine hayatoshelezi. Nashauri Mabaraza ya Madiwani yapewe mamlaka ya kuweza kuuhoji huu mfuko ili utekelezaji uweze kuharakishwa. Kwa kufanya hivyo, naomba mfuko huu kama kuna viongozi wa kisiasa wasiwe viongozi katika Mfuko wa CDTF ili kuepuka mgongano wa maslahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee athari zitakazopata na Halmashauri kuhusu kupunguza ushuru huu. Halmashauri za Mkoa wa Simiyu zaidi ya asilimia 60 ya bajeti yake ya mapato zinategemea ushuru wa pamba. Naishauri Serikali ifanye kama ilivyofanya 2003, baadhi ya vyanzo vya mapato vilivyokuwa kero kwa wananchi vilifutwa, Serikali ilifanya mapitio kuangalia athari ya bajeti na baadaye Halmashauri hizo zilifidiwa. Naomba Serikali iweze kufidia Halmashauri zitakazoathirika kwa kushuka tozo ile kwa asilimia mbili kwa sababu zitashindwa kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/2017, umeendelea kutekeleza maeneo ya kipaumbele kwa kufungamanisha maendeleo ya uchumi na watu. Serikali imeendelea kusomesha kwa wingi kwenye fani za ujuzi maalum ambao pia ni adimu ili kuendana na mahitaji katika viwanda tarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo nami kuweza kuchangia katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri kwa bajeti hii nzuri ambayo ameiwasilisha katika

mwaka huu wa fedha wa 2017/2018. Tunashukuru sana kwa sababu bajeti hii sasa inaenda kupunguza ama kuleta picha fulani ya unafuu kwa wananchi wetu ambao tunawaongoza. Nami niseme tu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Manonga, Wilaya ya Igunga pia wananchi wa Mkoa mzima wa Tabora, tumeipokea vizuri sana bajeti hii ya mwaka huu wa fedha, hasa katika kuainisha baadhi ya maeneo ambayo kwa kweli kwa namna moja ama nyingine yanaenda kupunguza makali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa mfano katika uondoshwaji wa hii kodi ya *road license*, kuna watu watabeza kwa namna moja ama nyingine, lakini niseme tu tumeiondoa kutoka kuilipa moja kwa moja na tumeipeleka kwenye mafuta kwa maana tunapokwenda kununua mafuta ndipo tunakwenda kuilipa kidogokidogo. Hii pia inasaidia kupunguza kero kwa trafiki maana yake *Police Traffic* walikuwa wanapata usumbufu wa mara kwa mara kusimamisha magari na kukagua kama hawa watumiaji wa magari wamelipia ama hawajalipia, kwa hiyo imewapunguzia kwa namna moja ama nyingine kero ya kusimamisha magari. Naamini kabisa bado tutaendelea kupunguza kero zaidi za hawa *Police Traffic* itafikia hatua barabarani trafiki watakuwa hawaonekani maana yake tutaweka hata zile kamera zinazoweza kukamata kama ni mwendo kasi na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika bajeti hii, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais, katika suala zima ambalo limetokea muda siyo mrefu la makinikia kupitia Wizara hii ya Madini. Hii vita si ndogo kama ambavyo tunaweza tukaichukulia na sisi Wabunge kwa umoja wetu tukiweka itikadi za vyama vyetu pembeni, tuungane pamoja tumsaidie Rais katika jambo hili, vita ya uchumi ni vita kubwa kuliko vita nyingine ambazo tunaweza tukazifikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita hii ni kubwa kuliko hata vita ya kudai uhuru wa nchi, kwa sababu vita ya rasilimali ndiyo iliyowafanya hata baadhi ya Marais duniani kuondolewa madarakani. Hii ni vita ambayo kwa namna moja ama



nyingine kama Viongozi wa Taifa hili la Tanzania kama tuna mapenzi ya dharti na Taifa hili ni katika sehemu hii sasa tunahitaji kuungana, kusimama pamoja na Mheshimiwa Rais, kumsaidia kuhakikisha kwamba ile dhamira yake safi inatimia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wa aina au *caliber* ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni wachache sana duniani. Hiyo ndiyo napata siri ya kwa nini Mheshimiwa Dkt. Magufuli hajaenda nje ya nchi kwa muda wa miaka miwili sasa. Maana yake unaposafiri kwenda nje ya nchi unakutana na wakubwa, wakubwa hawa watakuomba mambo, mambo mengine wanayokuomba unaweza ukashindwa kuwakatalia. Sasa, sasa hivi kwa sababu tuko katika jitihada za kujikwamua kudai uhuru wetu wa uchumi, sio uhuru wa bendera, uhuru wetu wa uchumi, tupate fedha kama ambavyo Mheshimiwa Rais anasema Taifa hili linatakiwa liwe *donor country*, tuwe Taifa la kutoa misaada kwa Mataifa mengine, ni jambo ambalo linawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina rasilimali nyingi sana, ukiangalia Dubai wana mafuta tu lakini wanaweza kuwa wanafanya mambo makubwa sana, lakini Tanzania tuna kila kitu, kwa sababu tumepata sasa Kiongozi ambaye anaweza akasema bila aibu, bila kupepesa macho, hilo jambo si jepesi, hii kazi tukimpa mmoja wetu tukampa nafasi ile ambayo anaifanya Mheshimiwa Dkt. Magufuli nafikiri kila mmoja anaweza akajificha hapa. Ni jambo ambalo linahitaji uondoe sura ya aibu ndani ya macho yako, sasa inahitaji viongozi na Wabunge tuungane tumuunge mkono Mheshimiwa Rais katika vita hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua tupo baadhi ya Wabunge tunatumika kusaidia ama kudhoofisha jitihada mbalimbali katika jukumu hili. Hata kama kuna makosa, hayo makosa tuyafanye lakini tuhakikishe kwamba tunapata haki zetu za msingi. Haiwezekani makosa tuyaone tuseme kwa sababu tuna makosa tunaonewa tunaibiwa, tuseme kwa sababu tulikosea, haiwezekani! Tufanye masahihisho katika makosa yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo tunamuunga mkono na Wabunge tunahitaji kumuunga mkono na kum-*support* na kumpa moyo Mheshimiwa Rais, tufikie dhamira ya dhati. Leo hapa Wabunge tunasimama kila mmoja anadai barabara, anadai maji, anadai miundombinu, kila mtu anataka mara afya; fedha zinatoka wapi? Ndiyo hizi fedha za makinikia, ndiyo hizi fedha za rasilimali zetu tulizonazo, tuzidhibiti hizi fedha. Tutakapodhibiti tutaweza kutengeneza *fly overs*, tutaweza kutengeneza reli ambayo sasa hivi imeshaanza, naipongeza sana Serikali, tumeanza na ujenzi wa *standard gauge*, hizi zote ili kuhakikisha kwamba tunafikia malengo haya ni lazima tudhibiti rasilimali zetu tupate fedha ambayo itasaidia kujenga miundombinu yetu wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza bado tunaona kabisa katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri tuna ujenzi wa reli ya *standard gauge* kutoka Dar es Salaam inakuja Mwanza, itapitia Tabora itaenda Kigoma pia *in future* itakwenda Rwanda, itakwenda Burundi na Congo. Hii yote itasaidia kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakuwa. Tunavyoboresha miundombinu tafsiri yake tunakuza uchumi wa nchi yetu kwa sababu itarahisisha usafiri wa mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine, mzigo ambayo ilitakiwa itoke China iende Congo itapita Tanzania kupitia reli hii itakusanya mapato, kupitia mapato haya ndiyo tutatatua changamoto mbalimbali za maeneo yetu tunakotoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali katika kuboresha bado tumeweza kuona tumenunua ndege mbili kubwa ambazo zinafanya kazi na bado Serikali ina mpango wa kununua ndege nyingine, hii yote ni kufufua uchumi wa nchi yetu. Jamani, lazima tuiunge mkono Serikali hii, sasa tusipoiunga mkono mnataka tufanye nini? Kila kitu kukosoa tu, kila kitu kukataa, kila kitu kupinga, haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge wa Vyama vyote, Wabunge wa Upinzani wenyewe kazi yao kupinga, haiwezekani. Ifike hatua kwenye mambo ya msingi, masuala ya uchumi tusaidiane, tupeane moyo, ikifika

uchaguzi twende tuzungumze kila mmoja anadi yake lakini kwenye masuala ya maendeleo tuungane pamoja ku-*support* nchi yetu isonge mbele. Ninyi mnasikia furaha gani tunapokuwa na miundombinu mibovu, mnabaki tena mnalalamika, tukija hapa tupitisha bajeti ninyi mnasema hapana! Sasa nashindwa kuelewa ninyi ni watu wa aina gani? Lazima ifike hatua tubadilike, nchi hii inataka tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona jitihada za Mheshimiwa Rais kwenye ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda kwenda Tanga, bado kuna watu humu wanapinga. Hebu jamani tuache hizi kasumba za kupinga kila kitu, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, tuiunge mkono Serikali hii mpaka 2020, tukifika kwenye uchaguzi, haya mtaleta sera zenu lakini hapo tayari tutakuwa tumeshapiga hatua mbele ambazo zitahakikisha kwamba tunawakwamua wananchi wetu kuwatoa katika shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mengi sana ya kuzungumza lakini pamoja na yote naiomba Wizara kwamba *next budget*, bajeti iwe imeelekezwa kwa kiwango kikubwa sana kwenye utatuzi wa maji hasa wa vijijini, tuchimbe visima vingi sana vya maji kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo hili ambalo nafikiri kwa namna moja ama nyingine tutamtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama muda wangu utakuwa umekwisha, basi napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa mchana umekwisha, ninawashukuru kwa michango. Jioni tutaanza na Mheshimiwa Salma Mwassa, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa Joram Hongoli.

Baada ya maneno hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

**MWENYEKITI:** Tukae. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mchana niliwataja wachangaji wa leo kwamba tunaanza na Mheshimiwa Salma Mwassa, Mheshimiwa Kaboyoka na Mheshimiwa Joram Hongoli. Mheshimiwa Mwassa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na uhai. Vile vile napenda kuchangia hii bajeti kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nijielekeze kwenye hoja. Naanza kwa kusema kwamba nimewasikia Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wakisema kwamba ninyi Wapinzani huwa ni watu wa kupinga tu. Siyo kweli, sisi Wapinzani hatupingi kila kitu ila pale ambapo tunaona kabisa Serikali haitendi sawa, tunashauri. Hiyo ndiyo kazi yetu, kusimamia na kuishauri Serikali. Kwa hiyo, siyo kila kitu tunapinga ila tunapinga kile ambacho tunaona hakiendi sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile msituangalie kwenye ile *negative way* kwamba Wapinzani hawa; sisi ni kioo chenu ninyi watawala. Wapinzani ni kioo cha Mtawala. Sasa kama utaona kabisa kwamba kioo kinakwambia hapa bwana hujapaka mafuta, halafu bado unabisha kwamba aah, nitakwenda hivyo hivyo, utachekesha. Kwa hiyo, lazima ukiheshimu kikoo chako. Kwa hiyo, Upinzani ni kioo na lazima mkubali kama Watawala, sisi ni vioo vyenu, lazima tuseme pale mnapokosea na mnapofanya sahihi, tunasema kwamba mmefanya sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie bajeti hii kwenye maslahi ya wafanyakazi. Nikiangalia Tanzania tuna makundi makuu mawili, au manne; kuna wafanyakazi, wakulima, wafanyabiashara na wawekezaji. Nikiangalia hii bajeti, imewataja wakulima. Ukiangalia kwenye tozo zao wamepunguziwa tukaenda sawa. Wafanyabiashara nao

wametajwa, kodi zao nyingi nazo zimeguswa. Wawekezaji nao wametajwa vile vile. Je, mfanyakazi katajwa wapi? Mshahara wake umeongezewa wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyakazi huyu sijaona hata sehemu moja mmesema kwamba mnamwangalia kwenye maslahi yake kama hizo posho mbalimbali; au basi hata kama hiki anachostahili kuongezewa mshahara; imepita Mei mosi hapa juzi hatujaona *increment* yoyote ya mshahara. Tukasema basi bajeti kuu hii tuiangalie labda mtawaongezea wafanyakazi mshahara, hakuna. Vile vile wafanyakazi basi kama hamtaki kuwaongezea mshahara, basi waangalieni makato yao. Bado makato ya wafanyakazi ni makubwa, kuna *Pay as You Earn* ambayo hiyo ni tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *income tax* inasumbua sana. Sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge hapa tunakatwa asilimia 30. Tunalipa kodi kweli kweli, lakini ukiangalia mfanyakazi wa umma naye ana ile *two digit* sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha hawa wafanyakazi hata ukiwasikiliza kwenye vikao vyao ni hii *Pay as You Earn* kuja kwenye *single digit*, mnaichukuliaje kama Serikali? Mheshimiwa Waziri, wewe ulikuwa mfanyakazi, usisahau ulikotoka. Wangalie wenzio! Dada yangu Mheshimiwa Angella vile vile mshauri Mheshimiwa Rais vizuri, awaangalie wafanyakazi hawa, maana yake ni tatizo. Yaani mfanyakazi sasa hivi anajiona kama ni tatizo kufanya kazi. Anaona kama vile yeye ni mtu ambaye anachukuliwa sijui vipi. Watu wote mnawaangalia, lakini bado mfanyakazi anaonekana sijui kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu wafanyabiashara wadogo. Wafanyabiashara wadogo mmesema kwamba mtawatambua. Kwanza napongeza kwa kuwatambua na kuwapa vitambulisho. Hiyo italeta faida gani? Itawafanya hata waende benki kirahisi; lakini unamtambuaje kama hana ardhi; kama hujamtengea eneo? Hivi unamtambua halafu atembe barabarani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam sisi tuna tatizo kubwa sana la wafanyabiashara wadogo wadogo, hawana maeneo sahihi. Basi mtambue, mweke sehemu sahihi pia. Unamtambua halafu anazungukazunguka! Leo yuko Tandika, akigeuka huku, kwenye miji yote mikubwa tatizo ni wafanyabiashara wadogo wadogo. Kama mnataka kweli mwatambue walipe kodi, basi waandalieni na mazingira sahihi. Kwa hiyo, waandalieni mazingira sahihi waweze kufanya kazi zao kama walivyo wafanyakazi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye kodi ya majengo. Kodi ya majengo Mheshimiwa Waziri umeisema. Kuna kodi ya majengo na mabango. Kwanza niseme kabisa, kwa kuchukua kodi hii kwanza kabisa mmepoteza ile zana ya *D by D*, japo hapa Waziri wa TAMISEMI anatuambia kabisa, mimi ni muumini wa *D by D*. Basi afanye kwa vitendo! Siyo *D by D* anaangalia Halmashauri zinanyang'anywa hata bajeti zao saa hizi zimefurugika. Kwa sababu hii kodi ya mabango ilikuwa kwenye bajeti zao. Kwa hiyo, saa hivi ina maana tutavuruga? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, kuchukua kodi ya majengo au kodi ya mabango kwenda Serikali Kuu linaweza lisiwe kosa, lakini sasa mngewaachia kule kule. *System nzima* ya ukusanyaji ingekuwa Halmashauri. Kwa maana wao wenyewe wangukuwa na *data* na *TRA* ingekuwa na *data*. Ninachomshauri Mheshimiwa Waziri, aanzishe Kitengo cha *TRA* ndani ya Halmshauri zote. Angalau achukue wale wafanyakazi wawili wa *TRA* waje kwenye Halmashauri wao wenyewe wafanye ile *collective responsibility*, lakini kazi ya kwenda *site*, kazi ya kukusanya *data*, kazi ya kuthamini majengo yote, waachie Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hapa amesema mwenyewe eti nyumba zote atazi-charge kwa *flat rate*. Ghorofa itakuwa Sh.50,000/=-, nyumba za kawaida Sh.10,000/=. Kwanza kuna ile *Urban Authority (Rating) Act* ya mwaka 1983. Sijui ameisoma vipi? Sijui inaenda kuwa *accommodated* wapi? Kwa sababu ile inasema hivi,

nyumba yoyote inayochajiwa kodi ni ile nyumba iliyojengwa kwa *permanent material* au *material* haya ya muda ambayo ni ya tofali na bati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaponiambia kama huko sijui Chunya au Mbozi huko kwenye Halmashauri hizo za huko ndani; na ile ni *Urban Rating* inaitwa hivyo; kwa hiyo, kwanza ni kodi ya Mijini. Sasa unaposema kila nyumba Sh.10,000/= mimi sijaelewa. Mpaka hapo labda Mheshimiwa Waziri anitolee ufafanuni akija kuhitimisha. Ana-charge nyumba za udongo? Nyumba za undogo anazi-charge vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri asikwepe jukumu lake, yaani hawezi ku-charge kwa *flat rate*. Kwanza anaikosha mapato Serikali. Lazima ufanye uthamini. Uta-charge vipi wewe *flat rate*? Ghorofa kumi utai-charge vipi Sh.50,000/= ? Ghorofa moja uta-charge vipi kwa Sh.50,000/= ? Au ata-classify vipi? Sisi atueleze akimaliza hapa, hii *flat rate* anaifanyaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachomshauri Mheshimiwa Waziri, apeleke watu wa TRA kwa uchache wao, kwa sababu hawana *manpower* ya kwenda kila Halmashauri, hawana! Wanachofanya sasa hivi, wanachukua wale wafanyakazi wa Halmashauri wachache wanawapeleka kule. Halmashauri ina *manpower*, ina Balozi wa Nyumba Kumi, ina Mwenyekiti, ina Mtendaji wa Mtaa. Kwa hiyo, cha kufanya, wale ni watoto wake awalee. Wapelekwe hao watu wa TRA kwenye kitengo maalum kwenye Halmshauri pale, kila Halmashauri wawepo. Kwa hiyo, wao wataangalia ile *collection* inavyoenda na hao Halmashauri nao watakuwa na *data*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *road license*. Sisi kwa kweli kilio chetu kilikuwa ni madeni makubwa wanayolimbikiziwa wananchi. Kwa hiyo, tuipongeze Serikali kwa kusikia hilo. Kweli mmefuta, lakini sasa hii 40 mwiangalie tena kwa mapana. Tatizo kubwa bado ni maji. Tatizo la maji

bado linatafuta, yaani Tanzania nzima ni *issue* kwa kweli! Basi kama ndiyo hivyo, hii 40 mchukue asilimia 20 mpeleke kwenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba kodi hii pia nami niungane na wenzangu isiwekwe kwenye mafuta ya taa, iwekwe kwenye tu kwenye vyombo vya moto. Mafuta ya taa yanatumika kwenye chombo cha moto? Unaweza kuweka kwenye gari! Hii kodi ilikuwa ni kodi ya barabara. Sasa kibatari hakiko barabarani. Mafuta ya taa msiyaingize kwenye kodi hii. Kodi hii iwekeni kwenye *diesel* na mafuta ya petrol peke yake. Vile vile hiyo Sh.40/= basi mwiangalie na mambo ya maji mnayaingizaje hapo? Kwa sababu hiyo nayo ni huduma sahihi na inatakiwa pia ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kitu kingine, mmeangalia tu kodi ya majengo, lakini kuna kodi zinazopotea nyingi sana. Kwa mfano, kodi ya ardhi ni chanzo kikubwa mno ambacho kinaweza kikaendesha Serikali nzima hii bila ya kutegemea Wizara nyingine yoyote. Inaendesha Wizara zote; lakini hampangi, hampimi. Hebu wekeni mkakati kabisa wa kupima, kupanga na kuthaminisha ili mpate zile kodi zilizo sahihi. Tukiweza kupata hata asilimia 50 kabisa ya ardhi iliyopimwa hapa, tuaongea mambo mengine, maana ardhi nayo ni madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mlivyosikia kwenye madini, ushauri wetu mkausikiliza mkafanya, naamini kwamba na Mheshimiwa Rais naye atalisikiliza vile vile. Lazima atafute hela apange na apime. Haya nayo ni madini yanayopotea, kwa sababu ardhi kubwa hailipiwi, ardhi haielelewi, ugomvi kila siku, inapoteza mapato ya Serikali. Pimeni, mpange ili mweze kupata mapato. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naona Mheshimiwa Maftaha umekomaa kisiasa. Maana yake wewe ukisema hupigiwi makofi. Wewe wenzako unawapigia. Kwa hiyo... *(Makofi)*

Haya, tunaendelea. Mheshimiwa Kaboyoka na Mheshimiwa Hongoli ajiandae. *(Makofi)*



**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Mwaka wa 2017/2018. Nataka kujikita katika maeneo machache na hasa nikiangalia maeneo ya kipaumbele katika mwaka huu wa 2017/2018. Viko vinne, lakini nitataja viwili tu. Kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, hiyo nakubali; kufunganisha uchumi na maendeleo ya watu; hapo ndipo ninapoona tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mahali ambapo kuna wananchi wengi ambao ndiyo wanataka *focus* yetu iangalie ni vijijini kwenye sekta kubwa inayoajiri wananchi wengi, ambayo ni Sekta ya Kilimo. Nilikuwa najiuliza, hivi bila kuweka kipaumbele katika kilimo, mifugo na uvuvi, tunafunganishaje uchumi na maendeleo ya watu? Kwani watu wengi wako katika sekta hiyo ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka huu unaoishia 2016/2017, kilimo kilipata shilingi bilioni 3.369 sawa na asilimia 3.31; mifugo na uvuvi walipata shilingi bilioni 1.2 sawa na asilimia nane tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Sasa tunaposema kilimo ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu ambao inachangia asilimia 28 katika maendeleo ya nchi yetu, lweje basi asilimia 96.69 haikuidhinishwa, badala yake wamepewa asilimia 3.3 tu? Hivi kweli Sekta hii ya viwanda itakuaje kama hatuunganishi na malighafi kutoka kwenye kilimo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona kwamba mambo yetu yako *mismatch* kwamba hatu-*focus* kwamba kama kweli tunataka viwanda na kama tunataka kuondoa umaskini, lazima *concentration* yetu iwe katika kilimo, ambapo kule ndiyo kuna wananchi wengi. Kule ndiko kuna maskini wengi na kwa ajili hiyo tukiongeza thamani kwenye mazao yao, kwenye viwanda tutakuwa tumewasaidia wananchi wetu kwa sehemu kubwa katika kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia sekta nyingine ya Wizara ya Maliasili na Utalii, hii ni Sekta ambayo pia inachangia asilimia 25 (mnaweza kunisahihisha) katika uchumi wetu. Nayo ilipewa shilingi milioni 156.6 sawa na asilimia nane ya fedha walizoomba. Sasa hii ina maana kwamba asilimia 92 ya pesa yote waliyoomba hawakupata. Sasa ninachojuliza, kama hata Sekta hii ya Utalii ambapo Balozi wa Marekani aliyekuwa *Black American* wakati ule hapa nchini, alisema, Tanzania hii kwa utalii wake tu kama wangeweka *emphasis* kwenye utalii, sisi tungetoka Marekani kuja kuomba msaada katika nchi hii. Sisi tunapuzia zile sehemu ambazo ndizo zinachangia katika uchumi wetu kukua haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kuweka barabara na reli ni kitu kizuri na ninakiunga mkono, lakini tuwe *focused* kwamba reli inaenda kuchukua nini kwa mfano Mwanza? Je, kilimo cha pamba tumekitilia mkazo? Je, viwanda vinavyowekwa ni vya kutengeneza nguo ili tuongeze thamani katika pamba zile au tunaweka huku kiwanda, usafiri unawekwa pengine na maji yanawekwa pengine? Sasa huu uchumi wetu wa Tanzania na huu umasikini tunauondoaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza, maajabu gani tutakayopata sasa hivi kwenye kodi ambayo tutatoka kwenye ile shilingi trilionini 29 tuingie shilingi trilionini 31.7? Tunakusanya vitu gani? Pesa zinatoka wapi? Ukiangalia, hata hii tunayosema tuchukue kodi ya nyumba ambazo hata hazikuthaminiwa, kwa kweli ni maajabu sana. Kwanza itakuwa ni kilio kikubwa kwa wananchi wetu maskini, kwamba juu ya shida walizonazo vijijini, bado tuwaongezee mzigo ambao wanatakiwa walipe Sh.10,000/= kwa kibanda cha mbavu za mbwa! Hii kweli mimi siioni ni sawa kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitegemea kwamba aidha bajeti yetu ibaki ile ile, tu- *address* ule upungufu wote ambao kwa mwaka huu unaoisha hatukuweza kuufikia au ipungue ili tuwe *very realistic*, tuseme kwamba tutafanya kazi kwa pesa ambayo tunayo. Mfadhili

akileta itakuwa *bonus*. Sisi tuna-*assume* kwamba hawa wafadhili watatuletea tu au tutapata mikopo *as a result* tunaweka bajeti kubwa ambayo mwisho wa siku tunarudi kusema ooh, bajeti ya maendeleo ilitekelezwa kwa asilimia 38. Ni aibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, tukiingia kwenye hii kodi ya mafuta ya taa, kwa kweli mimi hili siliungi mkono kabisa. Mafuta ya taa ndiyo nishati kubwa sana vijijini, *especially* ukingalia kwa mama zetu wengi ndio wapishi, wengi hasa wa mjini pia, wanatumia haya majiko ya kichina ambayo yanatumia mafuta ya taa. Sasa hivi hapa kwenye Bunge lako tunaambiwa mkaa unakatazwa, kuni zinakatazwa, tusikate miti; kuna mwenzetu alisema sasa hivi tunaleta gesi. Hivi ana habari gesi hii miaka saba mpaka kumi ijayo ndiyo itaweza kuingia majumbani kwetu kwa kutumia mitungi? Ana habari hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa akinamama maskini vijijini, wakae miaka saba mpaka kumi wakingojea gesi? Mimi nafikiri hii kodi ya mafuta ya taa tuiondoe ili wanawake wengi ambao ndio wapishi; vibatari huko vijijini ndiyo vinatumia mafuta ya taa, tuwasamehe katika kuongeza hiyo Sh.40/= kwenye mafuta ya taa. Kwa hiyo, nasema kama hii bajeti kweli inajali maskini, nasema hii Sh.40/= itolewe kwenye mafuta ya taa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji. Nashauri ianzishwe *agency* ya maji vijijini, maana tumeshaona pesa nyingi za maji zinakwenda kwenye maji ya mijini na kutokana na *audit report* ya CAG imeshaonesha kwamba kuna ubadhirifu mkubwa sana katika hii miradi ya maji ya mijini. Kwa hiyo, sioni kwa nini maji bado yaendeleo kuwekwa mjini badala ya kupelekwa vijijini. Kwa hiyo, nashauri kwamba angalau asilimia 70 ya bajeti ya maji ipelekwe vijijini ili kusudi akinamama tuwatue ndoo vichwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira, kweli hii inashangaza sana. Kama hatutatilia mkazo ajira na ukiangalia *standardza ILO*, tuzungumzie *gainful employment*,

tusizungumzie tu ajira, maana ajira tunaambiwa mbona mashambani watu wanaajiriwa wengi, ardhi yetu ni kubwa! Tuangalie *gainful employment*, watu wapate kipato kutokana na ajira zile. Hapa katika mpango huu sioni mahali ajira ilipowekewa msisitizo. Kwa maana hiyo ni kwamba, tutatoa wanafunzi wengi wanaomaliza Vyuo Vikuu, wanamaliza VETA na maeneo mbalimbali ambao watakuwa mijini. Katika uzee wetu tutakuta wanatuingilia mpaka majumbani. Tunatengeneza majambazi wengi ambao kesho hatutaishi kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kabisa tungeangalia kwamba ajira zetu tunaziwekaje ili tuone tuna-*create* vipi ajira hii? Hii kusema kila mtu aanzishe viwanda, hiyo siyo *practical*. Viwanda vina *systems* zake, siyo kwamba mimi kila leo nikiamka naenda kuanzisha kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uangalie mtaji unapata wapi? Kiwanda cha aina gani? Hata hicho kiwanda ukianzisha ume-*import material*. Vipuri unatoa wapi? Soko lako liko wapi? Ni kitu kikubwa ambacho kingetakiwa Serikali ibainishe yale maeneo muhimu ambayo tunasema tukianzisha kiwanda hiki, kitaajiri wananchi wangapi na *material* yake yatatokana na kilimo, tuta-*add value* na tuta-*export* wapi ili tupate ajira na tupate fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli zetu za maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema bado sijaridhika kwamba uchumi wetu... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Getere ajiandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake wa kizalendo na kijasiri wa kuzuia usafirishaji au utoroshaji wa madini nje ya nchi na makampuni haya ya madini. Nampongeza sana. Naomba Watanzania hasa Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa kwenye mambo ya msingi yanayohusu nchi na maslahi ya nchi, ni muhimu sana kuungana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamepiga kelele hapa, wamelalamika kwamba wanaonewa, mara tutashtakiwa, lakini leo hii, mchana huu tumeshaona Mwenyekiti wa Makampuni ya *Barrick* amekuja kuomba msamaha kwamba fedha au madini waliyotorosha watarejesha hizo fedha na wapo tayari kujenga mtambo wa *smelting* wa kuweza kuyeyusha madini haya nchini. Kwa hiyo, nampongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi huo. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tunapokuwa na mambo ya Kitaifa, tunapokuwa tunatetea jambo la kuhusu Taifa hili, kuhusu uchumi wa nchi hii na tunapotetea wanyonge wa nchi hii, ni muhimu sana kuungana. Tunapotengana Waheshimiwa Wabunge ndio tunapoteza na tunawakandamiza wale wenzetu wanaobaki kule ambao wametutuma tuwatetee. Naomba siku nyingine tujifunze kuungana na kuwa wazalendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuleta hotuba nzuri ya Wizara yake. Ni hotuba ambayo inatuonesha kwamba tunaenda sasa kwenye uchumi wa kati, uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kuondoa hizi kodi na tozo mbalimbali. Nimeona mmeshaondoa tozo na kodi mbalimbali kwenye malighafi ambazo zinatumiwa kutengenezea vifaa vya walemavu. Zinapoingizwa toka nje, kodi zimepungua na kuondolewa

kutoka asilimia 25 na sasa itakuwa asilimia sifuri. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii hakuna asiyejua, walemavu tunao wengi na kila siku walemavu wanaongezeka. Hata sisi Waheshimiwa Wabunge tuliopo humu ndani ni walemavu watarajiwa. Kwa hiyo, kwa kupunguza hii kodi na tozo kutoka kwenye asilimia 25 mpaka sifuri kutawezesha sasa viwepo viwanda vya kutengeneza au kuunganisha vifaa vile ambavyo wanatumia watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutatoa ajira ambayo itasaidia vijana wetu waliopo hapa nchini, waweze kuajiriwa kwenye hivi viwanda vya uunganishaji au kwenye viwanda vile vinavyohusika na utengenezaji wa hivi vifaa ambavyo wanatumia walemavu. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wako kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, napongeza pia kwa kazi kubwa mliyoifanya kwa kuondoa kodi hasa kwenye mazao wanayozalisha wakulima wadogo wadogo. Wakulima wamekuwa wakipata shida sana na bei ya mazao imekuwa haipandi kwa sababu ya kodi nyingi ambazo wanawekewa hawa wakulima. Kwa hiyo, napongeza kwamba mmeondoa hizi kodi, naamini sasa wataweza kuuza kwa bei nzuri na hatimaye kupata faida kutokana na shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo pengine tuliangalie vizuri. Kule Lupembe katika Jimbo langu, tuna kilimo cha miti; tunapanda miti na tunahamasisha watu wapande miti kama zao la biashara. Sasa inapofika wakati huyu mkulima ametunza miti yake, anaenda kuuza sokoni, anakutana na kodi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kodi anayolipa anatakiwa kulipa *transit pass* ambayo inalipwa Serikali Kuu Sh.15,000/=, anatakiwa kulipa *TP*katika Halmashauri ambayo

ni Sh.3,000/=, anatakiwa kulipa ushuru wa mbao ambao ni Sh.200/= kwa kila mbao, lakini pia anatakiwa kulipa ushuru wa leseni ya biashara ambayo ni Sh. 261,000/= kila mwaka, anatakiwa alipe kodi ya mapato ambayo ni Sh.1,500,000/= kwa mwaka, anatakiwa alipe leseni ya uvunaji ambayo ni Sh.261,000/= na vile vile anatakiwa akodi gari kwa Sh.3,000,000/= ili aweze kufikisha mzigo wake pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hizi kodi ni nyingi mno. Anaambiwa kwamba unapokuwa amelipa hizo kodi mbalimbali ni lazima awe na risiti ya *EFD*. Huyu mkulima amelima miti yake, ameungana pengine na wenzake au yeye mwenyewe ameamua kuipeleka sokoni ili aweze kupata bei nzuri. Anapopeleka sokoni anakutana na hiki kikwazo kwamba lazima awe na risiti ya *EFD*; huyu mkulima hana mashine, atapata wapi risiti ya *EFD* zaidi ya ile risiti ambayo inakatwa na Halmashauri na risiti nyingine za ushuru ambazo nimeziorodhesha hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuliangalia hili. Kwa kweli wakulima wa miti wa Njombe, Lupembe na maeneo mengine ya Njombe tunaozalisha miti, imekuwa ni kero kubwa sana kwao. Hebu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ajaribu kuziangalia hizi kodi ambazo wakulima wetu wamekuwa wakitozwa wanapokuwa wanasafirisha huu mzigo wa mbao ambao wameuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijaribu kusema pia kodi moja ambayo ni kero kwenye maeneo mengi lakini pia na kwenye eneo letu sisi. Kuna hii kodi ya *SDL (Service Development Levy)* ambayo inatozwa kwa kutoa huduma; wanalipa kwenye mashule lakini pia wanalipa wafanyabiashara. Hebu tujaribu kutoa ufafanuzi mzuri na tujaribu kuwaelimisha na kutoa elimu ya kodi vizuri ili waweze kuielewa, maana ilivyo sasa hivi hawaelewi vizuri. Kwa mfano, kwenye shule wamekuwa wakitoa hizi kodi nyingine nyingi lakini pia wanalipa na hii kodi ya *Service Levy* na wakati huo

huo wanatakiwa warejeshewe fedha zile kwa ajili ya kuendeleza mafunzo ya ufundi, lakini shule zimekuwa hazipewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tujaribu kuziangalia hizi kodi na ikiwezekana tukae na hawa wenye shule na wafanyabiashara ili wasione kama ni kero. Waelimishwe vizuri, naamini wakielewa vizuri wataweza kulipa hii kodi vizuri bila tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi nyingine ambayo ni kodi ya uanzishwaji wa maduka ya madawa. Nawapongeza sana, imeshaondolewa, nayo ilikuwa ni kero kubwa; lakini mmesahau kodi ya uanzishwaji wa maabara. Maana duka la madawa linaendana na maabara. Kwa sababu kuwa na duka la madawa maana yake kuna Daktari ambaye kabla ya kutoa *prescription* anatakiwa aende kwenye maabara huyu mgonjwa akapime na akishapimwa arudi kuandikiwa dawa. Sasa kwenye maabara hamjatoa hizi kodi. Mpaka sasa hivi wanalipa kodi kwa maana ya uanzishwaji wa maabara Sh.330,000/= kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama basi ajaribu kuaingalia hii kodi pia, maana wenye maabara wanalalamika kwamba kwa nini wao wamesahaulika wakati wenzao wamepewa hilo punguzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme juu ya maji vijijini. Wote tunajua Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakipiga kelele sana juu ya tatizo la maji vijijini. Maji yamekuwa yakipoteza muda mwingi sana wa akinamama na mabinti zetu kwenda kutafuta maji. Naomba katika ile Sh.40/= basi fedha hiyo iende kwa ajili kuongezea kwenye Sh.50/= ya zamani ili iwe Sh.90/= ili usambazaji wa maji uweze kuongezeka na hatimaye mama zetu hawa wasipoteze muda mwingi kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anaweka mambo haya



sawa tujue hii Sh.40/= inaenda wapi? Wengine wamelalamika kwamba Sh.40/= ni kubwa inaongezea wananchi gharama. Wamesema wasafirishaji hapa kwamba haiongezi chochote kwa maana ya gharama za nauli. Kwa hiyo, kama haiongezi chochote na watumiaji wa mafuta ya dizeli na petroli ni watu wenye magari au ni watu ambao wana bodaboda, naamini kwamba wana uwezo wa kustahimili kulipa hii Sh.40/= ambayo imeongezwa kwenye tozo za mafuta ili wananchi wetu waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya miradi ya umeme kwa maana ya *REA*. Naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha utaratibu huu kuhakikisha kwamba kila kijiji sasa kinapata umeme. Nashukuru, nimeona kwenye mpango katika vijiji vyangu vyote; Vijiji vya Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe vimeshawekwa kwenye mpango wa kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba watakapofika wasisahau maeneo au kusiwepo na vitongoji vitakavyopitilizwa bila kuwa na umeme au havishushiwi umeme kwenye eneo fulani ili kusiwe na ugomvi au kusiwe na malalamiko ya wananchi ambao hawajapata umeme kwenye Vitongoji. Kwa hiyo, naamini Serikali yangu, naamini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini yupo, basi mtahakikisha kwamba kila kijiji na kila kitongoji kinakuwa na umeme ili wananchi wetu waweze kutumia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Edward Mwalongo, ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wao. Nachukua nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa nguvu na juhudi kubwa anazozifanya katika kuokoa mali ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili iko dhana inajengwa hapa kwamba Rais Magufuli anafanya kazi yake bila kuhusisha Chama cha Mapinduzi. Sasa leo nimekuja hapa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuonesha wenzetu kwamba Rais hafanyi mambo yake, anafanya ya Chama cha Mapinduzi. Baadaye kama kuna mtu anahitaji Ilani hii tutampa aisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kunukuu maandishi ya Chama cha Mapinduzi kwa ujumla wake. Na. 4 inasema:-

“Katika miaka mitano ijayo 2015 - 2020, CCM ikiwa madarakani itaelekeza Serikali zake kutumia nguvu zake zote kuendeleza na kupambana na changamoto kubwa nne.

(i) kuondoa umaskini; kupambana na makinikia, kuzia wizi ni kupambana na umaskini;

(ii) Kupunguza tatizo la kukosefu wa ajira hasa kwa vijana wetu. Kutafuta fedha zinazoibiwa ni kuleta ajira ambayo tutaitumia baadaye kwenye viwanda; na

(iii) Kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hii ni ilani inayozungumza mambo hayo, maana yake CCM tunaelekeza kwamba Rais wa kwetu atakayepatikana atatekeleza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikutosha tukasema, sambamba na kupambana na tatizo la rushwa, Serikali pia zinaelekezwa na CCM, zinatakiwa kushughulikia kwa ukali zaidi tatizo la ubadhirifu na wizi wa mali ya umma. Kwa hiyo,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anatekeleza yale tuliyoumwelekeza Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ile dhana inayojengwa kwamba Mheshimiwa Dkt. Magufuli anafanya yake, siyo kweli na yako mengi humu ndani. Mkitaka tutawapa mwendelee kusoma hayo mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo nayashangaa humu ndani, nayashangaa sana. Leo duniani kote, Korea Kusini pamoja na vita waliyonayo na Korea Kaskazini wamemfukuza Rais wao kwa sababu ya ubadhirifu; leo Brazil pamoja na umaskini ambao umekithiri, wamemfukuza Rais wao. Leo Urusi pamoja na juhudi kubwa za Putin lakini leo wanaandamana kwamba anakula rushwa. Sasa leo Rais wetu anapopambana kutoa rushwa na ubadhirifu...

**MBUNGE FULANI:** Na Venezuela.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Venezuela nao wamemtoa Rais, naambiwa hapa. Rais wetu anapopambana kwenye mambo ya ubadhirifu, tunashindwa kumshangilia na kumpa na pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba siyo jambo jema, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wote tukaungana pamoja, tukashughulikia ubadhirifu huu na bahati nzuri sasa taarifa zilikuwa hewani kwamba wale watu ambao mlikuwa mnasema watatupeleka Mahakamani, wameshakubali kulipa. Sasa shida iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelekezo haya sasa, niende kuchangia, nijielekeze kwenye mambo ya viwanda na kilimo. Tunapozungumza viwanda maana yake tunazungumza kilimo; tukiendeleza kilimo chetu, ni lazima tubadili kilimo chetu cha mazao mbalimbali ili kupata nakisi ambayo itasaidia kwenda kuendeleza viwanda. Ni lazima ufugaji wetu tuabadili ili tuweze kupata mazao bora kwa

ajili ya kupata viwanda. Malighafi itakayopatikana katika kilimo na katika mifugo isaidie kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji kwenye Jimbo langu la Bunda ni tatizo kubwa sana na namshukuru Mheshimiwa Rais kwamba anapopambana na ufiisadi huu hela zitapatikana ili zije kwenye maji katika Jimbo la Bunda. Tuna miradi mitatu ya maji; kuna mradi wa Nyamswa wa *World Bank*, mradi wa Kiloleli na Salamakati. Miradi yote hii haijaenda kwa sababu fedha hazijaenda kwenye maeneo yangu. Mheshimiwa Waziri anapokuwa kwenye bajeti yako, naomba ufikirie namna ya kupeleka fedha Bunda kwa ajili kuendeleza miradi yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya barabara. Tuna barabara ya Nyamswa – Bunda, barabara ya Makutano – Sanzati – Nata na tuna barabara ambayo inakwenda kukasimiwa kuwa barabara ya *TANROAD* ya Mgeta – Siolisimba – Mikomalilo. Kwa hiyo, naomba maeneo haya tuzingatie wakati tunapokuwa tunafanya bajeti hiyo waone namna gani mnasaidia miradi yangu kwenye Wilaya ya Bunda na Jimbo la Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Hospitali yetu ya Kongwa Mkoa wa Mara, ni ya muda mrefu sana na tumeisemea sana. Tunaomba kipindi hiki cha bajeti waikumbuke Hospitali ya Kongwa ambayo ni Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Bandari yetu ya Musoma, hii ni bandari ya muda mrefu sana na kwa sasa hivi imechakaa. Tunaomba waitengee fedha na niliona wanaenda kuishughulikia. Kwa hiyo, waone namna gani ya kusaidia ili Mkoa wa Mara nao upate bandari na iweze kutumika vizuri. Bahati nzuri kuna meli ya *MVButiama* ambayo iko Mwanza inatengenezwa. Kwa hiyo, ikitengemaa tuone namna ya kuifikisha Musoma kwa ajili ya kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna reli ya kutoka Tanga – Arusha – Musoma, tumeizungumza sana. Pamoja na kwamba

tuna reli ya kati ambayo tunaipigia upatu, lakini hata reli hii inayotoka Tanga – Arusha – Musoma inaweza kusaidia katika maeneo yetu na kuendeleza uchumi wa watu wetu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa tunazungumzia mambo ya wakulima, lazima tukubaliane namna ya kuboresha zao la pamba. Katika Mkoa wa Mara hakuna zao lingine la kibiashara, ni zao la pamba ambalo liko pale. Kwa hiyo, tunapokuwa tunazungumza haya mambo, ni lazima tuone ni namna gani tunapandisha bei ya pamba. Miaka mingi sana tumekuwa tukitegemea Soko la Dunia, lakini lazima tutegemee viwanda vyetu vya ndani ili tuweze kukuza bei ya pamba katika Mkoa wa Mara na Kanda ya Ziwa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo ya wafugaji. Tumekuwa na Kamati mbalimbali; kuna Kamati zimeundwa kwa Wizara tatu. Tunaomba zile Kamati zifike Mkoa wa Mara na hasa eneo moja linaitwa Kawanga kwenye Jimbo langu la Bunda ambako kuna migogoro mikubwa sana ya wafugaji kati ya Pori la Akiba la Ikorongo na eneo langu na Vijiji 15 vilivyopo kwenye maeneo haya ili tuweze kuona namna gani tunaweza kusaidia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo mengi sana ya ndovu kwenye maeneo yetu. Tunaomba zile fidia ambazo zinahitajika kwenye maeneo haya; kuna Kijiji kimoja ama Vijiji vitatu vimebaki vya Maliwanda, Mgeta na Kyandegge. Tuone namna ya kuvisaidia hivyo vijiji ambavyo havikupata fidia ya kifuta jasho ambapo vijiji vingine vimepata lakini vyenyewe havikupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viwanda viwili vidogo vidogo vya maziwa, havifanyi kazi muda mrefu sana; kimoja kipo Kyandegge na kingine kipo Mgeta. Kwa hiyo, tunaomba waone namna gani hivyo viwanda vinaweza kusaidiwa ili viweze kutoa mazao yao kwa ajili ya kuwapa faida wakulima wa maeneo hayo. Hivi viwanda vilijengwa enzi

hizo za miaka ya nyuma tukiwa na Kiwanda cha Maziwa Musoma ambacho kimekufa, sasa tuone namna gani ya kuvifufua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viwanda vya pamba viwili; Ushashi na Bramba. Kwa hiyo, tunaomba tuweze kusaidiwa kuvifufua viwanda hivi kwa ajili pia ya kuongeza zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii zana inayozungumzwa ya tozo ya *road license*. Gharama za mafuta kwa miaka ya hivi karibuni zimekuwa zikishuka sana, lakini hatujawahi kuona nauli ya kutoka Bunda kuja Dodoma inapungua. Kwa hiyo, hata tukipunguza habari ya mafuta, wala hawa watu wanaofanya biashara ya usafirishaji hawapunguzi gharama zao za nauli. Kwa hiyo, naona kwamba hii Sh.40/= tuliyoiweka tungeongeza Sh.10/= ili tuipeleke kwenye maji kwa ajili ya kusaidia akinamama wanaohangaika na maji kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tukiwa tunazungumza suala la walemavu, ni vizuri tukaona namna gani ya kupunguza baadhi ya gharama. Pamoja na kwamba zimepungua, lakini bado. Tuwasaidie walemavu katika maeneo mbalimbali na hasa wale watoto wanaotakiwa kusoma ili wapewe vifaa bora kwa ajili ya kujifunza na kwa ajili ya kupata manufaa katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hapa ni kuhusu umiliki wa akinamama katika suala la ardhi. Sasa ni vizuri tukiwa tunazungumza hapa, tuone kama bajeti hizo zinawekwa kwenye maeneo haya ili tuweze kuona, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Felister Bura wajiandae.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante wa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, mpaji wa yote kwa kutujalia afya njema mchana wa leo na tunaendelea kujiadili Bajeti yetu ya Mwaka wa Fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niseme nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizaru ya Fedha na Mipango kwa ujumla. Vile vile nawapongeza Mawaziri wote na Serikali yetu kwa ujumla kwa kazi nzuri wanazoendelea kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nami nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ajili ya nchi yetu na kwa manufaa ya Watanzania wote. Leo tumepata taarifa kwamba amekutana na Profesa John ambaye ndio Mkurugenzi wa *Barrick*, amefika na wamekubaliana kwamba tukae chini tuongee na Kampuni ya *Barrick* imekubali kutulipa Watanzania sehemu ya fedha ambayo tunaidai na tutarekebisha mikataba kuifanya nchi yetu ipate manufaa makubwa sana kwenye machimbo ya madini mbalimbali ambayo tunayo hapa nchini. Mheshimiwa Rais amesimamia kwa niaba yetu wote Watanzania. Tuna wajibu wa kumpongeza na kumwomba ili aendelee na kazi hiyo vizuri, tuweze kunufaika kama Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijikita kwenye bajeti iliyopo mbele yetu, nianze na suala la maji. Kuna miradi ya maji kwa kweli inasuasua sana. Kama ahadi ya Mheshimiwa Rais inavyosema, ni kumtua ndoo mwanamke wa Tanzania, lakini kwa mwendo huu tunaokwenda, sidhani kama tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ya maji iliyopo katika Jimbo la Njombe Mjini, upo mradi wa maji ambao tumeambiwa kwamba tutapata fedha kutoka Serikali ya India, ni mkopo. Sasa hivi ni mwaka mzima, hakuna hata dalili ya hiyo fedha kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba *documents* na mikataba yote iko ofisini kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, kwa taratibu za nchi na nchi. Hebu tuombe sasa basi hiyo fedha ipatikane ili Mradi huu wa Maji wa Njombe Mjini uweze kufanyika, vinginevyo wananchi wa Njombe wataendelea kuteseka sana na kuona kwamba Serikali haiwajali. Mji wa Njombe jinsi ulivyo, umezungukwa na mito pande zote mbili; ni jambo la kusikitisha sana kwamba tunapokuwa Njombe tunakosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, miradi ya maji ya Njombe inasuasua sana na kinachofanya issues; na nimeshalalamika sana hapa Bungeni, inawezekana kabisa kwamba ndani ya Halmashauri ya Mji wa Njombe kuna shida ya wataalam. Tunaomba sana Wizara ya Maji na Umwagiliaji ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango waone namna gani wanaweza kutusaidia tupate wataalam wa kutosha waweze kusaidia hii miradi iweze kwenda ukiwemo Miradi Rugenge na Igogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha Miradi ya Maji ya Njombe nije suala la Liganga na Mchuchuma. Suala hili kwa kweli linasikitisha sana. Ni mradi ambao ni miaka mingi sana tumekuwa tukiuongelea. Wapo watu mpaka sasa wanazeeke wanaacha Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana ukizungumza habari ya Liganga na Mchuchuma, watu wanafikiri ni vitu ambavyo viko hapo hapo pamoja. Ni kwamba Liganga na Mchuchuma viko sehemu mbili tofauti na vina umbali zaidi ya kilometa 80. Kutoka Liganga kwenda Mchuchuma pana kilometa 80, lakini kinachotakiwa kuchimbwa ni chuma kilichopo Liganga na kuna makaa ya mawe yaliyopo Mchuchuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kuvuna chuma hivi ni kweli makaa ya mawe ya Mchuchuma yatatumika yote kwenye chuma? Kama makaa haya yana matumizi mengine, basi makaa yaanze kutoka. Hivi makaa yanahitaji *process* gani? Kwa sababu tunachojua sisi, kwa



mfano ukienda kule Ruvuma wanakochimba makaa ya mawe, kiko kile kijiko kinachimba na *crusher*, vitu viwili tu; na magari yanasomba yanasafirisha makaa. Tuombe na sisi yale makaa yaanze kutoka tuanze kupata manufaa yake. Vinginevyo tuambiwe kwamba makaa ya Mchuchuma yanatosha kwa ajili ya kiwanda cha Liganga tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dalili ya mvua ni mawingu. Tunapotaka kuchimba chuma cha Liganga na tunapotaka kuchimba makaa haya ya Mchuchuma yatasafiri kwa barabara. Barabara ya Itoni – Manda ni ya vumbi na ipo kwenye ilani iliyopita na ipo kwenye ilani hii. Tumeambiwa itaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha iliyopatikana ni kuanzia kipande cha kilometa 60 kuanzia Mawengi mpaka Lusitu. Sasa kipande hiki ni kidogo sana, sehemu kubwa ya barabara itakuwa bado ya vumbi. Kama kweli hiki chuma kitatoka, maana yake kutakuwa na malori yanayosafirisha chuma kwa sababu tumeambiwa uzalishaji ni tani milioni moja kwa mwaka. Ukifanya hesabu ya kawaida tu kwamba *Jory* libebe tani 30, ni malori 76 kwa siku yatabeba chuma. Kweli malori 76 yataipita barabara ya vumbi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi Wananjombe tunaona kabisa kwamba hatutendewi haki na hatuambiwi ukweli. Tunaambiwa tu kwa kuridhishwa kwamba huu ni mradi wa kielelezo, lakini hakuna cha kielelezo wala cha nini. Sasa tunasema tunataka kazi hii ianze, kama haianzi, basi habari ya kwamba Mchuchuma na Liganga ni mradi wa kielelezo, ifutwe na isiwepo, tuseme kabisa kwamba hii tumeiacha kwa sababu ni *depositya* miaka ijayo, karne ijayo na vizazi vijavyo. leleweke hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara sisi tunaihitaji, kwa sababu ukiacha Mchuchuma na Liganga, tunahitaji kusafirisha mazao. Chakula kingi kinatoka Ukanda wa Ludewa; viazi vinatoka Ukanda wa Ludewa, vije kwenye masoko yanayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Njombe – Ludewa inatakiwa iwe ya lami ili tusafirisha mazao. Kwa sababu tunaona katika nchi hii, sehemu nyingine zimetengenezwa barabara za lami, nasi tunahitaji barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ndugu yangu Mheshimiwa Hongoli pale amelizungumzia. Sisi Njombe miti na mbao ni zao kama mazao mengine. Sasa figisufigu na mizengwe inayowekwa kwenye mbao inatukatisha tamaa. Kwa sababu mkulima wa kawaida ana uwezo wa kuvuna miti yake na kuiza sokoni. Vinginevyo, tuambiwe kuanzia sasa ni marufuku wakulima kuvuna miti yao; na maana yake ni marufuku wasipande miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anapanda miti, anapasua; akifika barabarani anaulizwa mashine ya *EFD* kwenye mbao. Jamani, hebu Serikali ifanye kazi, muwe mnajua na mazao ya wananchi wenu, kwa sababu mbao ni mazao ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hiyo, kuna kitu kinaitwa *TP (Transit Pass)*. Sheria inasema, *Transit Pass* unadaiwa unapovuka Wilaya. Ndani ya Wilaya ya Njombe watu wanadaiwa *Transit Pass*; ukibeba kuni, *Transit Pass*; ukibeba mabanzi, *Transit Pass*; sasa inasikitisha sana kwamba wananchi hawa wanapanda miti; sehemu kubwa ya nchi hii haina miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Njombe kupanda miti ni maisha ya kawaida humhimizi mtu. Sasa bado wanakuja kupata adhabu kwenye kuvuna. Kama tunataka twende pamoja tutunze mazingira na mkumbuke kwamba ukanda ule una vyanzo vingi sana vya maji, basi tusaidiane. Kitu kama *Transit Pass* naomba Serikali itoe ufafanuzi kwamba *Transit Pass* ikatwe nje ya Wilaya. Kwa mfano, kama unasafirisha mbao kwenda nje ya Wilaya uwe na *Transit Pass*, mabanzi yasiwe na *Transit Pass*, kuni zisiwe na *Transit Pass* ili wananchi wale waone kupanda miti kwao ni sehemu ya maisha ya kawaida na waweze kuona neema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la vijana. Vijana wa Kitanzania tumewasahau jumla! Ni jambo la kusikitisha sana! Kama tunataka kujenga Taifa bora lenye vijana wanaoweza kufanya kazi na kuitetea nchi hii, ni lazima tuweke mikakati muhimu sana na kabambe kwa ajili ya vijana. Vijana wa Tanzania wale tu wanaomaliza Kidato cha Nne kwa mwaka ni vijana 400,000 kwa matokeo ya waliofanya mthani wa *Form Four* mwaka 2016. Waliochaguliwa kwenda Kidato cha Tano wapo 99,000. Vijana zaidi ya 300,000 wamebaki. Hakuna mpango wowote wa Kitaifa kuwasaidia. Kichaka tunachojificha ni asilimia 10 ya Halmashauri. Hivi *are we serious?* Vijana hawa watasaidiwa na asilimia 10 ya Halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali iseme upya kwamba vijana hawa tuwafanyie nini? Kama Wizara ya Fedha na Mipango mnataka fedha, tengenezeni walipakodi. Hawa ndio vijana walipakodi, wapewe maarifa. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikishauri hapa Bungeni, tuanzishe makambi kabambe kabisa ya shughuli za vijana, tuwawezeshe vijana kwa mkakati maalum ili vijana hawa waweze kuwa na kipato. Wakishakuwa na kipato watakuwa walipa kodi, lakini tunapowaacha hivi vijana 300,000 na mwakani 300,000 na mwaka mwingine 300,000, tunakuwa na vijana wazururaji, walalamishi, vijana ambao tutashindwa kuishi... (*Makoff*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Bura ajiandae.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia kwenye mjadala uliopo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema na baraka zake ambazo siku zote zimetuwezesha kuwatumikia Watanzania vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali inazochukua katika kuhakikisha maisha ya watu wetu yanaendelea kuboreka siku hadi siku. Tumekuwa na mjadala mrefu juu ya mambo ya makinikia lakini taarifa za hivi punde zinaonesha kwamba tunaelekea kwenye *right direction*, hongera sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 nilipochangia nilikuwa *bitter*, nilitumia lugha kali kwa Wizara hii na nilikuwa na sababu ya kufanya hivyo. Nilifanya hivyo kwa sababu Kamati ya Bajeti walikuja hapa wakalalamika kwamba Wizara hii imekuwa na shingo ngumu, ilikuwa haisikilizi ushauri inayopewa na Kamati. Nafurahi mwaka huu mambo yamebadilika. Wizara imekuwa sikivu, hongereni sana. Huo ni mwanzo mzuri, tuendeleo kuwa wasikivu, maana wote tunajenga nchi hii kuwatumikia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mapendekezo ambayo watu wengi humu tumekuwa tukipigia kelele ni kuongeza tozo ya mafuta ili twende kupata huduma za maji vijijini. Serikali imesikia hilo, imeongeza tozo kwenye mafuta. Wenzetu wa Kamati ya Bajeti wanashauri kwamba fedha yote itakayopatikana na ongezeko hili, asilimia 70 tuipeleke kwenye maji vijijini, asilimia 30 iende kwenye maji mijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunapiga kelele kuhusu maji vijijini? Kwa nini tunapiga kelele kuhusu huduma ya maji? Takwimu za Wizara ya Maji zinaonesha kwamba tumepeleka maji vijijini kwa asilimia 72 peke yake. Hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba takriban Watanzania zaidi ya milioni 10 vijijini hawana maji. Hatuwezi kuiacha hali iendeleo kuwa hivi. Lazima tuongeze nguvu kuhakikisha tunapeleka maji vijijini. Ndiyo maana naipongeza Serikali kwa kuwa sikivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimekuwepo hisia za hofu kwamba pengine uamuzi huu wa kuweka tozo umekuwa ni *blanket*, utagusa kila aina ya mafuta. Naiomba Serikali itakapokuja kuhitimisha hapa, itueleze tozo ile imewekwa

kwa mafuta ya aina gani? Vilevile, Wizara itakapokuja kuhitimisha hoja ituambie ina mkakati gani wa kuhakikisha tunafuta *Railway Development Levy* kwa mafuta ya ndege? Kwa sababu jambo hili limetusababishia kukosa biashara ya kuuza mafuta ya ndege kwa sababu kampuni za ndege zinajaza mafuta Kenya kwa sababu wenzetu hawakuweka *levy* hii. Kwa hiyo, naomba wakija watupe ufafanuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji nilisema mchawi wetu wa Tanga ni Wizara ya Fedha na Mipango. Nilisema hivyo *specifically* kwa sababu ya Kiwanda cha *Tanga Fresh*. Tunaingiza maziwa ya dola milioni 40; tuna uzalishaji wa maziwa hapa nchini lita bilioni mbili; lakini usindikaji tunasindika *only 1.4 percent*. Hii haiwezi kuwa sawa. *Tanga Fresh* kwa miaka miwili sasa wanahangaika kutaka kuongeza uwezo wa kiwanda chao wanazuiwa na *TRA*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanazuiwa na *TRA* kutumia majengo yao kama dhamana ya kukopea. Kwa sababu gani? Kwa sababu aliyewauzia majengo *Tanga Fresh*, alikwepa kodi. Mkwepaji kodi huyu anajulikana, anafanya biashara katika nchi hii. *TRA* wanaacha kwenda kumkamata mkwepa kodi, wanamuadhibu *Tanga Fresh*. Hii haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanga Fresh* wamemwandikia barua Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji; Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ameandika barua tangu mwanzoni mwa mwezi wa Tatu kuja Wizara ya Fedha na Mipango. Mpaka leo hatuna jibu. Nataka mtakapokuja kuhitimisha mtuambie, nini hatma ya Kiwanda cha *Tanga Fresh*? Kwa nini wanawaadhibu *Tanga Fresh* kwa kosa ambalo siyo la kwao? Kwa nini uzembe wa wafanyakazi wao usababishe *Tanga Fresh* wakose haki yao? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naipongeza Serikali kwa jitihada inazofanya za kuhakikisha suala la lishe linapewa kipaumbele. Tuna watoto milioni 2.7 waliodumaa; tuna

watoto 600,000 wenye utapiamlo; hii ni hatari kwa Taifa letu. Naipongeze Serikali kwamba kwa mwaka huu wameonesha *commitment* ya kutenga shilingi bilioni 11.4 zipelekwe kwenye Halmashauri zetu. Rai yangu ni kwamba tuhakikishe fedha hizi zinakwenda kwa wakati. Ziende zikaondoe baa hili. Pili, mtakapopeleka fedha hizi, mpeleke maagizo maalum kwamba huko kwenye Halmashauri fedha hizi zisibadilishiwe matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie sula la huduma za kifedha. Tunayo Taasisi inaitwa *SELF Microfinance*. Mwaka 2016 walipanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 12, lakini wakatoa shilingi bilioni tisa; mwaka huu 2017, wamepanga kutoa shilingi bilioni 20. Naipongeza sana taasisi hii kwa kazi kubwa inayofanya. Wakati nikiipongeza Serikali, hebu fanyeni mambo pale. Mmeondoa Bodi, haipo *in place*, wanashindwa kutoa mikopo kwa sababu bodi haipo. Harakisheni mhakikishe bodi inakuwa *in place* ili *SELF* iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni shilingi milioni 50 za kila kijiji. Fedha hizi hebu tuziwekee utaratibu maalum. Tumeshasema hapa kwamba njia nzuri ya fedha hizi kwenda kwa wananchi hebu tuhakikishe mfumo wa benki za jamii *(Community Banks)* unaimarishwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Bwanausi ajjandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini namshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kunipa muda wa kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mheshimiwa Dkt.

Ashatu Kijaji kwa kazi nzuri pamoja na Watendaji wengine ambao wapo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kila jambo chini ya jua lina makusudi; na sisi tumeletwa humu ndani kwa makusudi ya Mungu.

**MBUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Hata kama ulitumia njia zako za giza, lakini Mungu amekubali uingie humu kwa makusudi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Mungu kamweka kuwa Rais wa nchi hii kwa makusudi maalum.

**MBUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Kwa anayoyafanya ni makusudi ya Mungu anayoyatekeleza. Kwa hiyo, nawaomba Watanzania tudumishe amani, tudumishe umoja tunapozungumza mambo ya Kitaifa.

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Dkt. Magufuli, tumwombe kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema, amwezeshe kuwa na hekima na maarifa ya kufanya kazi hii kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tu. Kazi anayofanya ni kubwa, hawezi kuwa na marafiki. Marafiki wasioitakia mema Tanzania hawawezi kumpenda. Kwa hiyo, lazima tumweke kwa Mwenyezi Mungu kila siku. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Amen! *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Nampongeza sana kwa kazi nzuri anayofanya ya kusimamia rasilimali za Taifa hili. Nimesoma kwenye Mtandao kwamba Mwenyekiti Mtendaji wa *Barrick* kaingia Tanzania. (*Makofi/Vigelelele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaingia kwa ndege yake binafsi, kaja kuongea na Rais wetu kuhakikisha kwamba rasilimali, fedha ambazo hawakulipa wanalipa. Jamani, ningekuwa na uwezo ningesema Watanzania wote tumwombe huyu baba, Mungu ampe maisha marefu, lakini pia aendelee kumpa maarifa ya kutawala katika nchi yetu. Asiyemtakia mema na sisi tunamlaani kwa sababu Mungu alishatupa uwezo; ukimlaani mtu ambaye hakutakii mema na amani, analaanika. Kwa hiyo, yule ambaye hamtakii mema Rais wetu, atalaanika tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika baada ya kuona makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga sasa wataanza kuchimba na kiwanda kitajengwa pale na wananchi wanalipwa fidia. Tumelizungumza muda mrefu sana suala la Mchuchuma na Liganga na sasa imefika mwisho. Sasa tunaona matokeo ya Mchuchuma na Liganga. Nimeona kwenye bajeti kwamba na wananchi watalipwa fidia. Kwa hiyo, Tanzania chuma cha reli ambacho tunakitaka tutatoa Liganga kule ambako tutachimba chuma; lakini na vyuma, nondo kwa ajili ya ujenzi tutapata Liganga kwa sababu tutakuwa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watani zangu wale wa kutoka Bukoba, reli inajengwa, watakuwa wanafika baada ya siku moja tu badala ya siku mbili. Ndugu zangu wa Mwanza na Mara watakuwa wanasafiri kwa muda wa siku moja tu kwa sababu tunajenga reli ya *standard gauge*. Tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa juhudi kubwa na kazi kubwa anayoifanya ya kuwatetea Watanzania. Tulikuwa mvua ikinyesha tunalala Kilosa siku mbili, ukitoka Dar es Salaam unalala Kilosa siku mbili ndiyo ufike Dodoma. Kwa hiyo, hayo tena hatuna.



Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeze pia kwa ajili ya kuleta Makao Makuu Dodoma. Sitaacha kumpongeza Mheshimiwa Rais wangu kwa suala la Serikali kuhamia Dodoma. Nawashauri Wawekezaji, Waheshimiwa Wabunge, Dodoma viwanja vipo, fursa za uwekezaji ni nyingi, karibuni mwekeze Dodoma. Dodoma patakuwa pazuri kuliko Dar es Salaam kwa sababu tunajenga kufuata *plan* ya Mji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme habari ya kilimo. Nilipozungumza katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu niliomba kwamba suala la kilimo litiliwe mkazo kwa sababu tunataka viwanda, nchi yetu iwe ya viwanda; lakini je, tuna malighafi? Malighafi ya viwanda vya kilimo iko wapi? Nikapendekeza kwamba tuwatumie JKT katika suala la kilimo cha umwagiliaji, tutapata mazao ya kulisha viwanda vyetu. Pia tunaweza tukatumia Magereza wakalima kilimo cha umwagiliaji na tukajitosheleza kwa mazao kwa ajili ya viwanda vyetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *ranch* zetu sioni kama zinaweza ku-*feed* viwanda vyetu vya nyama. Hata hivyo, wafugaji bado hawajafuga ufugaji wa kisasa kiasi kwamba tunaweza tukalisha viwanda vyetu ndani ya nchi. Kwa hiyo, lazima tuwe na mikakati katika masuala ya kilimo, kilimo cha umwagiliaji, ufugaji wa kisasa lakini hata vijana wetu tunaweza tukaanzisha Makambi ya vijana kwa ajili ya ufugaji, kilimo cha *horticulture*, kilimo cha kisasa na tukawa na malighafi ya kutosha katika nchi yetu; na tukawawezesha hasa hawa wanaoandaa mbegu. Wazalishaji wa mbegu ni asilimia 35 tu wanazalisha, tunaweza tukawawezesha lakini kama hawawezi pia watu binafsi wanaweza kupata mikopo kutoka mabenki yetu na wakazalisha mbegu za kisasa kwa ajili ya kilimo chetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu vivutio vya utalii. Bado vivutio vyetu havijatangazwa. Tulipotangaza kidogo, Waisrael walikuja 600 kwenye utalii wa nchi yetu. Je, tukitangaza zaidi ya hapo tutapata pesa nyingi kutoka kwa watalii? Tuwafundishe watoto wetu utalii. Utalii ufundishwe mashuleni; vivutio vifundishwe mashuleni ili mtoto anapokua

ajue kwamba kuna vivutio vizuri ndani ya nchi yetu. Hapa ukiwauliza Waheshimiwa Wabunge wangapi wametembela Serengeti, Selous na Mikumi, inawezekana wasifike hata 50. Kwa hiyo, hatujatangaza utalii vya kutosha. Tutangaze utalii vya kutosha tutaopata fedha za kutosha kuendesha nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Sekta ya Uvuvi tuitangaze kwa kadri inavyowezekana ili hata doria zifanyike tuone kwamba Sekta ya Uvuvi inachangiaje pato la Taifa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma tuna *uranium* hapa Bahi, hatujaanza kuchimba. Tuna madini ya kutosha ndani ya nchi yetu; tuna *nickel* pale Itiso, Chamwino. Tukiweka sheria nzuri ambazo zitawabana wawekezaji kama Mheshimiwa Rais alivyoamua, tunaweza kuwa matajiri kiasi kwamba watoto wetu wakaishi maisha ambayo hawakuyatarajia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiseme kwamba Tanzania ni nchi maskini, sisi sio maskini na wala tusikae tunalaumiana. Juzi juzi nilimsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja anasema kwamba wawekezaji sio wezi, hawa wachimbaji wa madini sio wezi. Amesahau kwamba mwezi uliopita tu alisema kwamba wawekezaji ni wezi, kutokana na mikataba yetu. Tunataka kuijenga nchi yetu, tumetumwa na wananchi kuishauri Serikali. Tuishauri Serikali pamoja ili tusonge mbele katika mambo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Dabalo tunajenga Kiwanda cha Miwa na tumeshampata Mwekezaji, lakini huyu Mwekezaji hajapa hati ya kumiliki ardhi. Naiomba Serikali, mpeni yule Mwekezaji hati miliki aweze kujenga kile kiwanda na wananchi wa Dabalo ambao amewapa mikopo kwa ajili ya kulima miwa waendeleo na kile kilimo na viwanda viendeleo kuwa vingi vya kutosha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bwanausi na Mheshimiwa Ali Salum Khamis ajjandae.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Serikali. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Mpango na Dada yangu Mheshimiwa Dkt. Kijaji kwa kazi nzuri wanazozifanya na kutuletea bajeti ambayo imejenga matumaini makubwa sana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano kwa jinsi anavyofanya kazi. Nami nataka niseme tu, hii ni zawadi kwa Watanzania. Kama ambavyo nchi nyingine wanatamani Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli awe Rais katika nchi nyingine, sisi wote kwa pamoja tunatakiwa tuienzi hii tunu ambayo tumepata kutoka kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mjumbe aliyetangulia kusema hapa Mheshimiwa Bura, kwamba ziko taarifa kwamba yako matumaini makubwa ya kupata zile fedha ambazo Mheshimiwa Rais alikuwa anazisema, nashauri hizi fedha zikipatikana, basi baadhi ya sehemu kubwa ya fedha hizi zielekezwe kwenye mradi wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuzungumzia suala la uchumi bila kuhusisha suala la upatikanaji wa maji kwa wananchi wetu. Tulipendekeza kuanzia kwenye Kamati ya Bajeti lakini pia kwa Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba tungeweza kupata Sh.50/= kwa kila lita ya mafuta ili iende kwenye maji, lakini bahati nzuri imetengwa Sh.40/= kwa kila lita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa hizi fedha sasa zielekezwe kwenye maji ili ziweze kwenda kutusaidia kuwafanya Watanzania waweze kufanya kazi nyingine na kuhakikisha kwamba maji yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye uti wa mgongo wa Taifa letu ambao ni kilimo. Naishukuru Serikali kwamba imefanya juhudi sana za kuondoa tozo na kwenye korosho Serikali imeamua kwa mara ya kwanza kabisa kutoa *sulphur* bure kama ruzuku kwa wakulima wa korosho. Sasa isiishie tu kwenye kuondoa tozo, ni lazima tuelekee pia kwenye kuwatafutia masoko bora wakulima wetu ili waweze kupata masoko mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitembelewa na viongozi wengi hapa nchini akiwemo Waziri Mkuu wa India; na alipokuja alizungumza na Serikali na alizungumza na Mheshimiwa Rais, akatoa matumaini kwamba Serikali ya India iko tayari kushirikiana na Serikali ya Tanzania kununua aina zote za Kunde kwa maana ya choroko, kunde na mbaazi. Naomba Serikali iharakishe suala la mazungumzo na Serikali ya India. Hivi sasa Wakulima wa Wilaya ya Masasi na Mkoa mzima wa Mtwara kwa ujumla, waliitikia wito wa kulima mazao haya na choroko sasa ndiyo zinavunwa lakini bei imeshuka kutoka Sh.1,200/= hadi Sh. 400/= kwa kilo. Kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na juhudi ya kuondoa tozo kwenye mazao, lakini ihakikishe tunapata soko zuri la mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ninaotaka kuutoa kwa Serikali; hivi karibuni Kamati ya Bajeti ilipata nafasi ya kuzungumza na wenzetu ambao wanatusaidia misaada kutoka nje. Jambo ambalo limeonekana kuchelewa kupata misaada ya nje ni kwamba tunawatoza *VAT*, fedha zinazoletwa hapa nchini kwa misaada ya maendeleo, jambo ambalo Mataifa yanayotoa misaada yanakataa, kwamba sisi tunatoa misaada kuwaleteeni ninyi kwa maendeleo, kwa nini mtukate *VAT*? Kwa hiyo, naiomba Serikali hili suala liondolewe ili kuwafanya wafadhili wetu walete zile fedha zao bila vikwazo. Sasa tunalalamika kwamba fedha haziji

kumbe tatizo ni kwamba Serikali zile wamesita kuleta kwa sababu sisi tunawatoza VAT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nichangie ni juu ya Serikali kuona umuhimu wa kupeleka milioni 50 kwa kila kijiji. Fedha hizi zinahitajika sana kule, lakini iko haja ya kutazama pia upya jinsi ya kuzipeleka fedha zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri badala ya kwenda kuwagawia mmoja mmoja kwa ajili ya miradi midogo midogo, ni vizuri kuchagua mradi mmoja katika Kijiji na zile fedha zikatumika shilingi milioni 50 kwa ajili ya kusaidia kwenye maendeleo ya kile kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka nichangie kwenye bajeti hii, lakini kabla sijamaliza kuchangia nirudi kwenye kilimo kuwapongeza sana Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ole Nasha, wanafanya kazi kubwa sana na Watanzania wana imani nao sana kwenye Sekta ya Kilimo. Naamini kabisa wataongeza bidii ili kuhakikisha wakulima wanaweza kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye Sekta ya Viwanda. Ni lazima Serikali sasa tujielekeze kwenye suala la viwanda kwa moyo wa dhati kabisa na dhamira ya kweli. Tunavyo viwanda ambavyo kama tungevivufua tungeweza kuongeza uchumi wetu kwa kiasi kikubwa sana likiwemo zao la korosho. Tunavyo viwanda ambavyo vilijengwa, viwanda vile vikachukuliwa na baadhi ya watu wakisema watavivufua, lakini hadi sasa hawajafufua. Ni vizuri tukavivufua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza Serikali kwa kuwasaidia wakulima wa zao la tumbaku ambao kwa muda mrefu walikuwa wanalia, lakini naamini sasa wale wa Urambo, wale wa maeneo yote yanayolima tumbaku sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bwanausi, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Ali Salum Khamis, jiandae Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema nami kupata fursa hii kuchangia katika bajeti hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika mambo manne ambayo zaidi ya haya yatakuwa yanahusiana na mambo yale ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 133 inaeleza kwamba kunatakiwa kuwe na Kamati ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia katika Ibara ya 134 ikaeleza majukumu ya Kamati hiyo, lakini pia kulitakiwa kuwe na Akaunti ya Pamoja ya Fedha baina ya Zanzibar na Tanganyika ili kuweza kuthibitisha mapato ya Muungano katika Akaunti hiyo ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukichukua Katiba hii mwaka 1977, mpaka leo hii ni miaka 40 sasa hivi na hii imepelekea Zanzibar kukosa fursa zote za kufanya maendeleo ya visiwa vya Zanzibar kwa sababu ya tatizo hili la kutokupatikana *account* ya pamoja, kuweza kuyajua mapato halisi ya Muungano na mgao halisi kwa nchi mbili hizi. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie kwamba sasa ni lini Akaunti hii itafunguliwa kwa ajili ya kuweka mapato yote ya Muungano ili upatikane mgao sahihi kwa ajili ya nchi hizi mbili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuchangia hapa katika Wizara ya Fedha kusema kwamba ukiangalia Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaonesha mambo yote ni ya Muungano. Leo ukimwangalia Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Nyumba, anaitwa ni Waziri Waziri wa Ardhi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; lakini ukija huku ndani tunawatafsiria watu tunasema kwamba ardhi siyo

mambo ya Muungano, jambo ambalo Katiba hii ya Jamhuri ya Muungano inakataa inasema kwamba yule ni Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ina maana mapato na ukiangalia kwamba kodi ya Mashirika, watu binafsi, ushuru wa forodha; haya yote ni mambo ya Muungano. Kwa hiyo, ukitazama kwamba kodi hizi zinapokusanywa kabla hazijaanza kutumiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano inakua ni mapato ya Jamhuri ya Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa muda wote huu, imepelekea kulifanya Taifa la Zanzibar kuwa Taifa dhoofu, kuwa Taifa ambalo halijui mustakabali wake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa leo atuambie sasa ni lini Akaunti hii inafunguliwa kwa ajili ya kudumisha mustakabali wa nchi hizi mbili?

## TAARIFA

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mweyekiti, nataka kumpa mzungumzaji taarifa kwamba hamna Taifa la Zanzibar, kuna Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hamna nchi ya Tanganyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum, taarifa hiyo.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nafikiri Mheshimiwa hajaisoma Katiba vizuri. Katika Muungano huu mwanzo kulikuwa hakuna kitu kinaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kulikuwa na nchi ikiitwa Zanzibar ambayo mpaka leo inaitwa Zanzibar na nchi ambayo inaitwa Tanganyika. Tanganyika na Zanzibar ndiyo zimefanya kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa leo akitoa taarifa hiyo nitamshangaa sana. Kwa hiyo, naomba niendeleo na mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, atueleleze hii akaunti ambayo

imesemwa kwamba lazima kuwe na akaunti itakayothibitisha mapato ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, tuambiwe ni lini akaunti hii itaanzishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Visiwa ni tofauti na uchumi wa nchi ya Bara kama Tanganyika. Uchumi wa Visiwa siku zote ni uchumi wa huduma. Leo naomba nitoe mfano. Tuchukulle mfano wa nchi ya Singapore; Singapore ni Kisiwa kidogo, yaani kisiwa cha Unguja ni karibu mara mbili ya Singapore. Kisiwa hiki hakina *resources* za aina yoyote, isipokuwa wao wanatumia bandari na huduma ambazo wanatoa kwa Taasisi mbalimbali za kibiashara na kifedha duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo imekuwa kwamba Singapore, unapotaka huduma ya aina yoyote ya kifedha ama ya kibiashara unaipata Singapore. Ukiangalia leo Singapore wamewekeza katika bandari tu ya Singapore peke yake kwa siku inapokea makontena 91,000 ambayo ni sawa sawa na meli 60 zinazofunga kwa siku Singapore; na Kijiji chenyewe ni kidogo. Kama hiyo haitoshi, Singapore leo ndio wenye *destination* kubwa ya utalii. Meli zote za Kitalii ambazo zinakwenda katika sehemu mbalimbali duniani zinaanza safari zake kutoka Singapore.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa 2017 Singapore imefanya *location* ya meli za kitalii kwenda sehemu mbalimbali duniani 63. *Crew Ship* ambapo katika meli hizi watalii wanatoka Australia, Marekani, Ulaya na sehemu nyingine duniani wanakwenda Singapore. Wakifika Singapore wanapanda meli wanakwenda kwenye utalii wao, wakirudi wanarudi Singapore wanachukua ndege wanarudi makwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo cha ajabu, nashangaa, Mheshimiwa Waziri wa Utalii hapa kwetu, anashindwaje kuitumia fursa ya Zanzibar pamoja na Mbuga ama vivutio vya kiutalii vilivyopo Tanzania kuweza kuihuisha nchi hii kiuchumi? *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia Tanzania imekuwa maskini kwa sababu imeinyima fursa tu Zanzibar. Wakati aliyekuwa Waziri Mkuu wa Malaysia Dkt. Abdallah Mahadhir naye pia alikuwa na nia kama ambayo aliifanya Baba wa Taifa, kuifanya Singapore na Malaysia iwe ni nchi mmoja. Singapore wakakataa wakasema sisi tunataka tujiendeshe wenyewe na matokeo yake leo Singapore kwa kujiendesha wenyewe na kujitegemea imechochea maendeleo katika nchi ya Malaysia kwa haraka sana. Leo Malaysia ni miongoni mwa nchi ambazo zinakuwa kiuchumi kwa...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

#### TAARIFA

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji. Sekta ya Utalii siyo ya Muungano. Hayo mambo ya kuzungumza sijui tumewazuia, sijui Muungano, angezungumzia kule kwenye Baraza la Wawakilishi. Akaingiza watalii anavyotaka, asituletee ndoto za Alinacha za usiku. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu tafadhali. Inaonekana Mheshimiwa Keissy alikuwa hajasikia nazungumza nini, kwa sababu mwanzo nilinukuu hii Katiba. Hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano, inasema kwamba Waziri wa Utalii ni Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa sijui yeye anavyosema anafuata Katiba ipi? Kwa hiyo, inaonekana hata yeye mwenyewe hafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Singapore imechochea ukuaji wa kiuchumi wa nchi ya Malaysia na leo kila mtu anafananisha kwa kusema kwamba Malaysia inaendelea kiuchumi kwa haraka zaidi. Hii ni kutokana na Kisiwa cha

Singapore kuweka uchumi wa huduma na kuiacha Malaysia iweze kujiendesha katika uchumi wa mazao na kibishara kupitia Singapore.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunampongeza Mheshimiwa Rais kwamba amefanya kazi nzuri ya kusimamia rasilimali za nchi hii ili watu ambao walikuwa wanazipora, sasa nchi hii iweze kunufaika. Nachukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Rais kwamba kama ambavyo amechukua juhudi kwa ajili ya kuzuia makinikia, sasa umefika wakati sasa wa kupata suluhisho katika Muungano wetu. Mwisho hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitujibu kwenye bajeti yake kwamba jambo hili bado lipo kwenye mazungumzo baina ya nchi mbili hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikiwa leo tumeungana na sisi tunasema ni ndugu, miaka 40 hatujapata maelewano ya nchi hii kupata Akaunti ya Fedha ya Pamoja ya Jamhuri ya Muungano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona sasa ifike mahali, kama ambavyo mmekubali kwamba mlifanya makosa katika mikataba ya madini, basi na hapa mkubali kwamba miwakosea Wazanzibari na sasa tunaelekea katika mwanzo mpya kwa ajili ya kutafuta mustakabali wa Muungano wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ilikuja mifano mbalimbali. Mheshimiwa Rais Mstaafu alipendekeza, aliunda Kamati ya kutengeneza Katiba mpya; na tuliadini kwamba alikuwa na nia njema na Kamati hii ikafanya kazi ya Jaji Warioba, matokeo yake ilipokuja hapa Bungeni kwa sababu ile nia na dhamira ilikuwa bado, Katiba ile imekataliwa na matokeo yake watu wakatayarisha Katiba nyingine pendekezwa ambapo yale maoni ya wananchi yakakataliwa na yakatupwa pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alivyotokea Mheshimiwa Warioba, kutaka kutoa maelezo ya mambo yalivyokwenda, kilichofanyika, alitumiwa watu wa kwenda kumvamia na

asitoe ule uhalisia wa mambo. Leo hii watu wale wale wameonekana ni watukufu, wametukuzwa kwa ajili ya kuonekana ni watu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ahsante.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar na Mheshimiwa Bilakwate atafuata na tutamalizia na Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa dunia kwa kuweza kunifikisha katika hali ya uzima katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nawashukuru Viongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kufanya kazi kwa hali ambayo ni ngumu sana. Jambo la tatu, kabla sijaendelea kuchangia, naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Waziri Mpango ambayo ni hotuba ya Serikali, nimeshangaa kwamba hotuba nimesoma yote, lakini halijazungumziwa suala la ajira. Suala la ajira ni suala muhimu kwa kila Mtanzania. Tunaona watu wanamaliza Vyuho mamia kwa mamia, lakini mwisho wa siku wanaranda na vyeti vyao mifukoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Serikali hii inawapenda Watanzania ni bora wachukue suala hili walifanyie kazi vizuri sana. Kwa sababu suala la ajira ni muhimu kila mtu anapatia mahitaji yake. Nasema hivi kwa sababu wananchi wa Tanzania hawajapewa elimu ambayo

itawawezesha kujajiri. Pindi watapewa elimu ya kujajiri ndiyo hili suala ambalo pengine lingeweza kufanywa, kwa hivi liliyofanywa katika bajeti hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la kilimo; Kilimo ni uti wa mgongo. Marais mbalimbali walikuja na kauli mbiu mbalimbali. Kuna wengine ambao walisema Kilimo kwanza, lakini naona katika bajeti hii haijapewa kipaumbele. Kilimo kimedharauliwa, ukiangalia kwamba kilimo chetu kinakuwa kwa asilimia 1.7, hii ni kwamba Serikali hii ya CCM haijakipa kilimo kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kilitarajia kifikie asilimia sita ya kukua lakini mpaka sasa hivi kilimo kimefikia asilimia 1.7. Hii ni ndoto kwamba tutategemea Serikali ya Viwanda, Serikali ya Viwanda itakuwa haipo kwa sababu kilimo hakijapewa kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nakusudia kulizungumza ni kwamba Serikali hii katika bajeti yake Mheshimiwa Waziri Mpango, haijatuambia kwamba imetekeleza kupunguza umaskini kwa kiasi gani? Nimesoma bajeti hii lakini sijaona sehemu ambayo Serikali kama imejipanga na kama iko tayari kuwasaidia Watanzania kutuambia kwamba wamejipanga ni namna gani watapunguza umaskini Tanzania? Tunawaona akinamama na akinababa wanaangamia kutokana na kwamba umasikini umekithiri katika nchi hii ya Tanzania. Tukizungumzia umaskini ni kwamba, katika maeneo mengi wananchi wa Tanzania wako katika hali duni. Kwa hiyo, ni muhimu sana bajeti hii ilikuwa ielezee ni kiasi gani itapunguza umaskini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la *Motor Vehicle*. Katika bajeti hii tukiangalia ukurasa wa 48, tumeambiwa kwamba watu ambao wana magari wamesamehewa ada ya kulipa *Motor Vehicle*. Kiukweli ni kwamba ada hii haikutolewa bali imepelekwa kwenye vyanzo vingine. Ni jambo ambalo linawaumiza Watanzania

hususan watu ambao wanaishi vijijini. Tozo hii imewekwa katika mafuta ya taa Sh.40/=. Hii inamkandamiza mwanamke wa kijijini, inawakandamiza wananchi wote wa vijijini kwa sababu wao ni watu wa hali duni, kuwalipia watu wenye wanamaslahi makubwa, watu wa kati na wakubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukisema kwamba hatujamkandamiza Mtanzania ambaye yuko katika hali ya chini, hii itakuwa siyo kweli kwa sababu bajeti yetu imeonesha kwamba inawapendelea sana watu wa kati na matajiri kuliko watu wa chini. Kwa hiyo, naiomba Serikali, kama ikiwezekana, ada hii kama hawataki waiweke katika *Motor Vehicle*, basi waifute kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nitakalozungumzia ni kuhusu madini. Madini ni Rasilimali muhimu katika Tanzania hii. Ni jambo la kushangaza kwamba madini yetu yanaibiwa kila siku kwa sheria za ovyo ambazo zimetungwa na Serikali ya CCM. Leo hii wanakaa hadharani kutaka kujisafisha jambo ambalo haliwezekani. Ni bora kwanza waseme ukweli kwa sababu kulikuwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wa Kambi Rasmi ya Upinzani wakilizungumzia suala hili, lakini mkiwaona sio lolote sio chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Tanzania imeshaibiwa matrilioni kwa matrilioni ndiyo leo tunaona kwamba mtu au Kiongozi anatoka hewani na kusema kwamba tunaibiwa. Tumeibiwa sana na tutaendelea kuibiwa kama hatutarekebisha mikataba yetu na sheria zetu. Nasema hivyo kwa sababu gani? Tuna madini pia ya *Tanzanite* ambayo Tanzania pekee ndiyo ambayo...

## TAARIFA

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nataka nimpe taarifa mchangiaji anayechangia sasa kwamba Mheshimiwa Rais wetu hajatoka hewani kama anavyosema, ni Rais ambaye amechaguliwa kwa mujibu wa Katiba, kwa kura halali, kura za kishindo, kwa hiyo, ni Rais ambaye yuko Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo asiseme maneno yake kwamba anatokatoka tu hewani na afute haya maneno. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza taarifa hiyo siipokei, kwa sababu mimi sikumtaja kama ni Mheshimiwa Rais. Kama umejishuku itakuwa ndio huyo huyo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuchangia katika maoni yangu ni kwamba Tanzania hii ni pekee ambayo inazalisha *Tanzanite*, lakini leo kama hatuibiwi, Tanzania ni nchi ya nne ambayo inauza *Tanzanite*. Hivi nchi nyingine madini haya wanapata wapi kama itakuwa hatuibiwi? La muhimu ni kukaa tukaweza kurekebisha sheria zetu, zikaletwa hapa ili tuondoe janga hili la kuibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumza, ni kwamba... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ni kengele ya pili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye bajeti hii muhimu. Kwanza namshukuru

Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kipekee kumpongeza Mheshimiwa Rais, Jemedari wetu kwa kazi nzuri ambayo kwa kweli anaifanya katika Taifa hili. Kwa kweli tunamwomba kwa Mwenyezi Mungu amlinde, ampe afya njema, ampe nguvu, aendeleo kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya ambazo zinaonekana. Kuna watu wengine walikuwa wanasema aah, ndiyo tunaanza, siyo kusema ndiyo tunaanza, Mheshimiwa Rais ameshaonesha mfano mkubwa kwa kazi ambazo amezifanya, sina haja ya kuzieleza, wenye masikio wanasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Rais, kazi ambayo anaifanya mtu yeyote mwenye akili timamu ambaye ni mzalendo na Mtanzania, lazima apongeze kazi hii. Inasikitisha ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, anaposimama mtu ambaye anaona kazi kubwa iliyofanyika halafu anasema kilichofanyika ni upuuzi. Ni kitu ambacho kwa kweli mimi nimejuliza sana Waheshimiwa Wabunge sijui kama na nyie mmejiliza. Hawa watu wanadai wao ndio waliokuwa na hoja ya kusema hii mikataba mibovu haifai. Leo ni nini kilichowabadilisha? Wakati mwingine tunaweza tukaamini maneno ambayo yanayosemwa huko nje kuwa wengine kuna sehemu mmepelekwa ndiyo maana leo mmegeuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea leo msemi kwa kweli tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa hoja ambayo tulikujanayo, sasa leo ameishikilia na sisi tunaenda naye. Leo

mmegeuka, nini kilichowageuza wenzangu? Ni nani aliyewaloga? Huo upofu umetoka wapi leo? Watanzania wenye akili wanajua Rais anachokifanya na wanamuunga mkono na wanamwombea. Naamini Waheshimiwa Wabunge katika vita hii Mheshimiwa Rais atalindwa atatunzwa na hakuna kitakachomdhuru kwa sababu ni wakati wa Mungu kuitengeneza Tanzania. Ni wakati wa Mungu kurudisha vile ambavyo viliihiwa, ndiyo maana mmeona Mwenyekiti mwenyewe wa hiyo kampuni amekuja kwa ndege binafsi. Huu ni wakati wa Mungu, kwa hiyo, nyamazeni, Mungu yuko kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee bajeti yetu. Bajeti yetu kwa kweli ni nzuri, naipongeza sana, lakini niombe Wizara, Mheshimiwa Waziri Mpango kuna vitu ambavyo tukiwekeza nguvu Taifa hili litainuka kwa muda mfupi. Sehemu kubwa ya Watanzania, wakulima ndio walio wengi, lakini nguvu ambayo tumeiwekeza kwenye kilimo ni ndogo sana. Naiomba sana Wizara, tunasema tunaingia kwenye Tanzania ya viwanda, hivi viwanda vitapata malighafi wapi tusipowekeza kwenye kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuwekeze kwenye kilimo ili tuweze kumwinua mkulima. Kuna mazao ambayo ni muhimu, kwa mfano, kuna mazao kama kahawa. Mazao haya tumeyaacha kwa muda mrefu, lakini mazao haya kama kahawa, korosho, tumbaku na mazao mengine yanaweza kuliingizia Taifa hili pesa nyingi na tukamwinua mkulima na kipato cha Serikali kikaongezeka. Kwa hiyo, naomba sana hilo tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la viwanda. Nchi hii tumejipanga kwenda kwenye viwanda. Naomba sana Wizara yangu, ili tuwe na viwanda lazima tuwe na umeme wa uhakika ambao utaweza kuendesha viwanda vyetu; lakini ukiangalia bado uzalishaji wa umeme ni mdogo kulinganisha na jinsi ambavyo tumejipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Wizara iweze kuongeza nguvu tuweze kuzalisha umeme, tuwe na



umeme wa uhakika ndipo tutafanikisha Tanzania ya viwanda na tunapowakaribisha wawekezaji ili kuwekeza kwenye viwanda, pawepo na umeme wa uhakika. Kitu kingine kwenye viwanda, tuweke mazingira ambayo ni rafiki, mazingira ambayo hata wawekezaji wakija waweze kuvutiwa na mazingira ambayo ni rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa hizi tozo ambazo wameondoa kwenye mazao mbalimbali kama korosho na kahawa. Hili ni jambo ambalo ni zuri na litaweza kumwinua mkulima. Bado zipo tozo kwa upande wa kahawa na mazao mengine. Huyu mkulima amesahaulika sana na tunasema kilimo ni uti wa mgogo, lakini uti huu wa mgongo umesahaulika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, ni kengele ya pili hiyo. Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome na Mheshimiwa Ulega ajiandae. Mheshimiwa Salome dakika tano.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami niweze kuchangia bajeti hii japo kwa dakika tano. Nimesoma vizuri kitabu cha Mheshimiwa Waziri. Jambo kubwa lililopelekea tukashindwa kufanikisha bajeti iliyopita ni ukosefu wa fedha za wahisani. Kukosa fedha za wahisani Mheshimiwa Waziri anasema eti tulichelewa kufanya *negotiation* na wahisani ndiyo maana tulichelewa kupata pesa.

Mheshimiwa Waziri, wahisani wanatupa pesa pale tutakapokuwa tumetimiza masharti ya kupewa mikopo. Hatuwezi kupewa pesa kama Serikali yetu haizingatii utawala wa kidemokrasia, haizingatii utawala bora, uhuru wa vyombo

vya habari na tunapitisha Sheria kandamizi zinazowakandamiza Watanzania. Mheshimiwa Waziri angekuwa mkweli juu ya hilo, kwamba tunahitaji tusimamie utawala bora, utawala wa sheria na kila mtu awe chini ya sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwenye kitabu chake, ili tuweze kupunguza deni la Taifa, ameamua kuwekeza miundombinu kwenye maeneo ambayo yanachochea uchumi. Miundombinu hiyo anataja ni barabara, reli na ndege. Bajeti inapitishwa tunakwenda kujenga kiwanja cha ndege Chato; hivi kweli Tanzania nzima tukitafuta sehemu zenye vichocheo vya kiuchumi utataja Chato kweli? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chato wameweka *traffic light!*

**MBUNGE FULANI:** Eeh!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Inapita gari moja baada ya saa nzima ndiyo inapita gari pale. Wanaweka kiwanja cha ndege wanasema pale ndiyo kuna vichocheo, tupate pesa kwa ajili ya kuboresha uchumi kwenda kulipa deni la Taifa. Hizi ni ndoto ambazo haziwezi kutekelezeka. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka Sh.40/= kwenye mafuta ikiwa ni mbadala wa *Motor Vehicle Licence*. Kweli mafuta ya taa wataalam wetu waliosomeshwa na pesa za nchi hii wanasema tupandishe mafuta ya taa kwa sababu petroli imepanda, kwa sababu ndiyo njia pekee ya kuzuia uchakachujaji magari yasiharibike. Huo ndiyo utalam wa Wazalendo wa Tanzania waliowekwa kwamba tuwakandamize masikini kuokoa magari yasiharibiwe, mafuta yatachakachuliwa. Huo ndiyo utalam umeishia hapo. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Piga mama piga! (*Makofi*)

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sijaelewa vizuri kuhusu taratibu za manunuzi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha anapokuja atueleze; kweli bado tunazingatia Sheria ya Manunuzi Tanzania au ni mtu mmoja ndio anaamua tununue vipi, tufanye vipi shughuli za manunuzi Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba akija aje atueleze ni taratibu ipi ya manunuzi litumika kuwapa mkataba watu wanaokuja kujenga reli ya Dar es Salaam – Morogoro? Atueleze utaratibu upi ulitumika kununua zile ndege mbili ambazo mpaka sasa hivi inasemekana ndege moja iko *down*? Utaratibu upi ulitumika wa manunuzi kujenga barabara kwa pesa za uhuru barabara ya Mwenge – Morocco? Ni utaratibu upi umetumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo tulitegemea kuyaona kwenye bajeti hii ambayo sisi tulipitisha hapa sheria, watu wanakwenda kinyume na sheria, Bunge linadharauliwa kile tulichokifanya, halafu tumebaki tunacheka, tunapiga makofi, tunapongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi bado sijapata picha ya zile *propaganda* zinazoenezwa kuhusu suala la madini na migodi. Tunaonekana kwamba sisi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Makamba ahsante, dakika zako zilikuwa tano na ulipewa taarifa mapema. Sasa namwita Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia mjadala huu wa mapendekezo ya bajeti. Nami moja kwa moja napenda nichukue fursa hii kumshukuru sana

Mheshimiwa Waziri wetu Dkt. Mpango, lakini pia napenda nichukue fursa hii kumshukuru Naibu wake na timu nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, popo hajafahamika kama ni mnyama ama ni ndege mpaka hivi leo. Hawa wenzetu hata sitaki kuwaita ni vinyonga, naomba niwaite popo. Maana yake hawajafahamika *either* ni ndege ama ni wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo limewashuka! Walijigeuza kuwa ni Mwakili wa wale ambao sisi tumewatumu kwamba ni wezi wetu na yule mhusika mkuu amewathibitishia mchana wa leo, ameingia na amekiri mwenyewe kwa kinywa chake kwamba wako tayari kulipa pesa tunazotaka au tunazowadai. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Ndiyooo!

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tena lile liliokuwa linaonekana kwamba ni jambo gumu la kujenga *smelter* katika nchi hii amelichukua na amesema wako tayari kujenga *smelter* katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika, *our home land*; Afrika ina bahati mbaya, Wapinzani wa Afrika wamekuwa wakitumika na mabeberu miaka yote. Wale ni mfano wa *UNITA* na Savimbi wao ni *Tundu Lissu*. (**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UNITA* wametumika na mabeberu kuiangamiza Angola miaka yote, wale pia wanatumika na mabeberu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna kila sababu ya kutamba. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, eneo la madini ukurasa wa 32 Kifungu cha 35 (a) kinaeleza wazi wazi, "kuweka na kusimamia mfumo thabiti wa kukagua shughuli za migodi." Ukienda ukurasa wa 34, hiyo hiyo 35(k) utaambiwa.... (*Makofi*)

## TAARIFA

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Tayari umesharuhusiwa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, sema Mheshimiwa Kubenea, endelea.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mchangiaji anayechangia sasa hivi kwamba kimeo cha dhahabu alipewa Mheshimiwa Benjamini Mkapa, hajapewa Tundu Lissu. Kwa hiyo, kama kuna mabeberu wanaotumika ni viongozi waliopo madarakani, sio Mheshimiwa Tundu Lissu, naomba nimpe taarifa. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nataka nitoe tahadhari nyingine. Tulishatoa *ruling* asubuhi ya kuwataja viongozi wetu wastaafu na nafikiri Mheshimiwa Kubenea hukuwepo, kuna *ruling* ambayo tumeifanya leo ya kutokuwahusisha viongozi wastaafu kwa namna yoyote nyingine, kwa heshima yao na utendaji wao katika Taifa hili. Vile vile sitaruhusu mchangiaji yeyote humu ndani kuanza ku-*profile* kwa kutumia majina. Siyo utaratibu wa kikanuni na kanuni zetu haziruhusu. Kwa hiyo, hilo neno la Mheshimiwa Tundu Lissu, nalitoa kwenye *Hansard* na Mheshimiwa Ulega endelea na mchango wako.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alale mahala pema Profesa Chachage aliyeandika kitabu juu ya makuwadi. *Sasa hawa ni makuwadi na sisi tunajua kwamba hawa ni makuwadi wa Wazungu.* Leo taarifa yake kaka yangu Mheshimiwa Kubenea siipokei na najua juzi

alipata kichapo hapa cha *Comrade* Mwambalasa, sasa bado anaweweseka labda inawezekana. **(Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais.... *(Makofi)*

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ulega kaa chini.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64 (1) (a) na Kanuni ya 64 (1) ile ya maneno ya kuudhi. 64 (1) (a) maneno yasiyokuwa ya kweli, sisi Wapinzani sio makuadi. Makuadi ni wale waliouza madini kwa wageni tangu mwaka 1997/1998. Wale waliosaini mikataba, walipitisha sheria, wale ambao wamefanya nchi yetu imeibiwa mabilioni kama mnavyoyasema. CCM, ndio *makuwadi!* *(Makofi)* **(Neno Hili Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Nimetoa tahadhari na Waheshimiwa nawaomba tuzingatie Kanuni. Lugha za kuudhi, lugha ambazo hazitakiwi, naelekeza neno hilo nalo litolewe kwenye *Hansard*. Nimesikia kuna mtu anasema mbona hawa wanasema? Kiti hiki kikikaa, akiwepo Mheshimiwa Spika na wengine wote, kazi yetu kubwa ni kusimamia Kanuni. Tumeanza vizuri sana mchana leo; tumepita salama, tumalize salama. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Ulega endelea.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyotokea mchana wa leo hayawezi kupita hivi hivi, lazima kuna watu wahangaika. Yale mambo siyo mchezo mchezo! Wale Wazungu wakimwaga mzigo hata wa trilioni 10, 20 au 50 tu hapa, haya mambo tunayoyazungumza juu ya barabara zetu, juu ya maji, juu ya shilingi milioni 50 katika

vijiji, juu ya *SGR*, juu ya kuongeza ndege nyingine, juu ya maendeleo yote katika nchi hii, tutapaa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikwambie tu na Bunge hili pia, *Word Bank* wametoa ripoti na wame-*predict* Tanzania *is going to be the third fastest growing economy* katika Afrika. Itapitwa na Ethiopia kwa *8.3 percent*; itapitwa na Ghana kwa *7.8 percent*; sisi tutakuwa *7.2*. Hiyo ndiyo habari. Nataka nikwambie, ukitaka kuyaona hayo, ndiyo maana utaona watu wamekimbia siti zao leo, wametoka mbele wamehamia kule nyuma. Aibu! Eeh, habari hii ni ngumu! Hii habari ni nzito!

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Dkt. Mpango na timu yake msumari huo umeingia! Hatari sana haya mambo! Huyu JPM sio mtu wa mchezo mchezo, watu wanaweweseka, watu wamepoteza uelekeo! Haya mambo siyo ya mchezo mchezo! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi sasa katika bajeti yetu, natoa ushauri ili yale mapato yaendele kutuimarisha katika uchumi wetu. Dozi imeshaingia, hela za Morena zimepotea, basi tunasonga mbele. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi katika *blue* economy. Nasisitiza ya kwamba *fisheries*, kama Ilani yetu inavyoeleza, tunayo nafasi kubwa sana ya kuendelea kukuza kipato chetu kwa kutumia Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu, tununue meli tuhakikishe kwamba tunachakata na kufanya maendeleo mengine katika Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii pia kuelezea juu ya kilimo. Wapo watu hapa wamesema Serikali hii haishughuliki na kilimo wakija kwetu sisi tunaolima korosho tunaweza tukawapopoa kwa mawe. Sisi tumeambiwa msimu huu wa kilimo, korosho tutapata *sulphur* bure, mabomba ya kupulizia bure. Ni nani huyo anayeweza

kusimama hapa; Serikali imetuondolea zaidi ya tozo tano za kilimo, wewe leo unasimama unasema mambo yasiyokuwa na kichwa wala miguu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba sasa, sisi kama Taifa tunapoteza siyo chini ya Dola milioni 110 kwa kupeleka korosho ghafi nje ya nchi. Hiyo tukibaki nayo, tunao uwezo wa kutengeneza kiwanda cha kuchakata korosho na tukaweza kuuza na tukatoa ajira za kutosha. Tuweke mkakati maalum kabisa; ule uliowekwa na Bodi ya Korosho wa kuhakikisha tunatengeneza viwanda vyetu, basi hilo tusiliache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza wakati, katika bajeti hii nimeona mambo mengi; mojawapo ya jambo nililoliona ni misamaha mbalimbali kwa viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wote wamekwisha ilikuwa tu ni bahati mbaya kuna wengine wameachwa tu kutokana na muda ambao tuliutumia kwenye azimio, lakini tumekwenda vizuri. Nawashukuru kwa michango mizuri; na hii ya mwisho inaitwa jaza ujazwe. *(Kicheko/Makofi)*

Naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.  
*(Kicheko/Makofi)*

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 15 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*